# KUTATHMINI MABADILIKO YA USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA RIWAYA YA UTENGANO NA KAMWE SI MBALI TENA: UTAFITI LINGANISHI

**SHARIF JUMA FAKIH**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa, ameisoma tasnifu hii yenye mada: **Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena: Utafiti linganishi.** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya jamii katika Kiswahili Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

**Profesa Emmanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

.....

**Tarehe**

## HAKIMILIKI

Haki ya kunakili tasnifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali za kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili, Utafiti na Uchapaji kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## IKIRARI

Mimi, **Sharif Juma Fakih,** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote.

.....

**Saini**

.....

**Tarehe**

## TABARUKU

Kwa heshima na taadhima, natabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi: Mama yangu Bimkubwa Hussein Juma na marehemu baba yangu bwana Juma Faki Juma kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi sasa. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yenu na awajaalie muwe miongoni mwa waja wa Peponi kwa rehema na mapenzi yake (Amiin)

## SHUKURANI

Awali ya yote, anayestahiki kushukuriwa ni Mwenyezi Mungu mtukufu (Subhaanah Wataalah) kwa kuniumba, binadamu na kunijaalia uzima, afya, uvumilivu, uwezo, busara na hekima wa kuifanya kazi hii ya utafiti hadi kuimaliza. Kwa ufupi nastahiki kusema: Allhamdulillah Rabbil Allamiin. Namuomba M/Mungu anijaalie ziada za kheri.

Pili, shukurani zangu za dhati ziwafikie wazazi wangu wapenzi: Mama yangu Bimkubwa Hussein Juma na marehemu baba yangu bwana Juma Faki Juma kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi sasa. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yenu na awajaalie muwe miongoni mwa waja wa peponi kwa rehema na mapenzi yake (Amiin).

Tatu, Shukran zangu zisizo na ukomo zimfikie Msimamizi wangu Profesa Emmanuel Mbogo, ambaye amekuwa msaada na kiongozi mahiri katika tasnifu hii. Profesa Emmanuel Mbogo amenilea na kuniongoza bila kuchoka kinadharia na kitaaluma hadi kufikia kiwango kizuri, hatua ambayo hapo awali sikuwa nayo. Amekuwa akiisimamia na kufanya kazi hii bila ya kuchoka na kunitia hamasa kubwa niweze kumaliza kazi hii kwa wakati muwafaka. Sina budi kumuombea kwa Mola amlipe malipo mema (Amiin).

Sukurani zangu za pekee ziufikie uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT) kuanzia makao makuu Dar es Salaam hadi tawi lao la Pemba. Kwa kuwa chuo ni kikubwa, kwa heshima naomba niwataje baadhi: Profesa, Daktari,

Sheikh T.S.Y.M. Sengo, Profesa James Saleh Mdee, Dkt. Muhammed Omari Maguo, Dkt. Peter P. Lipembe, Dkt. Anna Kishe, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Zelda Elisifa, mwalimu Bakari Kombo Bakari, mwalimu Juma Rashid Khamis, mwalimu Nassor Ali Suleiman na wengineo. Hawa wote juhudi zao, mwamko, hamasa na maelekezo yao yamekuwa ni dira katika kufanikisha tasnifu hii kwa kiwango kizuri. Mungu awajalie umri wa mafanikio. Shukurani zangu za ziada zimfikie Profesa Said Ahmed Mohamed ambaye amekuwa akinisisitiza kusoma kwa bidii bila kukata tamaa.

Mwisho na kwa umuhimu mkubwa shukurani zangu za dhati ni kwa familiya yangu: Ndugu yangu Hamad Juma Faki na mkewe, pamoja na mke wangu kipenzi Wasila Othmani Ali kwa busara, juhudi, hamasa na uvumilivu wao mkubwa katika kipindi chote cha masomo hadi sasa. Vilevile napenda niwashukuru walimu na wanafunzi wote wa Skuli ya Sekondari ya Utaani - Wete - Pemba wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Mwanakombo Nassor Ameir na wasaidizi wake Mwalimu Rashid Sinani Massoud na Zaina Omar Othman kwa mashirikiano yao na mapenzi makubwa kwangu ambayo nayo yamesaidia kufanikisha vyema tasnifu hii. Mungu awatunuku neema na baraka za juu kwenu. Zaidi ya hayo yote naomba radhi kwa wote waliochangia kwa namna yeyote kufanikisha tasnifu hii na ambao sikuwataja.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika riwaya za *Utengano na Kamwe si mbali tena:* Utafiti linganishi. Utafiti huu ni utafiti linganishi ambao lengo kuu ni Kutathmini kwa undani ni kwa vipi mwandishi amekuwa na amebadilika katika kumsawiri mwanamke kupitia riwaya hizi mbili teule ikizingatiwa riwaya hizi zimepishana kwa miaka thelathini na nne (34). Riwaya ya *Utengano* ni katika riwaya za mwanzo (1980) na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ni katika riwaya mpya (2014) za mwandishi Said Ahmed Mohamed. Katika kufikia malengo ya utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa lengo la kumsawiri mwanamke na alitumia nadharia ya Fasihi linganishi kwa lengo la kutathmini kufanana na kutofautiana kwa usawiri huo wa mwanamke katika riwaya hizi mbili teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Mtafiti alibaini kuwa riwaya hizi zimetafautiana katika kumsawiri mwanamke na hii ni kutokana na mabadiliko ya wakati, mazingira, utamaduni na mahitajio ya mwanadamu ingawaje yako yanayofanana. Mfano katika usawiri wa mwanamke yanayolingana ni pamoja na mwanamke kama muhusika mwenye mapenzi ya dhati, daktari wa kienyeji, msimamo thabiti, muwajibikaji na mlezi wa familiya. Kwa upande wa kutofautiana, katika riwaya ya *Utengano* mwanamke amesawiriwa kama: Mshauri mwema, jasiri na mwenye kujitoa mhanga, mlevi, mwenye mipango na hadaa na mtenda rushwa. Katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* mwanamke amesawiriwa kama: Msomi, mpenda dini, msamehevu, yatima, mwenye huruma na imani thabiti, mwenye tamaa, jeuri na kiburi. Hali hii imedhihirisha kuwa, tabia njema ndizo zinazostahili kufuatwa na zile mbaya ndizo za kuachwa na ndio siri ya mafanikio.

## YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ..... ii

**HAKIMILIKI** ..... iii

**IKIRARI** ..... iv

**TABARUKU** ..... v

**SHUKURANI** ..... vi

**IKISIRI** ..... viii

**ORODHA YA MAJADWELI** ..... xvi

**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... xvii

**SURA YA KWANZA** ..... 1

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli wa Mada ..... 2

1.3 Tatizo la Utafiti ..... 6

1.4 Malengo ya Utafiti ..... 7

1.4.1 Lengo Kuu ..... 7

1.4.2 Malengo Mahsusi ..... 7

1.5 Maswali ya Utafiti ..... 7

1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 8

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake ..... 8

1.8 Mipaka ya Utafiti ..... 10

1.9 Muundo wa Tasnifu ..... 11

1.10 Hitimisho ..... 12

**SURA YA PILI** .....14

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** .....14

2.1 Utangulizi .....14

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali .....14

2.2.1 Maana ya Riwaya .....14

2.2.2 Maana ya Usawiri .....15

2.2.3 Dhana ya Wahusika .....16

2.2.4 Uainishaji wa Wahusika .....18

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi .....26

2.3.1 Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu riwaya za Said Ahmed Mohamed .....27

2.4 Mkabala wa Kinadharia .....34

2.4.1 Nadharia ya Ufeministi .....35

2.4.2 Nadharia ya Fasihi Linganishi .....45

2.5 Hitimisho .....51

**SURA YA TATU** .....53

**3.0 MBINU ZA UTAFITI** .....53

3.1 Utangulizi .....53

3.2 Maana ya Mbinu za utafiti .....53

3.3 Eneo la utafiti .....54

3.3.1 Uteuzi wa Eneo la Utafiti .....54

3.4 Kundi Lengwa .....55

3.5 Mbinu ya Usampulishaji .....57

3.6 Ukusanyaji wa Data .....58

3.6.1 Data za Awali (Msingi) .....59

3.6.2 Data za Upili (Fuatizi) .....59

3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data .....60

3.7.1 Mbinu ya Usomaji makini kupitia maktabani .....60

3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data .....61

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo .....61

3.9 Zana / Vifaa vya Utafiti .....62

3.9.1 Kalamu na Notibuku / Shajara .....63

3.9.2 Vitabu, Tasnifu, Makala na Majarida .....63

3.9.3 Kompyuta na Wavuti / Tovuti .....63

3.10 Hitimisho .....63

**SURA YA NNE** .....65

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI** .....65

4.1 Utangulizi .....65

4.2 Usuli wa mwandishi: Said Ahmed Mohamed .....65

4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Utengano (1980) .....67

4.4 Muhtasari wa Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena .....68

4.5 Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano .....70

4.5.1 Mwanamke Kama Mhusika Mshauri Mwema .....71

4.5.2 Mwanamke Kama Muhusika Muwajibikaji (Bidii Katika Kazi) .....73

4.5.3 Mwanamke Kama Muhusika Jasiri Na Mwenye Kujitolea Mhanga .....75

4.5.4 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Msimamo Thabiti .....77

4.5.5 Mwanamke Kama Muhusika Mlezi wa Familiya .....79

4.5.6 Mwanamke Kama Muhusika Tabibu / Daktari wa Kienyeji .....81

4.5.7 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Mapenzi ya Dhati .....82
4.5.8 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Tabia ya Ushawishi Na Uchochezi ..83
4.5.9 Mwanamke Kama Muhusika wa Mipango na Hadaa .....85
4.5.10 Mwanamke Kama Muhusika Dhaifu Na Masikini .....86
4.5.11 Mwanamke Kama Mhusika Mtenda Rushwa .....89
4.5.12 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe Kwa Mwanamme .....90
4.5.13 Mwanamke Kama Muhusika Mlevi .....92
4.5.14 Mwanamke Kama Muhusika Mgomvi (Mshari) .....94
4.6 Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena .....96
4.6.1 Mwanamke Kama Muhusika Muwajibikaji (Bidii Katika Kazi).....97
4.6.2 Mwanamke Kama Muhusika Mtambuzi na Mwanahistoria.....99
4.6.3 Mwanamke Kama Muhusika Mpenda Dini.....100
4.6.4 Mwanamke Kama Muhusika Tabibu/ Daktari wa Kienyeji .....102
4.6.5 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Huruma na Imani Thabiti .....103
4.6.6 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Msimamo Thabiti .....104
4.6.7 Mwanamke kama muhusika Mwanamabadiliko / Mageuzi. .....106
4.6.8 Mwanamke Kama Muhusika Mlezi wa Familiya .....107
4.6.9 Mwanamke Kama Muhusika Yatima Anayehitaji Msaada .....108
4.6.10 Mwanamke Kama Muhusika Msamehevu .....109
4.6.11 Mwanamke Kama Muhusika Msomi (Mwenye Elimu).....111
4.6.12 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Mapenzi ya Dhati .....113
4.6.13 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe Kwa Mwanamme .....114
4.6.14 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi .....115

4.7 Kufanana Kwa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya Teule ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena ..... 118
4.7.1 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Mapenzi ya Dhati ..... 119
4.7.2 Mwanamke ni Muhusika Mwenye Msimamo Thabiti ..... 120
4.7.3 Mwanamke Kama Muhusika Muwajibikaji (Bidii Katika Kazi) ..... 121
4.7.4 Mwanamke Kama Muhusika Mlezi wa Familiya ..... 122
4.7.5 Mwanamke Kama Muhusika Tabibu/ Daktari wa Kienyeji ..... 124
4.7.6 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe Kwa Mwanamme ..... 126
4.8 Kutofautiana Kwa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena ..... 128
4.8.1 Mwanamke Kama Muhusika Mshauri Mwema ..... 129
4.8.2 Mwanamke Kama Muhusika Jasiri na Mwenye Kujitolea Mhanga ..... 130
4.8.3 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Tabia ya Ushawishi na Uchochezi ..... 131
4.8.4 Mwanamke Kama Muhusika wa Mipango na Hadaa ..... 132
4.8.5 Mwanamke Kama Muhusika Dhaifu na Masikini ..... 133
4.8.6 Mwanamke Kama Mhusika Mtenda Rushwa ..... 135
4.8.10 Mwanamke Kama Muhusika Mpenda Dini ..... 138
4.8.11 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Huruma na Imani Thabiti ..... 139
4.8.12 Mwanamke kama Muhusika Mwanamabadiliko / Mageuzi. ..... 140
4.8.13 Mwanamke Kama Muhusika Yatima Anayehitaji Msaada ..... 141
4.8.14 Mwanamke Kama Muhusika Msamehevu ..... 142
4.8.15 Mwanamke Kama Muhusika Msomi (Mwenye Elimu) ..... 143
4.8.16 Mwanamke kama Muhusika Mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi ..... 145

**SURA YA TANO** ..... 147

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ..... 147

5.1 Utangulizi ..... 147

5.2 Muhtasari ..... 147

5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza ..... 149

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili ..... 150

5.2.3 Lengo Mahsusi la Tatu ..... 150

5.3 Hitimisho ..... 151

5.4 Mapendekezo ..... 152

5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma ..... 152

5.4.2 Mapendekezo kwa Serekali ..... 153

5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii ..... 154

5.4.4 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine ..... 154

**MAREJELEO** ..... 156

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadwali 4.1: Muhtasari wa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano.....95

Jadwali 4.2: Muhtasari wa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Kamwe Si Mbali Tena.....118

Jadwali 4.3: Muhtasari wa Kufanana Kwa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena .....128

Jadwali 4.4: Muhtasari wa Tofauti Ya Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano Na Kamwe Si Mbali Tena.....146

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACLA | American Comparative Literature Association |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| BCLA | British Comparative Literature |
| Bw | Bwana |
| DC | District Commishner |
| Dkt | Daktari |
| Dr | Doctor |
| FCLA | French Comparative Literature Association |
| GCLA | German Comparative Literature |
| Nk | Na kadhalika |
| OUT | Open University of Tanzania |
| PhD | Doctor of Philosophy |
| Prof | Profesa |
| RCLA | Russian Comparative Literature Association |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAMWA | Tanzania Media Women Association |
| TAWLA | Tanzania Women Lawyers Association |
| TGNP | Tanzania Gender Network Programme |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| TY | Tafsiri Yangu |
| UDSM | University of Dar es Salaam |

| | |
|---|---|
| Uk | Ukurasa |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UMATI | Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania |
| UN WOMEN | United Nation – Women |
| WAMA | Wanawake na Maendeleo |
| WODSTA | Women Development For Science and Technology Association |

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imehusu vipengele muhimu vifuatavyo: Utangulizi, Usuli wa mada, Tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, Maswali ya utafiti, Umuhimu wa utafiti, Vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, Mipaka ya utafiti, Mpango / muundo wa tasnifu na Hitimisho.

Utafiti huu umehusu mada isemayo: Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za *Utengano (1980)* na *Kamwe si mbali tena* (2014). Kiudhati lengo la mtafiti ni kutaka kufahamu msanii / mwandishi amekuwa na kubadilika kwa kiasi gani katika kumsawiri mwanamke hususan kupitia uandishi wa kazi zake hizi. Hii ni kwa sababu riwaya hizi zimepishana kwa miaka thelathini na nne. Yaani riwaya ya *Utengano* iliandikwa (1980) ikiwa ni miongoni mwa riwaya za mwanzo za mwandishi baada ile ya *Asali Chungu* (1977) *na Dunia Mti Mkavu* (1980) na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ni katika riwaya mpya ya mwandishi aliyoiandika (2014) baada ya riwaya ya *Mhanga nafsi yangu* (2012) na *Mkamandume* (2013)

Kwa muhtasari, mtafiti amekusudia kutathmini juhudi za mwandishi (Said Ahmed Mohamed) katika kumsawiri mwanamke kupitia riwaya hizo teule. Mtafiti ametathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke huyo katika hali zake zote: Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii, Kiutamaduni na Kimazingira.

## 1.2 Usuli wa Mada

Wasomi, wanafasihi na wanataaluma wengineo kupitia jumuiya zao wamejitahidi sana kufanya tafiti mbalimbali kuhusu mambo kadhaa yakiwemo ya jinsia, wanawake na watoto. Kwa ujumla wasomi na wanataaluma hao wametoa mchango mkubwa katika kumueleza mwanamke katika hali na tabia tofauti, juhudi zake, mafanikio na changamoto au vikwazo anavyokabiliana navyo, utetezi na namna ya kupambana na vikwazo hivyo. Baadhi ya tafiti hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

Ripoti ya Umoja wa Mataifa – UN WOMEN (2014) inayohusu *Usawa wa jinsia na maendeleo endelevu* inahitimishia kwa kusisitiza:

> …Msingi wa mafanikio katika jinsia ni kuwepo kwa usawa, uwajibikaji wa serekali na taasisi za kijamii kwa lengo la kuimarisha sheria, sera, mifumo na utekelezaji wa huduma za kijamii kwa usawa. Ufanisi wa haya unaambatana na ushirikishwaji sawa wa wanawake katika mambo matano ya msingi ya kimaisha, nayo: Wanawake na ushirikishwaji katika uongozi, kuzuia matumizi ya nguvu dhidi ya wanawake, ushirikishwaji wa wanawake katika amani na ulinzi, uhamasishaji wanawake katika kuinua uchumi, Usawa wa jinsia katika ngazi za mipango ya kimaendeleo na bajeti. (TY)

Maelezo hayo ni muhimu kwa mtafiti kwa sababu yamelenga kutetea ushirikishwaji wa wanawake kwenye mambo ya maendeleo, jambo ambalo hata wanawake wenyewe wana mchango mkubwa katika kufanikisha maendeleo yao kibinafsi, kifamiliya na kitaifa.

Mkutano mkuu wa kimataifa uliofanyika Beijing kuhusu wanawake (1995) ulipitisha maazimio kumi na mbili (12) ya utekelezaji kuhusu wanawake yaliyolenga kumjenga mwanamke kitaifa na kimataifa. Maazimio hayo ni:

> Wanawake na umasikini, elimu na mafunzo kwa wanawake, wanawake na afya, unyanyasaji dhidi ya wanawake, wanawake na migogoro ya kivita, wanawake na uchumi, mamlaka kwa wanawake na utoaji wa maamuzi, njia na mbinu mbalimbali za kuwainua wanawake, wanawake na haki za binaadamu, wanawake na habari, wanawake na mazingira na usichana wa kitoto. (TY)

Maazimio yote hayo ni ya msingi na yamestawi katika nyanja karibu zote za kimaisha na kimaendeleo kwa kila siku ambazo ni Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni. Sambamba na hilo maazimio hayo yamesaidia kuimarisha tasnifu hii kwa sababu yametoa fursa ya kumzindua mwanamke kwa ajili ya maendeleo yake na taifa.

Kwa Afrika, ripoti ya Jumuiya ya usawa wa jinsia Afrika (2015) inayofafanua kuhusu Uwezeshwaji wa wanawake wa Afrika kwa ajenda na matendo imelenga kuchunguza usawa wa kijinsia baina ya mwanamke na mwanamme kwa kuzingatia vipengele muhimu vitatu (3) ambapo kila kimoja kuna swali la msingi, navyo:

> Mosi, Usawa wa nafasi za kiuchumi. Swali linaloulizwa: Je kuna fursa sawa baina ya wanawake na wanaume katika biashara na ajira? Pili, Usawa katika upatikanaji wa haki za kibinaadamu na maendeleo. Swali linaulizwa: Je wasichana na wavulana wanafursa sawa shuleni? Tatu, Usawa katika sheria na taasisi nyenginezo. Swali linaloulizwa: Je wanawake na wanaume wana fursa sawa ya uwakilishi katika taasisi za kijamii? (TY)

Vipengele hivi vimesaidia kutoa sura kamili ya kutambua fursa za mwanamke katika maisha yao ya kila siku. Maelezo hayo yamekuwa ni kielelezo chengine katika kutambua kuhusu maisha ya mwanamke. Jumuiya nyengine zinazojihusisha kuhusu jinsia, haki na sheria, wanawake na watoto kwa Tanzania, ni pamoja na TAMWA

(1987), TAWLA (1989), TGNP (1993), WAMA (2006), WODSTA (1990), UMATI (1959) nk ambazo nazo zinatetea kuhusu jinsia, wanawake, watoto na maendeleo.

Kwa Wizara ya Maendeleo ya jamii, wanawake na watoto Tanzania kupitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000). Katika maelezo ya Utangulizi, Sura ya kwanza, mada ndogo: *Nafasi ya Wanawake katika jamii za Tanzania*, kifungu nambari kumi na moja kinaeleza:

> Katika mazingira haya wanawake hawajitokezi kiasi cha kutosha kugombea nafasi za uongozi na kwa jumla hawashiriki vya kutosha katika kutoa maamuzi ya taifa .Wanawake na hasa wa vijijini wanaofanya kazi ni asilimia themanini (80%) ya nguvu kazi iliyopo vijijini na huzalisha asilimia sitini (60%) ya chakula chote. Ingawa wao ndio wazalishaji mali wakuu, mazingira haya yanawafanya wasiwe na uamuzi wa mwisho hata juu ya mali waliyozalisha wao wenyewe. Halikadhalika katika masuala ya uzazi, wanawake hawana maamuzi. Kwa mfano, hawana maamuzi juu ya idadi ya watoto katika familiya ingawa wao ni wazazi na wanajukumu kubwa zaidi la ulezi wa watoto hao.

Kwa upande wa Fasihi ya Kiswahili, tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu mwanamke na kueleza umuhimu, thamani, heshima, juhudi na vikwazo mbalimbali anavyokumbana navyo na namna ya kupambana navyo. Miongoni mwa waliotafiti kuhusu mwanamke ni pamoja na: (Nung'o 1985, Chacha 1986, Lughano 1989, Momanyi 1998, Osoro 2003, Jilala 2008, na 2010/2011, Sengo 2009, Juma 2008, Lyatuu 2011, Waruguru 2013, Ann 2013, Mapunjo 2014, na wengineo). Baadhi ya mifano ya tafiti hizo ni kama ifuatavyo:

Sengo (2009) amefanikiwa sana kumchunguza mwanamke na kuweza kubaini ya kwamba mwanamke ana vyeo tisa (9) hususan katika familiya, navyo: Mama, mke, nyanya, binti, dada, shangazi, shemegi, mkwe na mamkwe.

Maelezo hayo yamemsaidia sana mtafiti katika mada yake ambayo imelenga kumsawiri mwanamke kwa kuangalia heshima, thamani yake na uwezo wake mkubwa wa kuweza kusimamia nafasi yake na hadhi yake. Mfano, mwanamke kuwa mama atabaki kuwa na jukumu kubwa la usimamizi na ulezi hususan wa watoto baada ya mume na analazimika kuilea na kuwaongoza watoto na familia hiyo katika misingi mizuri na iliyo bora.

Juma (2008) katika mada yake: *Kiswahili cha Asili cha kinamama wa visiwani Zanzibari;* amefanikiwa kueleza usawiri wa mwanamke unaojitokeza katika mambo yafuatayo: Lugha ya upole, lugha ya ushawishi, lugha ya mipasho, malezi na mafunzo, nasaha / radhi, mapenzi na mahaba, urembo na utanashati, majina ya kanga, sanaa na nyimbo.

Katika ufafanuzi wa aya iliyotangulia inatoa muelekeo mzuri wa matumizi ya lugha hususan kwa wanawake kupitia nafasi zao, uwezo na changamoto zake. Mwandishi wa mada hiyo amejitahidi sana kufafanua uwezo wa wanawake katika matumizi ya lugha kupitia nafasi zao visiwani Zanzibar. Dhana hii imemsaidia sana mtafiti kutambua mchango wa wanawake katika kukiimarisha Kiswahili kupitia usawiri wao katika maisha yao ya kila siku, si Zanzibar tu na hata Tanzania au duniani kwa ujumla ambapo juhudi hizo zimehusishwa na mada ya mtafiti kupitia riwaya teule.

Kwa upande wa Fasihi ya Kiswahili, mtafiti amebaini kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kutafiti juu ya nafasi au usawiri wa mwanamke ingawaje watafiti wamejitahidi kutafiti katika tanzu kama Fasihi simulizi, ushairi, tamthiliya na riwaya.

Mtafiti kupitia riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* amekusudia kutathmini usawiri wa mwanamke katika misingi mbalimbali, ikiwemo kutambua majukumu, thamani, heshima uwezo, haki, vikwazo na mapendekezo ya kutatua changamoto / vikwazo hivyo.

Kwa misingi hiyo ni imani ya mtafiti kuwa utafiti huu umefanikisha vyema dhana ya kumsawiri mwanamke na kutambua namna bora ya kumuendeleza au yeye mwenyewe kujiendeleza kwa maslahi binafsi na taifa au kimataifa ili na yeye awe mfano bora wa kuigwa na wenginewe kutoka kizazi hadi kizazi kwa kuzingatia mada ya mtafiti.

### 1.3 Tatizo la Utafiti

Katika kazi za fasihi mada ya usawiri au nafasi ya mwanamke imefanyiwa utafiti na wataalamu mbalimbali, mfano: (Nung'o 1985, Chacha 1986, Lughano 1989, Momanyi 1998, Osoro 2003, Jilala 2008, 2011, Waruguru 2013, Ann 2013, na wengineo). Wanataaluma hao wameweza kumueleza mwanamke katika misingi ya hasi na chanya. Pamoja na tafiti hizo, mtafiti amebaini kuwa bado hakuna utafiti linganishi uliofanywa kuhusu mabadiliko ya usawiri wa mwanamke baina ya riwaya ya zamani ya *Utengano (1980)* na riwaya ya sasa ya *Kamwe si mbali tena (2014)* za Said Ahmed Mohamed

Mtafiti amekusudia kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* ambazo zimepishana kwa miaka (34). Kwa ujumla mtafiti ametaka kujua mwandishi amekuwa na amebadilika vipi katika

kumsawiri mwanamke katika riwaya teule. Pia mchango wa mwandishi huyo katika kumsawiri mwanamke huyo kwa maslahi ya jamii husika na duniani kote.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanywa katika makundi mawili: Lengo kuu na malengo mahsusi.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena:* Utafiti linganishi.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i) Kufafanua usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

ii) Kufananisha usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

iii) Kutofautisha usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Ni kwa vipi usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena?*

ii) Ni kwa namna gani usawiri wa mwanamke umefanana katika riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena?*

iii) Ni kwa tofauti gani usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?*

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matumaini ya mtafiti katika utafiti huu yamejikita katika maeneo matatu (3):

**Mosi;** Utafiti huu umetarajiwa utasaidia sana kudhihirisha uwezo wa mwanamke, vikwazo anavyokumbana navyo na namna ya kuvitatua katika maisha yake ya kila siku.Sambamba na hilo utafiti huu utatumia kama ni njia moja wapo ya kuwazindua wanawake na kuwafanya waweze kuendelea kutetea haki zao ipasavyo kwa kujiamini.

**Pili;** Utafiti huu umetarajiwa kuwa ni nyongeza muhimu kitaaluma na kinadharia katika elimu na fani nyenginezo kwa walimu, wanafunzi na wanataaluma wengineo kama msingi wa marejeleo.

**Tatu;** Utafiti huu utakuwa muhimu kwa wengine kuchunguza nadharia ya Fasihi linganishi kwa kurejelea utanzu wa riwaya wa utafiti huu na hata tanzu nyenginezo katika Fasihi ya Kiswahili na nadharia nyenginezo.

### 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake

Utafiti ni kazi adhimu na yenye faida kubwa kwa mtafiti na umma ingawa ina vikwazo vyake. Mtafiti amekumbana na vikwazo vifuatavyo na baadae ameweza kuvitatua ili kufikia malengo ya utafiti huu vyema.

**Mosi, Uhaba wa Marejeleo:** Marejeleo ni mambo muhimu katika utafiti wa aina

yeyote duniani. Kwa kuwa mtafiti ni mkaazi wa kisiwa cha Pemba, mtafiti amekumbana na kikwazo kikubwa cha kupata marejeleo muhimu yenye kuhusiana na mada yake yakiwemo yale ya kazi tangulizi au tasnifu zenye kuhusiana na mada husika. Jambo hili linahitaji gharama na limechangia kuzorotesha kwa kiasi fulani kazi hii ya mtafiti.

**Utatuzi wa Kikwazo:** Mtafiti ametumia wavupepe/ tovuti (internet) na maktaba za Chuo Kikuu Cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), maktaba kuu Zanzibar. Maktaba zote hizo ni kutoka tawi la Pemba na kwa ujumla zimesaidia sana kufanikisha kazi hii kwa kiwango kizuri sana na cha mafanikio.

**Pili, Utumishi wa Umma:** Mtafiti ni mtumishi wa serekali, ni mwalimu Skuli ya Sekondari Utaani, Wete – Pemba. Kikwazo kikubwa ni kulazimika kutimiza majukumu ya shule aliyopangiwa ikiwa ni pamoja na kufundisha. Hii imepelekea muda mwingi kuutumia katika maandalizi ya majukumu ya shule na muda mchache ndio hupata kushughulikia kufanya utafiti. Hali hii imechangia kuzorotesha kazi hii kwa kiasi fulani.

**Utatuzi wa Kikwazo:** Mtafiti imemlazimu kutumia mwisho wa wiki na muda wa usiku zaidi baada ya kukamilisha maandalizi ya shule. Siku moja ya ruhusa kazini (Jumatano) nayo imesaidia kupunguza ukubwa wa kikwazo hichi. Hata hivyo kazi hii imefanikiwa kukamilisha katika muda muwafaka baada ya juhudi za ziada za utatuzi wa vikwazo.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika mada**: "***Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena: Utafiti linganishi".* Mtafiti anatambua vyema muandishi wa riwaya hizi *(Utengano na Kamwe si mbali tena)* ni mwandishi nguli, gwiji na mashuhuri aliyeandika vitabu vingi zaidi ya arubaini vikiwemo vya hadithi fupi, ushairi, tamthiliya na riwaya. Kwa upande wa riwaya mwandishi ameandika riwaya zifuatazo: *Asali Chungu (1977), Utengano (1980), Dunia mti mkavu (1980), Kiza katika nuru (1988), Tata za Asumini (1990), Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Nyuso za mwanamke (2010), Mhanga nafsi yangu (2012) Mkamandume (2013) na Kamwe si mbali tena (2014).*

Kwa misingi hiyo, mtafiti amezingatia na kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena* ambazo mtafiti amekusudia kujua na kutathmini kufanana na kutafautika, maendeleo, vikwazo na mapendekezo ya mtafiti kuhusu mwanamke na usawiri wake.

Mtafiti amechagua riwaya hizo akiamini hazijawahi kufanyiwa utafiti ikizingatiwa riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ni riwaya mpya ya mwandishi. Kwa hivyo mtafiti hatachunguza riwaya nyenginezo au mada nyengine akiamini riwaya zilizoteuliwa zimetosha na kufaa sana kufanikisha malengo na maswali yake ya utafiti vyema. Marejeleo mengine yametumika ili kusaidia kufanikisha mada ya utafiti ipasavyo.

Sambamba na hilo, Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani na uliongozwa na mbinu ya uchambuzi wa data ambayo ni mkabala au mbinu ya kimaelezo ingawaje

mbinu ya majadweli ilitumika kwa lengo la kurahisisha ufahamu na ni muhtasari wa maelezo tangulizi. Zaidi ya hayo utafiti huu ulitumia nadharia ya ufeministi hasa ufeministi wa Kiafrika kwa lengo la kumsawiri mwanamke na nadharia ya Fasihi linganishi kwa nia ya kulinganisha na kulinganua kwa usawiri wa mwanamke katika riwaya hizo teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena.*

### 1.9 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu wenye mada isemayo: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za Utengano* na *Kamwe si mbali tena: Utafiti linganishi* umegawanywa katika sura kuu tano (5) zifuatazo:

**Sura ya Kwanza – Utangulizi wa Jumla:** Sura hii imehusu vipengele muhimu vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, mipaka ya utafiti, mpango / muundo wa tasnifu na hitimisho.

**Sura ya Pili – Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia:** Sura hii imelenga vipengele vifuatavyo: Utangulizi, ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia: Nadharia ya ufeministi na ufeministi wa Kiafrika, nadharia ya Fasihi linganishi, na hitimisho.

**Sura ya Tatu – Mbinu za Utafiti:** Sura hii imehusu kuchambua vipengele vifuatavyo: Utangulizi, maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data, zana/vifaa vya utafiti na hitimisho.

**Sura ya Nne – Uwasilishaji, Uchambuzi wa Data za Utafiti:** Sura hii imejadili vipengele vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mwandishi Said Ahmed Mohamed, muhtasari wa riwaya ya *Utengano,* muhutasari wa riwaya ya *Kamwe si mbali tena,* usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano na Kamwe si mbali tena* na uhusiano wake na nadharia ya ufeministi wa Kiafrika, kufanana na kutofautiana kwa usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano na Kamwe si mbali tena* na mwisho ni hitimisho.

**Sura ya Tano – Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo.** Sura hii imezungumzia vipengele vya msingi vifuatavyo: Muhtasari wa kila sura (sura ya kwanza hadi sura ya tano) kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti husika. Sura imetoa hitimisho. Hitimisho hilo limelengwa kutambua juu ya tabia ya mwanamke kuwa ni binaadamu na ana mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii pamoja na mapungufu yake. Sambamba na hilo, sura hii imetoa mapendekezo. Mapendekezo hayo yameelekezwa katika maeneo ya msingi yafuatayo: Mapendekezo ya kitaaluma, mapendekezo kwa serekali, mapendekezo kwa jamii na mapendekezo kwa watafiti wengine.

### 1.10 Hitimisho

Sura hii imekuwa na umuhimu mkubwa kwa sababu imekusudiwa kujadili vipengele muhimu vya utafiti ambavyo ni dira katika utafiti wote wenye mada isemayo: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za Utengano na Kamwe si mbali tena***.** Katika sura hii vipengele vifuatavyo vilizingatiwa: Utangulizi, Usuli wa mada, Tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, Maswali ya utafiti, Umuhimu

wa utafiti, Vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, Mipaka ya utafiti, Mpango / muundo wa tasnifu na Hitimisho. Sura inayofuata (sura ya pili) inahusu; Mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imejikita kuzungumzia juu ya mambo ya msingi yafuatayo: Ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, Mapitio ya kazi tangulizi, Mkabala wa kinadharia na Hitimisho. Kwa misingi hiyo sura hii imeimarisha hususan kwa kurejelea kazi mbalimbali tangulizi zenye uhusiano na mada husika ili kujenga ithibati na umakinifu wa kutimiza haja ya malengo na maswali ya utafiti huu.

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali

### 2.2.1 Maana ya Riwaya

Riwaya si neno geni katika ulingo wa fasihi hususan Fasihi Andishi. Riwaya ni utanzu ambao fasili yake imefafanuliwa na wanafasihi na wataalamu mbalimbali kwa mapana na marefu. Miongoni mwa fasili za istilahi hii “riwaya” ni pamoja na hizi zifuatazo:

Ndungo na Mwai (1991:120) wanaeleza, Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mchangamano wa visa ambavyo huchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu Kimaudhui na Kifani.

Senkoro (1982:73) anafasili, Riwaya ni kisa ambacho ni kirefu vya kutosha chenye zaidi ya tukio moja ndani yake, ni kisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani wa mambo mbalimbali, riwaya ni

kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kutamba mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo muandishi.

Mulokozi (1996:149) anasema, Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi.

Madumulla (2009: 28) anaeleza, Riwaya ni masimulizi marefu ya kubuni yaliyo katika mtindo wa nathari, yakisawiri maisha ya mtu wa wakati maalum na kwa madhumuni maalum. Mtu huyo anasawiriwa akiwa anawasiliana na nafsi yake, mwenzake au jamii yake.

Muhando na Balisidya (1976) wanafafanua, Riwaya ni kazi ya kubuni, ni hadithi ambayo hutungwa kufuatana na uwezo wa fanani kuibusha mambo kutokana na mazoea au mazingira yake. Wanaendelea kusema kuwa riwaya yaweza kuanzia maneno 35000 hivi na kuendelea.

Kwa kuhitimishia tunaweza kusema: Riwaya ni aina ya utanzu wa Fasihi Andishi, ambayo ni hadithi ndefu ya kubuni yenye kutumia lugha ya kinathari , mchangamano wa visa na mikasa, wahusika wengi wenye kushikamana, pamoja na Fani na Maudhui iliyotimia kwa jamii husika.

### 2.2.2 Maana ya Usawiri

BAKIZA (2010: 357) wanaeleza, Sawiri ni kitendo cha kuchora sura ya kitu kwa

kutumia vifaa kama vile kalamu, penseli au chaki. AU, Sawiri ni kitendo cha kuunda sura ya mtu, kitu au jambo katika akili.

Msokile (1993: 97) anafafanua: Sawiri ni fanya sura ya kitu kwa kutumia picha/kalamu au mashine za kutolea picha. Kusawiri maisha ni kuunda kazi ya sanaa inayosawiri, inayoiga maisha kwa kuzingatia misingi ya maisha ya jamii inayohusika.

Kwa kuhitimishia tunaweza kusema: Sawiri / Usawiri katika kazi za fasihi ni kitendo cha kuwajenga, kuwaumba, kuwabebesha, kuwafafanua, kuwachambua na kuwadhihirisha wahusika katika kazi ya fasihi ili waweze kutenda matendo yao kwa misingi ya Maudhui aliyoyakusudia msanii / mwandishi katika kazi husika ya fasihi. Wahusika hao wanaweza kuwa binaadamu au viumbe vyenginevyo ambavyo vitateuliwa na kubebeshwa majukumu hayo na msanii kwa minajili ya matendo na maudhui ya kibinaadamu.

### 2.2.3 Dhana ya Wahusika

Katika uchambuzi / uhakiki wa kazi ya fasihi, Fani na Maudhui ni misingi muhimu. Fani hujengwa na vipengele mbalimbali kama muundo, mtindo, mandhari, lugha na wahusika. Wahusika ni mojawapo wa kipengele muhimu katika kazi ya fasihi. Wahusika ni dhana ambayo ndio msingi wa kujenga maudhui ya msanii/ mwandishi katika kuiumba kazi yake na kwa lengo la kufikisha maudhui kwa jamii alizozikusudia. Dhana hii ya “Wahusika” imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao:

Kamusi la Kiswahili Fasaha – BAKIZA (2010: 247) wanaeleza, Mhusika ni kiumbe kama vile mtu, kitu au mnyama mwenye kupewa dhima katika kazi ya Fasihi.

Senkoro (2011) anafasili, Wahusika ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi za fasihi.

TUKI (2004) wanasema, Mhusika ni mtu anayekuwa na kauli au uhusiano wa karibu na kitu au mtu fulani.

Ndungo na Mwai (1991:160) wanaeleza, Wahusika ni watu au hata viumbe viliochorwa na mwandishi kisanii ili kuwakilisha watu anaowafikiria katika kazi yake.

Msokile (1993:117) anafasili, Wahusika ni vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa; mfano katika hadithi kuna wahusika wanyama, watu, mimea n.k.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema, Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi, riwaya ikiwemo. Wahusika hawa wanaweza kuwa wanaadamu, wanyama, wadudu, madubwana, majini, mashetani, mawe na vitu vyengine visivyokuwa na uhai.

Wamitila (2008: 369) anafasili, Mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanaadamu.

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yeyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni “binaadamu” wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi. Msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika ndiyo kiini cha motisha au uhamasishaji wa wahusika. (Wamitila, 2002:18).

Kwa kuhitimishia tunaweza kufasili: Wahusika ni watu (binaadamu) au viumbe vyenginevyo kama wanyama, au vitu vyengine vinavyowakilisha matendo ya kibinaadamu ambavyo msanii au mwandishi katika kazi ya fasihi huviteua maalum kwa lengo la kuwasilisha Maudhui aliyoyakusudia kwa jamii husika.

Wahusika ni kipengele muhimu katika kazi yeyote ya fasihi. Ndio raslimali muhimu kwa msanii au mwandishi katika kuipa uhai kazi yake ya fasihi ili ionekane imelenga jamii iliyokusudiwa Kimaudhui. Msingi mmoja muhimu wa wahusika ni kupima tabia, mienendo, hisia, uwezo, utendaji, fursa, uwajibikaji, maadili, nidhamu, malezi, pamoja na wema au/na uovu wa wahusika, matendo ambayo hutendwa na wanajamii au watu (binaadamu) katika jamii husika.

### 2.2.4 Uainishaji wa Wahusika

Uainishaji wa wahusika sio jambo jepesi. Wataalamu mbalimbali wameainisha aina mbalimbali za wahusika. Baadhi ya wataalamu hao ni: Msokile (1993), Madumulla (2009), Wamitila (2008), Ntarangwi (2004), Njogu na Chimerah (1999), Ndungo na

Mwai (1991) na wengineo. Wataalamu wote hao wametoa mchango mkubwa katika kuainisha aina mbalimbali za wahusika. Mchango wao umekuwa na thamani kubwa katika utafiti huu kwa kuwa wahusika hasa wahusika wanawake ni nyenzo muhimu ili kufanikisha kiu ya utafiti huu vyema. Ufafanuzi wa aina za wahusika ni kama ifuatavyo:

### 2.2.4.1 Uainishaji wa Kwanza Wa Wahusika

Ndungo na Mwai, (1991:160-163) na Msokile (1993: 32 - 34) na Wamitila (2002: 21-22) kwa kumrejelea Forster (1927) wameainisha aina zifuatazo za wahusika:

#### 2.2.4.1.1 Wahusika Wakuu

Mhusika mkuu hasa ni yule anayehusishwa katika kazi nzima tangu mwanzo hadi mwisho. Ukuu wa mhusika unatambulikana kuambatana na dhima aliyopewa na msanii. Pia mhusika huyu huwa na maudhui ya kazi ile kuliko mhusika mwengine yeyote. Hata mara nyingine mhusika mkuu hutumiwa na msanii kama kinywa chake. Yeye ndiye husema na kutenda msanii anayoyapendelea yatekeleke katika jamii. Wahusika wakuu wana umuhimu mkubwa katika kazi ya fasihi na wao huwa ndio watendaji wakuu wakufikisha maudhui ya kazi ya mwandishi. Kawaida katika kazi ya fasihi muhusika mkuu huwa mmoja ingawaje wakati mwengine msanii anaweza kuchora jamii au kundi la watu kama wahusika wake wakuu. Wakati mwingine, baadhi ya wahakiki wamewaona wahusika hawa kuwa ni “midomo” ya wasanii.

#### 2.2.4.1.2 Wahusika Wadogo (Wasaidizi)

Hawa ni wahusika wanaomzingira mhusika mkuu na wanaomsukuma aamue au asiamue jambo kinyume chake wahusika hawa hujitokeza hapa na pale katika kazi ya

fasihi wakiwa na lengo la kuukamilisha ulimwengu wa kazi zao. Wahusika wadogo pia husaidia kuijenga dhamira fulani inayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Hawa wanaweza kuchorwa sambamba na mhusika mkuu ili kusaidia hadhira kumwelewa mhusika mkuu zaidi. Wao pia husaidia kuyajenga maudhui fulani katika kazi ya fasihi. Lakini mradi tu wao wametumiwa kusaidia kuyajenga maudhui yale wao wangali wasaidizi tu.

#### 2.2.4.1.3 Wahusika Wajenzi

Hili ni kundi linalotumiwa kujenga aina hizi zingine mbili za wahusika. Wao hasa hutumika kimsingi kuwakilisha jamii nzima ya kazi ile ya fasihi. Makundi yote haya twaweza kuwapata wahusika wa aina zingine tatu.

**Wahusika Bapa:** Hawa ni wahusika ambao hawabadiliki bali hubaki kuwa vilevile tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi ile. Hawa ni wahusika ambao hawabadiliki na hawakui katika mazingira ya aina yoyote. Yaani hawakui kifikra bali huwa wakimfuata mhusika mkuu tu. Aina za wahusika bapa ni: Wahusika bapa sugu na wahusika bapa vielelezo.

***Wahusika bapa sugu:*** Ni wahusika ambao wanajulikana kutokana na maelezo ya msanii au mwandishi. Huwa sugu katika hali zote za maingiliano yao na wengine, na sifa zao au jinsi wanavyoelezwa na mwandishi ni ile ile katika utokeaji wao wote. Mfano mzuri ni bwana Msa katika riwaya za Mohammed Said Abdulla.

***Wahusika bapa vielelezo:*** Hawa ni wahusika ambao hawabadiliki, na pia hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo na tabia zao. Majina ya wahusika hawa

huwa kama kielekezi na kifupisho cha wasifu wao. Mifano ya wahusika hawa ni Boramimi na Taadabuni katika riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert. Wahusika wa aina hii huelekea kuonyeshwa upande mmoja. Yaani msanii anatilia mkazo kwenye kipengele fulani cha tabia za muhusika na kuzisahau nyinginezo.

***Wahusika duara (mviringo):*** Hawa hujulikana pia kama wahusika mviringo. Kinyume cha wahusika bapa hawa hubadilika badilika kitabia, kifikra, kimawazo n.k. Pia mazingira yao huwaathiri; jambo ambalo ni hali halisi ya maisha. Zaidi ya haya, wao huwa na sifa nyingi. Kwa hivyo kinyume cha bapa, wao huwa na miraba mingi ingawa wanajulikana kifasihi kama wa miraba minne. Bila shaka hawa ndio wanaofanana na binaadamu wa kilimwengu kwani bila shaka maisha ya binaadamu huwa ya hali nyingi.

#### 2.2.4.1.4 Wahusika Jalbosi

Hawa huongozwa na mawazo ya wahusika wenzao. Ni kama kuwa bila ya wahusika wengine hawawezi kudumu na kuendelea.

### 2.2.4.2 Uainishaji wa pili wa wahusika

Njogu na Chimerah (1999) wameainisha aina kuu nne (4) za wahusika:

#### 2.2.4.2.1 Muhusika Mkwezwa

Ni muhusika mwenye sifa za kiutendaji. Ni hodari na shujaa kama wahusika wa fasihi simulizi. Muhusika huyu anajitokeza zaidi katika riwaya za Mohammed Said Abdulla (Bwana Msa) kupitia mpelelezi bwana Msa. Bwana Msa anajua siri zote, ni

stadi na anatumia mantiki kufikia kauli na uamuzi. Ameinuliwa lakini habadiliki licha ya mpito wa wakati. Muhusika mwengine ni Karama anayepatikana katika riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert na yeye ana sifa za aina hii ya muhusika.

#### 2.2.4.2.2 Muhusika wa Kisaikolojia

Huyu ni muhusika anayekumbana na matatizo mengi ya kijamii na anaibusha hisia za huruma kwa wasomaji. Mfano mzuri ni Rehema wa *Nyota ya Rehema*, na Yasmini katika *Vuta N'kuvute*.

#### 2.2.4.2.3 Muhusika wa Kimapinduzi

Huyu ni muhusika anayeelewa historia, siasa, mazingira na hali ya kiuchumi ya jamii yake. Yuko radhi kujitoa muhanga kubadilisha maisha ya wanyonge. Ana itikadi kali na msimamo thabiti. Mfano mzuri ni Rashidi katika *Kuli*. Kumba na Bakari katika *Dunia Mti Mkavu*.

#### 2.2.4.2.4 Muhusika Jumui

Huyu ni muhusika katika *Nagona na Mzingile*. Ni muhusika wengi katika mmoja. Hupatikana zaidi katika Fasihi ya kidhanaishi. Muhusika huyo mmoja anakuwa na sifa za wahusika wengi. Anatumiwa kuonesha fujo za maisha. Hivyo anaitwa muhusika jumui . Mfano muhimu ni "mimi" na "sisi"

### 2.2.4.3 Uaninishaji wa Tatu wa Wahusika

Wamitila, (2008: 382 - 391) kwa muhtasari ameainisha aina tano (5) za wahusika:

#### 2.2.4.3.1 Mhusika wa Jadi

Mhusika wa aina hii ni mhusika anayeweza kuelezwa kama muhusika wa zamani. Aina za wahusika jadi ni pamoja na: Mhusika wa Fasihi Simulizi, Mhusika wa Kitendi / kiepiki, mhusika wa kisasili na mhusika mkwezwa.

#### 2.2.4.3.2 Mhusika wa Kimuundo na Kimtindo

Msingi wa uainishaji wa mhusika wa aina hii ni uchunguzi wa sifa za Kimuundo na Kimtindo kuhusiana na wahusika wanaorejelewa. Aina za wahusika wa kimuundo na kimtindo ni: Mhusika wa kiuamilifu, mhusika wa kiishara na mhusika wa kinjozi.

#### 2.2.4.3.3 Mhusika wa Kihalisi

Msingi mkuu katika uainishaji wa wahusika wa aina hii ni kanuni ya Ushabihikweli. Aina za wahusika wa aina hii ni kama zifuatazo: Mhusika wa kimapinduzi, mhusika wa kisaikolojia na mhusika wa kidhanaishi.

#### 2.2.4.3.4 Mhusika wa Kisasa

Dhana ya usasa ni dhana ngumu na yenye utelezi mkubwa kwa sababu inaibua maswala ya kiepistemolojia na wakati: Usasa wa aina gani na usasa wa lini? Kiwakati tunaweza kumweka mhusika wa aina hii katika kipindi kinachoanzia miaka ya themanini. Kwanza, muhusika wa aina hii huwa na sifa zinazohusiana na riwaya zinazoandikwa kwenye misingi ya falsafa ya usasa ambayo kwa kufuata mawazo ya Udenguzi na Ubaadausasa. Hii ina maana ni vigumu kumzungumzia mhusika huyo kama binaadamu wa kawaida. Pili, Muhusika ambaye hana utunafsi wa binaadamu wa kawaida kutokana na kukiuka sifa na mipaka ya binaadamu wa kawaida na kwa

kuwa anaweza kuwa nyenzo ya kisitiari ya kuonyesha hali ya ulimwengu. Aina za muhusika wa kisasa ni kama zifuatazo: Mhusika jumui, mhusika wa kimwingilianomatini na mhusika batili.

#### 2.2.4.3.5 Mhusika wa Kitanzu

Kimsingi, sifa inayotawala katika sehemu hii ni sifa za utanzu ambao wahusika wanaozungumziwa wanapatikana. Aina za wahusika wa aina hii ni: Mhusika wa kitendi, mhusika wa kihistoria na mhusika wa kipelelezi.

Kwa kuhitimisha, pamoja na mchango mkubwa wa wataalamu walioelezwa hapo juu kuhusu aina mbalimbali za wahusika, kwa mtazamo wa mtafiti tunaweza kuhitimishia kwa kuwagawa wahusika katika makundi au aina kuu tatu (3) zifuatazo:

**Wahusika Wakuu:** Hawa ndio watendaji wakuu wa kazi ya mwandishi. Ndio roho au nguzo ambayo kikawaida mwandishi huwatumia kufanikisha Maudhui ya kazi yake husika katika Fasihi. Wahusika wakuu huitamalaki kazi ya mwandishi kuanzia mwanzo hadi mwisho na matendo mingi huwa ndio watendaji katika kazi ya fasihi. Wahusika wakuu hawa wanaweza kuwa wanaume au wanawake katika kazi husika ya fasihi. Kwa mfano katika riwaya ya *Watoto wa Mama ntiliye* ya Emmanuel Mbogo, muhusika mkuu ni Mama Ntiliye. Riwaya ya *Nyota ya Rehema* ya Mohammed. S. Mohammed, muhusika mkuu ni Rehema. Riwaya ya *Vuta Nkuvute* ya Shafi.A.Shafi, muhusika mkuu ni Yasmini. Riwaya ya *Utengano* ya Said A. Mohamed, muhusika mkuu ni Maimuna na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ya Said .A. Mohamed, muhusika mkuu ni Bi Chani, nk. Sambamba na hilo muhusika mkuu

Maimuna na Bi Chani ni wahusika muhimu na ndio ambao kupitia riwaya teule ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* mtafiti pia amewahusisha katika utafiti huu.

**Wahusika wadogo (wasaidizi):** Wahusika wa aina hii ni wale ambao huchukua dhima ya kuwasaidia wahusika wakuu kufanikisha Maudhui yaliyokusudiwa. Wahusika wadogo (wasaidizi) hutumika sambamba na wahusika wakuu kuendeleza Maudhui ya kazi ya mwandishi. Wahusika hawa ni wasaidizi lakini huweza kutoa mchango mkubwa hasa katika dhamira ndogondogo, ujumbe na mafunzo katika kazi ya fasihi. Mfano ni muhusika Mwajuma katika *Vuta Nkuvute,* Zita na Peter katika *Watoto wa Mama Ntiliye.* Bi Tamima na Bi Farashuu katika *Utengano.* Kwa ujumla katika utafiti huu, wahusika wadogo (wasaidizi) wamejitokeza na wamesaidia sana kuendelea kufanikisha mada ya mtafiti. Wahusika hao katika riwaya ya *Utengano* ni bi Tamima, bi Farashuu na biti Kocho na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* wahusika wasaidizi ni pamoja na Mwavile.

**Wahusika Wajenzi:** Hawa ni wahusika ambao kwa kiasi kikubwa hutumika kwa lengo la kujenga au kukamilisha Maudhui ya kazi ya mwandishi. Pia hutumika kushirikiana na wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Wahusika wa aina hii huwa ndio wengi katika kazi ya fasihi katika kudhihirisha matukio au dhamira mbalimbali katika jamii. Mfano wa wahusika hao ni: Nunu na Jerry katika *Mfadhili,* Hanifa na Chande katika *Vuta Nkuvute,* Salila na Jokha katika *Kamwe si mbali tena*. Mama Jeni na Dora katika *Utengano.* Katika utafiti huu wahusika wajenzi nao wamejitokeza, mfano katika riwaya ya *Utengano* ni pamoja na Dora, mama Jeni, Selume na biti

Sururu. Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe si mbali tena* wahusika wajenzi ni pamoja na Salila, Janet na Jokha.

Maelezo kuhusu uainishaji wa wahusika umemsaidia mtafiti kwa sababu wahusika ndio msingi muhimu katika utafiti huu. Katika kazi za fasihi, wahusika huweza kuwa jinsia ya kike au / na kiume, mtafiti amejielekeza uchambuzi wake katika wahusika wanawake kwa kuzingatia mada ya mtafiti isemayo: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena: Utafiti linganishi.*

Sambamba na maelezo hayo kuhusu uainishaji wa wahusika, dhana ya usawiri wa wahusika ni muhimu katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Ponera (2014: 170) anafafanua kwamba, usawiri wa wahusika ni kitendo cha kuwachora, kuwafafanua, kuwatambulisha na kuwajenga wahusika huku wakipewa maneno, matendo, hadhi na uwezo unaolandana au unaowiana nao.

Hivyo basi usawiri wa wahusika hasa wahusika wanawake umekusudiwa katika utafiti huu kuwa ni kuwajenga, kuwatambulisha, kuwadhihirisha, kuwafafanua na kuwachambua wahusika hao wanawake kwa kuzingatia nafasi zao, majukumu yao, vikwazo na utatuzi wake, uwezo wao, maneno na matendo yao ambayo huyatekeleza katika maisha yao ya kila siku kwa lengo la kujiletea maendeleo binafsi, familia na taifa kwa ujumla kwa kuzingatia mada ya utafiti.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi,

unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaonyeshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa pia nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data. (Enon, 1998).

Sababu kuu ya kuyatalii yale yote yaliyoandikwa awali kuhusu somo la utafiti ni kuhakikisha kuwa swali lililotafitiwa awali halirudiwi tena kwa kutojua. Kwa kufanya hivyo, sehemu hii imemsaidia mtafiti kumridhisha mdhamini wake kuwa kazi yake ikikamilika itakuwa mchango mpya katika nyanja ya taaluma anayoishughulikia (Buliba na wenzake, 2014)

### 2.3.1 Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu riwaya za Said Ahmed Mohamed

Profesa Saidi Ahmed Mohamed ameandika vitabu vingi (zaidi ya arubaini) vikiwemo vya riwaya, tamthiliya, ushairi na hadithi fupi na makala nyengine za kitaaluma. Mtafiti ameona kuna umuhimu mkubwa wa kufanya mapitio ya baadhi ya kazi tangulizi za mwandishi upande wa riwaya ambao ndio mtafiti anaoushughulikia ili kuweza kubaini juhudi zake na uwandishi wake hususan kuhusu mwanamke. Sambamba na hilo mtafiti ametaka kubaini juhudi za watafiti wengine kuhusu riwaya za Said A. Mohamed na michango yao kupitia maeneo mbalimbali likiwemo hasa eneo la wanawake ambalo mtafiti amejikita kulishughulikia. Miongoni mwa kazi tangulizi hizo ni kama zifuatazo:

Ann (2013) katika tasnifu yake: "*Usasa na Mwanamke wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya S. A. Mohammed".* Katika tasnifu hiyo mtafiti amebainisha sifa na

tabia kadhaa za muhusika mkuu wa kike wa riwaya hiyo ambaye ni Nana. Miongoni mwa sifa / tabia hizo ni: Mwanamke ni muhusika msomi, mwenye maadili, mwenye msimamo thabiti, mtunzi mahiri na mutribu wa kutajika, mwenye busara ya kuchanganua mbivu na mbichi, shujaa aliyejiamini, mwanafalsafa, mwenye bidii na kuwajibika, mkwasi na mkurugenzi, mwenye nidhamu na mipango, hodari na jasiri, mcha Mungu, mdadisi na mpekuzi wa mambo, mrembo na urembo wa kunata, mwenye huruma na asiye na ubinafsi, mjuzi, mwenye moyo wa kujirudia na mnyenyekevu na shupavu

Kwa ujumla utafiti huu umekuwa na umuhimu mkubwa kwa mtafiti kwa sababu imedhihirisha sifa na tabia lukuki za mwanamke zilizo njema na ambazo zinafaa kuigwa katika jamii ingawa kwa kuwa Nana ni binaadamu hataacha kuwa na mapungufu yake madogomadogo. Kwa upande mwengine utafiti huo imempa fursa mtafiti kutaka kujua nafasi au usawiri wa mwanamke katika riwaya ambazo mtafiti hakuzichunguza. Kazi tangulizi hiyo ilijikita kwenye riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kwa kuzingatia msingi mkuu wa muhusika mwanamke. Katika utafiti huu mtafiti amejikita katika ulinganifu wa riwaya za *Utengano na Kamwe si mbali tena* kwa kuzingatia pia usawiri wa mwanamke.

Wanjiru (2013) katika tasnifu yake isemayo: "*Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya Mpya: Babu Alipofufuka (Said Ahmed Mohamed) na Watu wa Gehenna (Tom Olali)"* Mtafiti katika tasnifu hiyo alijielekeza kudhihirisha dhana nzima ya Nadharia ya Uhalisia na Uhalisiajabu akidhamiria kwenye riwaya hizo tajwa. Kwa mfano katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* mtafiti amebainisha baadhi ya sifa na

tabia za muhusika mkuu K. Tabia hizo ni pamoja na K ni msahaulifu, K ni mwenye kiburi na anajiona yeye ni "Proteus" wa kutegemewa na hajui akifa watu watafanyaje? K ni mpenda raha na starehe na kila usiku saa tatu lazima aende Neo-Casino kufurahi na wenzake, K ni kiongozi anayewathamini wageni kuliko wenyeji, K ni mwacha mila na mwacha mila ni mtumwa, K ni kiongozi fisadi. Anafuja pesa za umma kwa kuanzisha miradi isiyo na manufaa kwa raia. K ni mbinafsi na hapendi kuhusishwa na umaskini, K ni kiongozi anayekataa mabadiliko.

Tasnifu ya Wanjiru (ameshatajwa) nayo imekuwa msaada mkubwa kwa mtafiti kupitia tabia mbalimbali mbaya za muhusika K ambaye anaonekana ni mwanaume. Katika tasnifu hiyo mtafiti amezingatia zaidi nadharia ya Uhalisia na Uhalisiajabu kupitia matendo ya wahusika wake katika riwaya ya *Babu Alipofufuka na Watu wa Gehenna*. Kwa mantiki hiyo mtafiti wa kazi hii sasa amepata mwanya mkubwa kutathmini usawiri wa mwanamke kwa kulinganisha riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena* na sio *Babu Alipofufuka na Watu wa Gehenna* ambazo hazitafiti.

Ruto (2015) katika tasnifu yake yenye mada isemayo: "*Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke".* Kwa ujumla katika tasnifu hiyo mtafiti amemuelezea mwanamke juu ya madhila na dhulma anazozipata kupitia maisha yake ya kila siku. Katika riwaya hizo mbili (*Kidagaa Kimemwozea* ya mwandishi Ken Walibora na *Nyuso za Mwanamke* ya mwandishi Said. A. Mohamed) mtafiti amemsawiri mwanamke katika matatizo anayokabiliana nayo yafuatayo: Ndoa za lazima, dharau, kutawishwa, kunyimwa haki za kuchuma mali na kurithi,

dhuluma ya kimapenzi na kukengeushwa na jamii. Sambamba na hilo mtafiti amebainisha athari kubwa zinazowakabili wanawake kutokana na matatizo / dhuluma hizo. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na: Kusambaratika kwa ndoa, kukata tama kwa wanawake, kukosekana kwa uhusiano mwema wa kinyumba, umauti, upweke na woga.

Kwa hakika tasnifu hiyo imeongeza ladha na kutoa sura kamili ya idhilali zinazowakabili wanawake katika maisha yao ya kila siku na kuona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwaongoza ili kuweza kuepukana na matatizo hayo. Kama hiyo haitoshi, tasnifu ya Ruto (ameshatajwa) imesaidia sana katika Utafiti huu kwa kuwa imezungumzia kwa kina juu ya usawiri wa mwanamke kupitia riwaya hizo mbili ikibainisha matatizo anayokabiliana nayo mwanamke na athari zake. Ingawa mtafiti hajishughulishi na riwaya hizo lakini riwaya hizo zimekuwa ni dira katika kuangazia usawiri wa mwanamke katika riwaya anazozitafiti za *Utengano na Kamwe si mbali tena.*

Walibora (2010) katika makala yake: "*Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum".* Katika Tasnifu hiyo mtafiti alichunguza uhusiano uliopo baina ya riwaya mbili hizo ikiwemo *Dunia Yao* ya Said Ahmed Mohamed akihusisha na kipengele cha Mandhari kama anavyosema:

> Kwa upande mwengine, mandhari ya kihistoria ya riwaya ya Mohamed ni baada ya Uhuru katika karne ya 21 kwenye nchi ya Afrika Mashariki iliyobanwa jina. Nchi yenyewe inakaribia kusambaratika kutokana na matatizo ya ndani kwa ndani na pia kutokana na kani zitokazo nje (ukoloni mamboleo na utandawazi). Ingawa Mohamed hasemi hiyo nchi ni ipi, unahisi ni kama Zanzibar alikozaliwa. Ama kwa kujua au kwa kutokujua waandishi hawa wawili wamo katika 'dayolojia'ambayo twaweza kuifasili kama

> mawasiliano au mazungumzo yanayowezesha kuigana na kuathiriana kimtindo na kimaudhui. Kwa msingi huo fasihi moja inasema au inajibizana na nyingine au kutoa mwangwi wa mambo yanayofanana au kulingana na yale ya fasihi nyingine.

Makala ya Walibora (ameshatajwa) imekuwa ni msaada mwengine kwa mtafiti kwa kuwa imesaidia kuonesha uumbaji wa mandhari na uhalisia wa mambo kadhaa anayoyazungumza mwandishi likiwemo suala la ukoloni mamboleo na Utandawazi. Pamoja na kwamba mtafiti hachunguzi riwaya ya *Dunia Yao* lakini suala la Ukoloni mamboleo na Utandawazi linahusu jamii ambapo wanawake na wao ni wahusika. Jambo hili la wanawake ndio msingi wa mada ya utafiti kwa riwaya hizi mbili teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

Traore (2008) katika makala yake isemayo: "*Familiya na Jamii katika riwaya za Said Ahmed Mohamed"* amechambua suala la familiya na jamii kwa kutumia baadhi ya riwaya za Said Ahmed Muhamed akitumia mifano ya riwaya za *Asali Chungu (1977), Dunia Mti Mkavu (1980), Utengano (1980), Kiza katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990) na Babu Alipofufuka (2001).* Kwa mfano makala hiyo imeeleza kama ifuatavyo:

> "…Mwandishi katika riwaya zake amechunguza kwa undani masuala kadha ya kifamiliya na kudhihirisha uhalisia wa maisha hayo na baina matabaka na jinsia mbalimbali zilizomo katika jamii tofauti. Mbali na hayo katika uwasilishaji wa uhalisia huo ametuonesha jinsi nafasi ya baba (mzazi) kama kiongozi na mtumishi wa umma na jinsi utawala wake katika mambo ya (urithi, usimamizi na udhibiti, uchumi na propaganda) ambayo nayo huchangia katika harakati za ukombozi na jamii hususan ya Zanzibar"

Katika makala hiyo mtafiti amenufaika nayo kwa sababu imekusanya riwaya kadhaa za mwandishi ambazo nazo kwa namna moja au nyengine nafasi ya mwanamke

imezingatiwa na kutoa fursa kwa mtafiti kuendelea kuchunguza dhana ya ushirikishwaji wa mwanamke katika jamii kama ni kigezo kimojawapo mshabaha na mwanamme katika jamii zetu kupitia usawiri huo wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

Aiello (1999) katika makala yake yenye kichwa kisemacho: "*Mabadiliko ni maumbile yenyewe: The Thematic and Stylistic Dynamism in S. A. Mohamed's novel Utengano"* Mwandishi anasema:

> " … Katika *Utengano* wanawake ni wahusika waliomstari wa mbele kutaka mabadiliko. Kazija, Biti Kocho, Farashuu , wote hao walisimama kidete kupambana na mfumo dume ambao haukuwa ukiwatendea haki na ambao ulikuwa ukiwatenga na kuwanyanyasa lakini hali hii ni tofauti na baadhi ya wanawake wengineo wa Zanzibar, wanawake hawa kwa upamoja wao walifanikiwa kuuwangusha utawala wa kidhalimu wa bwana Maksuudi na familiya mpya ilizaliwa ambayo haikuwa tayari kuendeleza udhalilishaji wa awali…"

Makala hii imejitahidi kuhusu juhudi za wanawake katika maendeleo ya jamii dhidi ya mfumo mbovu usiohitajika. Makala hii imefafanua maudhui ya riwaya ya *Utengano* kwa ujumla na haikujikita hasa kuchambua kwa undani kuhusu usawiri wa mwanamke ingawa suala la wanawake limezungumzwa. Kwa maana hiyo makala hii nayo imekuwa muhimu katika utafiti huu. Hii ni kwasababu mtafiti amejikita zaidi kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya kongwe ya *Utengano* na mpya ya *Kamwe Si Mbali Tena* jambo ambalo mtafiti anaamini bado halijatafitiwa.

Mwamzandi (2013) katika makala yake: *Riwaya teule za karne ya Ishirini na moja na udurusu wa nadharia za Fasihi.* Makala hiyo pamoja na mambo mengine muhimu

kuhusu riwaya alizozichagua za *Musaleo (2004)* ya mwandishi Kyallo W. Wamitila na riwaya za *Dunia Yao (2006) na Nyuso za Mwanamke (2010)* za mwandishi Said Ahmed Mohamed. Mwandishi alizungumzia nadharia mbalimbali zenye uhusiano na riwaya hizo pamoja na dhana ya utambuzi wa riwaya za kimajaribio. Mwandishi wa makala hiyo ametoa ufafanuzi wa riwaya hizo tatu zikiwemo riwaya za *Dunia Yao na Nyuso za Mwanamke* kama anavyosema:

> *Nyuso za Mwanamke (2010)* nayo inamwendeleza nguli wa kike, Nana, na jinsi anavyojinasua kimawazo kutokana na wavu wa ulimwengu wa kiume kwa kufuata kile kinachoridhiwa na moyo wake. Ni safari ya msichana, mwanagenzi wa maisha, anayeabiri kujua utu wake na sifa zinazo-mfafanua binafsi kama mwanamke, tofauti na wanavyotarajia wahusika wengine wa kike na wa kiume wa riwayani. (Mwamzandi, 2013:50)

> *Dunia Yao (2006),* imesheheni mijadala ya kifalsafa inayozamia fani mbalimbali za sanaa na swala zima la ubunifu. Ninachokiona zaidi ni swala la uendelevu wa sanaa ukiwemo uhai na ufaafu wake katika kuzungumzia visa visivyowaelea watu katika ulimwengu mamboleo. Dunia, inavyosema *Dunia Yao*, ni bahari isiyotabirika kina chake na sanaa haiwezi kuwekewa mipaka tunapoabiri kuizungumzia. Kama ilivyoparaganyika dunia, sanaa nayo haina budi kufuata mkondo huo kwani kuifuatilia dunia kwa mstari ulionyooka kama zilivyo kazi za kihalisia ni kuishi katika njozi.

Kwa muhtasari makala hiyo imekuwa na mahitaji muhimu kwa mtafiti kwa kuwa imechangia kutambua juhudi za mwandishi katika nafasi ya mwanamke na maudhui mengineyo. Mtafiti amezitumia makala hiyo kama nyongeza muhimu katika utafiti huu unaolenga *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za Utengano na Kamwe si mbali tena: Utafiti linganishi.*

Osore (2013) katika makala yake: *Uhalisia mazingaombwe na Uhalisiajabu katika riwaya ya Said Ahmed Muhamed ya Babu Alipofufuka.* Mwandishi amechambua

dhana nzima ya nadharia ya Uhalisia Mazingaombwe na Uhalisiajabu kwa kutumia ushahidi wa riwaya ya *Babu Alipofufuka.* Katika uchambuzi huo mwandishi wa makala hiyo alieleza kwa muhtasari maudhui ya riwaya hiyo kama ifuatavyo:

> "*Babu Alipofufuka* ni hadithi inayomzungumzia muhusika anayeitwa K aliyezaliwa kutoka familiya ya kimasikini wakati baba na mama yake walikuwa wakifanya kazi kwa mtu tajiri. Wakati wa ukubwa wake K alichaguliwa kuwa mbunge. Yeye alipenda kuishi maisha ya kifakhari wakati watu/ wananchi wake wakiendelea kuishi maisha ya kinyonge na umasikini wa kutupwa. K ni mbinafsi, mkandamizaji, mpenda sifa na asiyejali hisia za watu wake……"

Katika uchambuzi wa makala hiyo, mtafiti imemsaidia kutambua hisia za mwandishi katika kuwaumba wahusika wake na kuwabebesha majukumu mbalimbali likiwemo la uongozi, jambo ambalo hata wahusika wanawake wanaweza kuchukua nafasi hizo. Suala hilo la nafasi au usawiri wa mwanamke ndio msingi wa kazi hii ya utafiti ambayo mtafiti ameijadili ingawa amejikita katika riwaya za *Utengano na Kamwe si mbali tena.*

Kwa ujumla, mapitio ya kazi tangulizi ni miongoni mwa kipengele muhimu katika kuipa ladha na uhalisia, uhalali wa mada ya utafiti ili kuweza kubainika kuwa mada hiyo imestahiki kufanyiwa utafiti. Mtafiti baada ya kupitia kazi tangulizi mbalimbali zikiwemo tasnifu na makala amebaini kuwa ipo haja ya kufanya utafiti juu ya mada husika kwa kuwa bado haijatafitiwa ikilenga kutathmini usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano (1980) na Kamwe si mbali tena (2014)*

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Wafula na Njogu (2007) wanasema, Nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

Msokile (1993) anafafanua, Nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani.

Massamba (2009:63) anasema, Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo.

Wamitila (2002) anaeleza, Nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia.

Kwa ujumla: Nadharia ni jumla ya maelekezo, taratibu, kanuni, misingi, mfumo uliorasmi, mwongozo na mpango unaotumiwa na mhakiki au mtafiti ili kumsaidia kuifanikisha na kutekeleza kazi yake ya fasihi katika kiwango cha ufanisi zaidi.

Kwa hakika kila nadharia huwa ni muhimu na yenye ubora na mapungufu yake. Uteuzi wa nadharia bora inategemea uteuzi wa mtafiti kwa mujibu wa mada, malengo na maswali ya utafiti wake. Utafiti huu umekusudia kutumia nadharia ya Ufeministi na hasa Ufeministi wa Kiafrika pamoja na nadharia ya Fasihi Linganishi. Msingi mkubwa wa kuchagua nadharia hizi ni imani ya mtafiti ya kwamba nadharia hizi zitaweza kufanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti ambao ndio roho kuu ya utafiti huu. Nadharia zote hizo zimechambuliwa vyema kama ifuatavyo:

### 2.4.1 Nadharia ya Ufeministi

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza: Nadharia ya Ufeministi ni nadharia inayoyaangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii

inayotawaliwa na wanaume. Matatizo ya wanawake yanahusiana na yanasababishwa na jinsia. Hii ina maana kwamba shida nyingi zinazowakumba wanawake zimejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Kwa sababu ya jinsia, mwanamke amewekwa katika kitengo maalum cha jamii. Nadharia inayohusu masuala ya wanawake inajaribu kufichua matatizo yawapatayo wanawake kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake. Kwa mujibu wa wahakiki wa Kifeministi kama Birke (1986) na Lovenduski na Randall (1993) wanaeleza, Ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbali na wanaume wanaokubali jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopingana na mfumo dume.

Nadharia hii ya Ufeministi iliasisiwa na Mary Wollstonecraft katika makala yake ya *A Vindication of the rights of women* iliyochapishwa katika mwaka wa 1792 huko Uingereza. Katika makala yake ya kwanza kabla ya kushughulikia masuala ya wanawake alikuwa ameshughulikia haki za mwanamume. Makala yake yaliyotetea haki za mwanamke *A Vindication of the rights of women* yalikuwa na athari katika kumwaza mwanamke huko Uingereza na Marekani. Malengo ya mwandishi huyu yalikuwa kuonesha dhahiri anayoyapitia mwanamke katika jamii. Ufeministi uliendelea na huku ukipata kuungwa mkono na wengi. Wanawake wamekuwa wakipigania haki zao katika kipindi chote ambacho binaadamu ameitawala sayari hii. Kinadharia, masuala ya kifeministi yalianza kuzungumziwa karne (19) na kutia fora katika miaka ya 60 na 70 ya karne iliyopita ambapo wanawake, hasa wa Kimagharibi walianza kuzungumza juu ya matatizo yao kwa utaratibu, yaani katika machapisho.

### 2.4.1.1 Matapo mbalimbali ya Ufeministi

Wafula na Njogu (wameshatajwa) wameainisha matapo mawili ya Ufeministi.

#### 2.4.1.1.1 Ufeministi wa Kimaeneo

Katika tapo hili wanawake kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wanasisitiza masuala tofauti yanayowakabili. Miongoni mwa wahakiki waliojizatiti kuuainisha Ufeministi katika makundi tofauti ni pamoja na Mary Eagleton (1991). Ufeministi wa Kimaeneo umegawanywa katika sehemu kuu nne za kiulimwengu ambazo ni: Wafaransa: Wanawake wa Kifaransa wanatilia mkazo lugha. Wao wanaona kuwa lugha ndio msingi mkubwa unaomtetea mwanamume kuliko mwanamke. Lugha ya jazanda hutumika kuelezea uwezo, nguvu na mamlaka kwa wanaume na ilhali ile yenye kusawiria ulegevu na kutoweza ni kwa ajili ya wanawake. Wamarekani: Wanaungana na Wafaransa kuhusu matumizi ya lugha na kutilia mkazo namna yao ya kipekee ya kuandika na kujieleza. Pia wanashughulika zaidi na dhamira na kazi za fasihi kwa ujumla zilizotungwa na wanawake kwa wanaume lakini zinajadili juu ya wanawake. Waingereza: Wanawake hawa wanaiona dhima yao kuwa ni siasa. Wanafikiria wenzao wa Marekani wanazungumzia zaidi masuala ya kihisia na kisanaa na kusahau historia na siasa. Kwao, mambo ya historia na siasa ndiyo huathiri matendo ya wanawake. Waafrika: Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni: Kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, tohara na ukeketwaji wa wanawake, kimya cha kulazimishwa, desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa au kuzaa wasichana tu.

#### 2.4.1.1.2 Ufeministi wa Kiitikadi

Wafula na Njogu (2007) wakiwarejelea Adamson, Briskin na McPhail (1988) wanabainisha mitazamo mitatu ya Kifeministi: Ufeministi Huru**:** Hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Wakati mwingine ufeministi huu huitwa ufeministi wa kibepari. Hushikilia kuwa wanaadamu wameumbwa sawa, hivyo wanapaswa kuwa huru ili kutekeleza malengo na majukumu yao vyema. Ufeministi wa Kiharakati: Huu humuangalia mwanamume kama adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Waitifaki wa mkondo huu wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanaume kumdhalilisha na kumtawala mwili wake. Kwa hivyo, ili wanawake waweze kujitawala katika nyanja zote za maisha wanahimizwa wasiolewe na wanaume. Kinyume na haya wanahimizwa kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi. Ufeministi wa Kijamaa: Huu hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kitabaka inayompa uwezo mwenye kumiliki njia kuu za kuzalisha mali kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake, huendeleza utabaka na unyonyaji katika misingi ya kijinsia. Ufeministi huu unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyengine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za wanawake. (Wafula na Njogu, 2007).

Kwa muhtasari mtafiti kupitia matapo yote mawili yaliyoelezwa hapo juu (Ufeministi wa Kimaeneo na Ufeministi wa Kiitikadi) yamekuwa ni muongozo muhimu katika Kutathmini na kubainisha hatua za awali juu ya dhana ya ufeministi katika utafiti huu ambao umejikita katika usawiri wa mwanamke. Mtafiti kupitia maelezo hayo ameona kuwa kuna umuhimu wa kufafanua juu ya nadharia ya

ufeministi kwa ujumla ili kufikia hatua ya ufafanuzi wa nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ambayo ndiyo nadharia mojawapo muhimu katika utafiti huu. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetumiwa na mtafiti ili kufanikisha lengo na swali mahsusi la kwanza la utafiti huu ikifuatiwa na nadharia ya Fasihi linganishi ambayo imetumika kukamilisha lengo na swali mahsusi la pili na la tatu la utafiti huu.

**2.4.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi**

Wafula na Njogu (wameshatajwa) kwa kuzingatia matapo ya Kimaeneo na Kiitikadi wamefafanua mihimili ya nadharia ya ufeministi kama ifuatavyo:

i) Ni nadharia inayotumia Fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo.

ii) Nadharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinaadamu: Baadhi ya amali ni za kike na za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.

iii) Mtazamo huu vilevile unajaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa, wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe.

iv) Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

v) Nadharia hii hunuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona, na uhusiano wao na wa watu wengine.

vi) Hatimaye, lengo muhimu la nadharia hii ni kuvumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

Ntarangwi (2004) anaeleza: Nadharia hii hudhamiria kuonyesha uana na uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke ni mambo ya kati kabisa katika fasihi. Uhakiki huu pia hupiga hatua mbele na kuonyesha uhafifu wa hali ilivyo hasa katika nadharia nyingi za uhakiki. Wahakiki wanaozingatia nadharia hii hudai kwamba tahakiki za kijadi zimekandamiza mjadala kuhusu uana jambo ambalo yaelekea ni kwa manufaa yao. Kwa hivyo azma kuu ya ufeministi ni `kusoma upya' kazi za fasihi ili kusisitiza umuhimu wa vipengele vilivyopuuzwa na wahakiki wengi au ambavyo hawangeviona kwa sababu walikuwa wanafanya kazi katika nadharia za kijadi zinazomtukuza mwanaume.

Kwa mtafiti maelezo yaliyotangulia kuhusu Ufeministi yamekuwa muhimu sana kwa kuwa yameendelea kuonesha kwa uwazi jinsi wanawake si watu wa kuachwa nyuma na badala yake ni washiriki sawa kama wanaume ambao wanatakiwa kuamka na kuendelea kutetea haki zao ipasavyo na kwa maendeleo ya jamii zao.

**2.4.1.3 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika**

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika iliibuka mwanzoni mwa karne ya ishirini na iliasisiwa kwa mtazamo wa mwanamke wa Kiafrika. Waasisi wake ni pamoja na Filomena Steady (1981). Waasisi wa nadharia hii waliweza kuwa na mtizamo sawa juu ya masuala ya wanawake Afrika.

Steady (1981) anasema: Ufeministi wa Kiafrika umejikita katika mwelekeo wa kuangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayoegemeana na kukamilishana. Anaendelea kusema kwamba majukumu haya yanaenda sambamba na jinsia na hata husababisha hali ya usawa. Maswala ya ubaguzi, uana, utabaka na mielekeo ya utamaduni huletwa pamoja ili kuanzisha ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe wala sio kwa msingi wa kijinsia.

Ufeministi unachunguza utamaduni unaomlemaza mwanamke. Hili ni muhimu katika utafiti wetu ikizingatiwa kwamba katika tamaduni nyingi za Kiafrika dhana ya ukuu wa mwanamume dhidi ya mwanamke si swala geni. Dhana hizi za ubaguzi, uana na utabaka hazikuwepo katika utamaduni wa kiasili wa Kiafrika lakini ziliingia kupitia kwa athari za kikoloni na kibepari. Mabepari walitoa mchango mkubwa kupitia kazi ambazo zilitengewa wanaume na wanawake.

Mwasisi wa Ufeministi huu wa Kiafrika ni Filomena Steady (1981) anayefafanua matarajio ya nadharia yenyewe. Kwake, nadharia inafaa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazorutubisha unyanyasaji wa wanawake katika jamii. Nadharia yenyewe ina nyanja zifuatazo:

i) Inadhihirisha nia na malengo mahsusi yanayotokana na hali halisi katika jamii za Kiafrika.
ii) Inatambua historia ya jamii za Kiafrika, zilizokuwa na watawala na mashujaa wanawake.
iii) Inachunguza hali ya mwanamke katika jamii ambazo zimekuwa na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya.

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza mihimili ya kimsingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Wanasema ufeministi wa Kiafrika ni kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyonayo mwanamke wa Kiafrika ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, vilevile hujaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na ambao hawawategemei wanaume ili kujitambulisha. Aidha, kisaikolojia wawe ni wanawake wanaojielewa na kujiamini wala wasiwe wanahisi kama wana udhaifu kwa ajili ya uwanauke wao.

Kuibuka kwa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika nikutokana na mielekeo mikali iliyotoka Amerikani iliyochukulia kwamba mwanamume ni adui ya mwanamke na kamwe mwanamume hawezi kushiriki katika ukombozi wa mwanamke. Pia mielekeo hii huunga mkono ndoa za jinsia moja. Nadharia ya mtazamo kike yenye msingi wa Ufeministi wa Kiamerikani ndiyo yenye misimamo hii mikali. Wafuasi wake hudai kuwa ushirikiano mzuri ni wa baina ya wanawake tu. Kwa kuwa na baadhi ya arki au elementi ambazo haziuiani vyema na masuala ya mwanamke hasa wa Kiafrika. Nyingine waasisi wake walikuwa wanawake wa kimagharibi na kuandika kwao kulitegemea kuhadithiwa yanayofanyika, hivyo maoni yao na msimamo wao ukawa na athari ya kupotosha na kukengeusha.

Bara la Afrika kwa mtazamo wao ni kwamba, mwanamke wa Kiafrika huwa hana uwezo ila kudhulumiwa chini ya himaya ya ubabedume uliotiliwa nguvu na tamaduni na mila za jamii na ukawa umekita mizizi barani Afrika. Kutokana na hayo wanaharakati wa masuala ya mtazamo kike barani Afrika wamekuwa katika harakati

za kuwasilisha matatizo yanayowakumba wanawake wa bara la Afrika pamoja na ukombozi wao. Wito wa kutaka kupigania haki na usawa ilitokana na misimamo ya baadhi ya wanasaikolojia waliomchanganua mwanamke na kumpa nembo mbalimbali kulingana na mtazamo wao. Kwa mfano Mwanasaikolojia Freud (1927) alichangia pakubwa kuweka wazi suala la jinsia kupitia Nadharia ya Jinsia. Wanaharakati wa mtazamo kike na waliochangia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika kama vile Betty Friedan na Kate Millet walipinga vikali maoni ya Freud maana waliona yalidhalilisha na kumtweza mwanamke na kumtwaza mwanamume.

Simon de Beavoir (1949) katika makala iitwayo *The Second Sex* kama alivyonukuliwa na Wamitila (2002) katika *Uhakiki wa Fasihi* ni kuwa ulikuwa wa kuushambulia uana ambao ni dhana ya kitamaduni inayomwangalia mwanamke kama kitu hasi na duni na huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo. Pia alisisitiza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia kumdidimiza na kuwa mnyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha mwanamke akubali kuwa ni kiumbe duni. Baada ya kuikubali hali hiyo mwanamke kufanywa chombo na jamii yake cha kuendeleza utamaduni huo hasi.

Hivyo basi, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika haina budi kuzama katika mila, desturi na kaida za kijamii ili ibainishe usawiri wa mwanamke na uwezo wake katika utendakazi sambamba na anavyofanya mwanamume bali na kuangalia dhuluma atendewazo mwanamke katika ufanisi wake kulingana na ulimwengu ulivyo. Yanayoangaziwa na nadharia hii ni pamoja na mahusiano ya jamii baina ya mwanamume na mwanamke, asasi za jamii zilizojengwa na kuhimiliwa kwa misingi

ya uana, utamaduni wa kigeni na athari zake na maonevu mengine kama ukeketwaji, ndoa zisizo za hiari, ukewenza na udunishwaji. Yote haya hutiliwa nguvu na taasubi ya mwanamume.

Nadharia hii aidha hujishughulisha na masuala ya kuyamudu maisha ndani ya mfumo wa ugandamizwaji. Wanawake wa Afrika wanapigania haki zao kama vile kuweza kumiliki ardhi na mali, kuwa na uhuru wa kujiamulia bila dhuluma, suala la usalama wao katika utekelezaji wa kazi zao, kuthibiti ajira na ugawaji wa chakula. Masuala yote yanayorejelewa na nadharia hii juu ya dhuluma yamesawiriwa vyema katika fasihi ya Kiswahili. Mfano kupitia riwaya, waandishi wengi wamewasawiri wanawake katika hali mbili kubwa (hasi na chanya). Kwa upande wa hasi (matendo maovu) kama dhuluma katika mirathi, umiliki wa mali, ukatili na ukeketwaji, ndoa za kulazimishwa, ukosefu wa elimu, ubakwaji, makahaba, na chombo cha starehe kwa wanaume.

Kwa upande wa chanya (matendo mema) Fasihi ya Kiswahili imeweza kuwasawiri wanawake kama viumbe wenye umahiri mkubwa katika kufanya maamuzi bora, mashujaa wa kujitoa mhanga kupigania haki zao na za wengine na kuipiga vita mifumo ya udhalimu, wasomi waliobobea, washauri, walezi wazuri wa familiya na mengineyo. Mfano mzuri wa kazi za Fasihi ya Kiswahili zinazodhihirisha na kuipa nguvu Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni riwaya ya *Nyota ya Rehema* ya Muhammed S. Muhammed (1976), *Wasifu wa Siti binti Saad* ya Shaaban Robert *(1967), Utengano (1980), Nyuso za Mwanamke (2010), Kamwe si mbali tena (2014)* za Said A. Mohamed na nyenginezo.

Utafiti huu umejikita kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ili kuweza kufanikisha vyema lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu ambayo yamelengwa kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena.* Sababu kubwa ya kuchagua nadharia hii ni kwamba mtafiti anaamini kuwa nadharia hii ni muwafaka katika kutimiza lengo mahsusi hilo la kwanza na swali hilo la kwanza kuhusu usawiri wa wahusika wanawake katika riwaya teule. Tukizingatia kwamba wahusika wanaosawiriwa ni wanawake na kutathmini matendo yao mbalimbali yaliyo mema na yale maovu kwa kurejelea riwaya ya *Utengano na Kamwe si mbali tena* hasa katika Afrika. Kwa upande mwengine nadharia ya Fasihi Linganishi imetumika kusaidiana na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa lengo la kufanikisha malengo na maswali ya utafiti huu yaliyobakia. Nadharia ya Fasihi linganishi imetumika kutimiza haja ya lengo mahsusi la pili na la tatu pamoja na maswali yake ya pili na la tatu ya utafiti huu. Kwa kuzingatia riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*.

### 2.4.2 Nadharia ya Fasihi Linganishi

Jilala (2016:10-11) akiwarejelea Wellek na Warren (1949) wanaeleza, Fasihi Linganishi ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa Fasihi hata wanasayansi kwa kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Ulinganishi unaweza kuwa wa Fasihi ya Kiafrika na Kizungu au Fasihi ya Kizungu dhidi ya Kihindu nk. Aidha, Bassnett (1993) anaiona Fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya usomaji matini za tamaduni tofauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana.

Jilala (ameshatajwa) kwa upande wake anaeleza: Fasihi linganishi ni taaluma inayohusika na ulinganishi wa kazi za fasihi za ndani na nje ya mipaka ya kitaifa, kibara na kilimwengu. Hii ina maana kwamba kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Fasihi linganishi tunaweza kulinganisha kazi za ndani ya nchi, nje ya nchi, bara moja na bara jingine na hata Fasihi ya lugha moja na lugha nyengine , jamii moja na jamii nyingine na hata kazi za mwanafasihi mmoja za vipindi tofauti. Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa ulinganishi haufanyiki tu kama tukio la bahati nasibu, hapana! Mlinganishaji au mwanafasihi linganishi anapaswa kuwa na vigezo na misingi inayomuongoza na inayomfanya afanye huo ulinganishi. Kwa nini analinganisha? ni swali muhimu sana kwa mwanafasihi linganishi.

Boldor (2003) akimnukuu Remak (1971) anaeleza: Fasihi Linganishi ni taaluma ya fasihi inayovuka mipaka ya zaidi taifa moja na kuonesha uhusiano uliopo baina taaluma ya Fasihi na taaluma nyenginezo kama Sanaa (uchoraji, uchongaji, usanifu majengo na muziki), Falsafa, Historia, Sayansi Jamii (mfano: Siasa, Uchumi, Sosholojia), Sayansi, Dini na nyenginezo. Kwa ufupi, ni ufananishaji wa Fasihi moja na Fasihi nyenginezo na uhusiano wa taifa nyengine. (TY)

Zepetnek (1998) anaeleza: Fasihi Linganishi ni mbinu ya kitaaluma inayoangaziwa katika sura mbili kubwa: Kwanza, Fasihi Linganishi ni taaluma inayojishughulisha na lugha na fasihi ya zaidi ya taifa moja na maarifa hayo yanayotumiwa katika kustawisha taaluma hasa ya Fasihi. Pili, ni taaluma ambayo msingi na stadi yake kubwa ni kujielekeza katika itikadi ya kuzijumuisha Fasihi za jamii zote za

ulimwenguni ikihusishwa na tanzu nyengine ambazo hazipewi nafasi kubwa sana na kushughulikiwa (TY)

Kwa kuhitimishia: Fasihi Linganishi ni aina ya taaluma na nadharia ya uhakiki wa kazi ya fasihi inayojihusisha na uhusiano uliopo baina ya fasihi ya taifa moja na taifa jengine, mwandishi au waandishi wa jamii moja na mwandishi au waandishi wa jamii nyengine katika taifa moja au mataifa tofauti, mwandishi mmoja na kazi zake tofauti za fasihi kwa kuzingatia misingi stahiki.

**2.4.2.1 Chimbuko la Nadharia ya Fasihi Linganishi na Waasisi Wake**

Ponera (2014) anaeleza: Usuli wa dhana ya Fasihi Linganishi uko katika maneno ya Kifaransa *"la Literature Comperee"* yenye maana ya "*Compared Literature"* katika lugha ya Kiingereza na ndiyo yakatafsiriwa kama *"Fasihi Linganishi"* kwa Kiswahili. Baadaye, hukohuko Ulaya, dhana hii ilipewa majina mbalimbali kulingana na vipindi ilivyovipitia. Miongoni mwa majina hayo ni *"Fasihi Linganishi ya Kihistoria","Fasihi Linganishi ya Kisasa", "Fasihi Linganifu ya Kimataifa"*

Dhana ya Fasihi Linganishi ilianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa (19) na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya ishirini (20). Inaaminika kuwa fukuto la kuipatia dhana ya Fasihi Linganishi umbo lililonayo sasa lilianza huko Ufaransa mnamo karne ya kumi na tisa ikijikita sana katika tamthiliya. Hii ni kwa sababu tanzu nyingine kama riwaya bado zilikuwa changa sana. Maarifa ya awali ya taaluma hii yalijikita kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na mambo yazungukayo kama vile dini, siasa na matabaka.

Wadau wakubwa wa Fasihi Linganishi mwanzoni walikuwa watu binafsi wachache waliokuwa wanafanya kazi kipwekepweke. Hawa walitoa mchango mkubwa sana katika kuitangaza na kuieneza dhana hii. Mifano michache ya watu hao ni Paul Van Tieghem ambaye aliendesha makongamano huko Sorbonne kati ya mwaka 1827 na 1840. Pia aliandika makala na vipeperushi kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi na kuvisambaza katika sehemu mbalimbali huko Ulaya. Katikati ya miaka ya 1800 kulikuwa na machapisho mengi ya Fasihi Linganishi kwa lugha ya Kifaransa yakiwa yametolewa na Dostoevsky na Marius Franco. Mwaka 1886 Hutchenson Macaulay Posnett alitoa andiko zito kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi kwa Kiingereza na kufanya dhana hii ienee katika nchi nyingi za Ulaya Magharibi. Wataalamu wengine waliotoa mchango katika taaluma hii ni Alezander Veselovsky na Fyodor Buslaev wa Urusi, Johann Wolfgang von Goethe wa Ujerumani na Hugo Meltzl de Lomnitz (Ponera, 2014)

Mtaalamu mwingine, na ambaye ndiye nembo ya taaluma hii kwa sasa, ni Steven Totosy de Zepetnek. Zepetnek ni Profesa wa uga huu ambaye amejipatia umaarufu sana katika karne ya ishirini (20). Amejikita katika kulinganisha tamaduni na asili za jamii mbalimbali na baadaye mawazo yake yakaathiri dunia nzima. Zepetnek ni mwana – Fasihi Linganishi aliyejihusisha pia na taaluma za sayansi. Alizilinganisha taaluma za sayansi na taaluma nyinginezo zinazohusu Tamaduni, Filamu, Fasihi, Habari na Mawasiliano. Zepetnek alihariri na kutunga kazi mbalimbali za Fasihi ki-ulinganishi. Akiwa Chuo Kikuu cha Martin Luther aliandika, kuchapisha na kuhakiki kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi takriban vitabu ishirini (20) na makala (120). Mojawapo wa vitabu vyake maarufu ni: "*Comparative Literature: Theory, Method*

*and Application (1998)"* Pia alijishughulisha na kutafsiri makala mbalimbali zilizohusu lugha za Kijerumani, Kichina, Kifaransa, Kihungaria, Kiitaliano, na Kipolandi. Kwa kufanya hivyo, alisaidia kuikuza na kuieneza Fasihi Linganishi ulimwenguni (Ponera, 2014)

Kwa hivi sasa, mashiko ya taaluma ya Fasihi Linganishi yameongezeka duniani kote. Zaidi ya kuwa mojawapo ya masomo maarufu katika Vyuo vikuu vingi, pia katika baadhi ya Vyuo vikuu hivyo, Fasihi Linganishi imefanikiwa hata kuwa na hadhi ya kuwa kitengo au idara inayojitegemea. Fasihi linganishi yamtaka mdau wake azitalii kazi za vipindi mbalimbali kama vile kazi za "Zama za Giza" hadi zile za "Zama za Ufufuo na Ustaarabu", za kabla ya ukoloni hadi baada ya ukoloni, na za Urasmi mkongwe hadi zile za Ulimbwende (Uromansia) na Uhalisia. Taaluma ya Fasihi Linganishi imeundiwa Jumuiya ya kimataifa ijulikanayo kama: *"International Comparative Literature Association (ICLA)"* Kwa sasa, Jumuiya hii hufanya kazi zake kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vihusikavyo na taaluma hii kutoka kanda tofauti ulimwenguni. Kanda kuu ni:

i) Chama cha Fasihi Linganishi cha Ufaransa (FCLA)
ii) Chama cha Fasihi Linganishi cha Marekani (ACLA)
iii) Chama cha Fasihi Linganishi cha Urusi (RCLA)
iv) Chama cha Fasihi Linganishi cha Ujerumani (GCLA)
v) Chama cha Fasihi Linganishi cha Uingereza ( BCLA)

Kanda hizi hufanya kazi kwa kushirikia na baadhi ya mataifa madogo. Kwa mfano, kijamii Tanzania iko karibu zaidi na nchi za Ujerumani na Uingereza. (Ponera, 2014)

**2.4.2.2 Mihimili / Misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi**

Zepetnek (1998) amefafanua misingi kumi (10) ya Nadharia Fasihi Linganishi ifuatayo:

i) Kutambua taaluma hii kwa kuzingatia mbinu stadi sahihi katika mafunzo ya Fasihi kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa Fasihi Linganishi na tamaduni nyengine.

ii) Fasihi Linganishi ni nadharia na pia ni mbinu muhimu inayodaiwa kujikita hasa katika uhusiano baina ya Utamaduni, Lugha, Fasihi na Maarifa.

iii) Kuwa na hamu ya mwana-Fasihi Linganishi mwenye uwezo mkubwa wa kutambua Lugha na Fasihi za jamii tofauti pamoja na maarifa mengineyo kwa undani na uhusiano wa nadharia na mbinu nyenginezo stahiki.

iv) Kuwa na hamu ya kujifunza Fasihi Linganishi ikihusishwa na stadi nyengine kama (Sanaa, Filamu, Utamaduni, Maigizo na mengineyo) ambayo nayo yanahusishwa na matawi makuu ya taaluma ya Sayansi Jamii katika fani zake (Historia, Sosholojia, Saikolojia na nyenginezo)

v) Kutambua na kujifunza Lugha na Fasihi katika mazingira ya kuzingatia Nadharia ya Fasihi Linganishi na matumizi yake lakini mazingira hayo yakienda sambamba na lugha ya Kiingereza ambayo imekitwa katika taaluma nyingi za nasaba yake.

vi) Kutambua nadharia na mbinu za Fasihi Linganishi zinazolenga na uhusishwaji wa utafiti na uchambuzi wake kwa lengo la kutolea ushahidi wake juu ya ubora na udhaifu wake.

vii) Kuwa na hamu ya kuitumia vyema Fasihi Linganishi kwa kuzingatia nadharia na mbinu na kuihusisha na mwamko wa kimawazo na kiitikadi ya siasa yake.

viii) Kutambua vyema uhusiano na uhusishwaji wa kimaudhui baina ya kazi za sanaa kwa kuzingatia wakati, mfumo, wahusika, upekee na Maudhui husika katika uhalisia au udhanaishi wake kitaifa na kiulimwengu.

ix) Kuhamasika juu ya matumizi ya nadharia katika mfumo wa kiutandawazi, kiteknolojia, kiviwanda na mawasiliano katika utekelezaji wa maendeleo na kuhadharika juu ya jamii, utaifa, jinsia, na mafunzo mengineyo.

x) Kuwa na shauku kubwa ya kujifunza nadharia ya Fasihi Linganishi ili kuweza kuwa mweledi / mjuzi wa matumizi yake, katika Fasihi, Sanaa na Matumizi mengineyo stahiki.

Kwa hivyo, sababu kubwa ya kuchagua nadharia hii ya Fasihi Linganishi, ni imani ya mtafiti kuwa Nadharia ya Fasihi Linganishi imekuwa na nafasi kubwa ya kutimiza shauku ya mtafiti kujibu na kutimiza lengo mahsusi la pili na la lengo mahsusi la tatu, pamoja na kujibu swali la msingi la pili na swali la tatu la utafiti huu ambapo kwa ujumla malengo mahsusi hayo na maswali yake yamelenga kuhusu ulinganishaji na ulinganuzi wa usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena* .

## 2.5 Hitimisho

Sura hii imekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kama sura nyenginezo. Kwa muhtasari sura hii ilijikita kujadili kwa kina vipengele muhimu ambavyo vinatoa uhai wa utafiti huu. Miongoni mwa yaliyojadiliwa ni pamoja na: Ufafanuzi

wa Istilahi mbalimbali, Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu riwaya za Said Ahmed Mohamed. Vilevile, sura hii ilijadili kuhusu Mkabala wa Kinadharia. Nadharia zilizojadiliwa ni Nadharia ya Ufeministi hasa Ufeministi wa Kiafrika ili iweze kutumika kwa lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu. Vilevile Nadharia ya Fasihi Linganishi imetumika ili iweze kutimiza haja ya lengo mahsusi la pili na la tatu, sambamba na swali la msingi la pili na la tatu la utafiti huu. Sura inayofuata inahusu Mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imejikita kufafanua vipengele muhimu vifuatavyo: Maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, zana / vifaa vya utafiti na hitimisho. Kwa ujumla sura hii ina mchango mkubwa katika kufanikisha namna utafiti ulivyofanyika kuhusu mada husika ya utafiti.

## 3.2 Maana ya Mbinu za utafiti

Kothari (2004) anaeleza, mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu / taratibu zote stahiki zinazotumika wakati wa kufanya utafiti.

Enon (1998) anafafanua, mbinu za utafiti ni njia na taratibu zote zinazopaswa kufuatwa wakati wa ukusanyaji wa data (taarifa) kulingana na aina ya utafiti.

University of Abuja (1992) wameeleza, mbinu za utafiti ni utaratibu maalum wa kufuatwa au kuchunguza kitu kwa kuzingatia hali ya umakini, malengo na mantiki nzuri kwa lengo la kufanikisha kazi husika vyema.

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema, mbinu za utafiti ni jumla ya taratibu, mpango na hatua maalum atakazozifuata mtafiti wakati akiendelea na zoezi lake la kukusanya data kulingana na  mada halisi yake ya utafiti. Mbinu za utafiti lazima zizingatie

utaratibu uliorasmi ili kuweza kufuatwa na mwishowe kuijenga kazi ya utafiti katika uhalali na ithibati timilifu.

### 3.3 Eneo la utafiti

Enon (1998) anaeleza, Eneo la utafiti la kijiografia ni pahala mahsusi ambapo mtafiti amekwenda au amekutumia katika kukusanya data za utafiti wake.

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyikia au unakusudiwa kufanyikia. Katika eneo la utafiti ndipo data za utafiti hupatikana kwa mtafiti kufanya usaili, mahojiano, kushuhudia au kushiriki shughuli au tukio fulani pamoja na watafitiwa. (Babbie, 1992).

Kwa kuhitimishia, eneo la utafiti  ni mahali maalum ambapo kwa udhati mtafiti huliteua kwa ajili ya kufanya utafiti wake ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa data kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti kwa mujibu wa mada husika ya mtafiti.

#### 3.3.1 Uteuzi wa Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa mada ya mtafiti, *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena: Utafiti Linganishi,* mtafiti amekusanya data kupitia maktabani: Mtafiti ametumia maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo Kikuu cha taifa cha Zanzibar (SUZA), maktaba kuu Zanzibar, zote tawi la Pemba na maktaba ya wilaya ya Wete. Sambamba na hayo matumizi ya wavuti / tovuti na vyanzo vinginevyo vya kimtandao vimetumika kwa lengo la kupata taarifa za ziada zinazohusiana na mada ya mtafiti.

#### 3.3.1.1 Sababu za Uteuzi wa Maktaba Tajwa

Mtafiti ametumia maktaba mbalimbali tajwa mfano: Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha taifa cha Zanzibar, Maktaba kuu Zanzibar, (zote tawi la Pemba) Sababu kubwa ya mtafiti kuchagua maktaba hizo ni kuwa zote zinapatikana kisiwani Pemba ambapo mtafiti anaishi. Hivyo mtafiti ameweza kufika maeneo husika kwa lengo la kukusanya taarifa anazozihitaji. Pia taarifa anazozihitaji mtafiti amezipata katika maktaba hizo lakini katika kiwango tofauti. Kiwango hicho kimesaidia sana kufanikisha kazi ya mtafiti ipasavyo hususan ile inayomuhusu mwanamke.

#### 3.3.1.2 Sababu za  Matumizi ya Wavuti /Tovuti (Internet)

Matumizi ya wavuti / tovuti yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kuongezea maarifa mbalimbali kuhusu mada ya mtafiti. Sababu kubwa ya mtafiti kutumia wavuti / tovuti mbalimbali ni kwa lengo la kupata taarifa za ziada za vyanzo vyenginevyo kulingana na mada ya utafiti. Hivyo basi wavuti / tovuti zinamekuwa na umuhimu mkubwa kwa mtafiti katika kufanikisha mada ya utafiti wakati wa kurejelea.

Kwa muhtasari eneo la utafiti lina mchango mkubwa katika kujenga uhalali wa taarifa zitazokusanya na mtafiti wakati wa uchambuzi wa taarifa (data) na kuifanya kazi ya utafiti iwe na uhai na yenye kuaminika na kuleta tija kwa umma wote.

### 3.4 Kundi Lengwa

BAKIZA (2010) wanaeleza, uteuzi ni uchaguaji wa kitu au mtu miongoni mwa

wengi. Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari, 2004).

Enon (1998) anaeleza, uteuzi wa kundi lengwa ni ule wa mtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data atakazozihitaji ili kupata data za utafiti wake. Mtafiti ametumia uteuzi wa kundi lengwa katika mada husika.

Uteuzi lengwa ni uteuzi ambao huteuliwa na mtafiti kwa makusudi akifahamu kuwa uteuzi huo utampatia data sahihi zitakazojibu maswali yake ya utafiti. (Babbie, 1999). Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni riwaya teule za *Utengano na Kamwe si mbali tena.* Msingi wa uteuzi lengwa unatokana na sababu kuu zifuatazo:

**Mosi,** Riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe Si Mbali Tena.* Msingi mkubwa wa kuteua riwaya hizi ni kwamba mtafiti anaamini bado hazijawahi kufanyiwa utafiti kwa mujibu wa mada, ingawa riwaya ya *Utengano* imeshawahi kufanyiwa utafiti kwa kuwa ni kongwe (1980) lakini riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ni mpya (2014), haijatafitiwa.

**Pili,** Riwaya hizi zimefanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti kupitia mada husika ambayo ni: *Kutathmini Mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena.* Kwa msingi huo mtafiti anaamini kwamba vitabu teule hivyo vimefanikisha vyema kiu ya mtafiti kwa mujibu wa mada yake kwa kiwango kikubwa kinachostahiki.

### 3.5 Mbinu ya Usampulishaji

Hornby (2005) wanaeleza, Sampuli ni kundi la watu au vitu walioteuliwa kutoka kundi kubwa na ambao watatumika kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu kundi kubwa. Au Sampuli ni kundi dogo teuliwa litakalotumika kwa lengo la kutoa taarifa kuhusiana na jambo au mada fulani. Sampuli ni nyenzo muhimu katika kufikia hatua ya ukusanyaji wa taarifa zinazohitajika na mtafiti katika utafiti wake kulingana na mada. (TY)

Kwa mujibu wa Kothari (1990, 2004) Sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake. Bryman (2004), Uteuzi wa Sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima.

Kwa ujumla sampuli ni  kundi la watu au vitu ambapo mtafiti hulitumia kama kiwakilishi cha kundi kubwa wakati wa ukusanyaji wa data / taarifa anazozihitaji mtafiti kwa mujibu wa mada ya utafiti wake. Sampuli ni kipengele muhimu katika utafiti kwa sababu ni njia muhimu ya kufikia hatua ya kukusanya data. Kwa hakika ili mtafiti aweze kupata sampuli anayoihitaji kwa mujibu wa mada ni lazima kwa mtafiti huyo kufuata utafatibu maalum wa kupata sampuli. Utafatibu wa kupata hiyo sampuli huitwa mbinu za usampulishaji. Hivyo basi katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya Usampulishaji lengwa.

Babbie (1999) anaeleza kuwa, Usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza malengo ya utafiti kwa wepesi na haraka. Kwa upande wake, Yin (1994) anaeleza, usampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti anateua watafitiwa ama vitafitiwa akiwa amejiridhisha kwamba watafitiwa hao watampatia data itakayoweza kutimiza malengo ya utafiti wake.

Mbinu hii ya Usampulishaji lengwa imetumika katika kuteua riwaya ya *Utengano (1980)* na *Kamwe si mbali tena (2014)* ya mwandishi Said Ahmed Muhamed kuwa ndio msingi mkuu wa watafitiwa wake ambapo mtafiti amejiridhisha kwamba itamsaidia sana kupata data za uhakika za utafiti huu tunaoukusudia na kufanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti ipasavyo.

Mbinu ya Usampulishaji lengwa ina manufaa makubwa kwa mtafiti kwasababu humwezesha mtafiti kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi. Vilevile mbinu hii humfanya mtafiti kutokutumia muda mwingi kwenda kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiki hivyo basi mtafiti atafanya utafiti wake kwa watafitiwa watokanao na sampuli lengwa tu kulingana na malengo na maswali ya utafiti (Adam na Kamuzora, 2008).

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Enon (1998) anaeleza, Ukusanyaji wa data, ni zoezi la awali katika utafiti, zoezi ambalo, humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika

lengo lake la utafiti. Kothari (2004) anafafanua, Ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti. Aidha, hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua ya ukusanyaji wa data. Kiudhati, katika utafiti wowote hususan wa kitaaluma ukusanyaji wa data huwa unajitokeza katika aina kuu mbili: Data za Awali (Msingi) na Data za Upili (Fuatizi)

### 3.6.1 Data za Awali (Msingi)

Adam na Kamuzora (2008) wanaeleza, Data za Awali ni aina ya data zilizokusanywa na mtafiti mwenyewe au msaidizi wa mtafiti kutoka katika eneo halisi kwa lengo la kujibu maswali au mada ya utafiti. Kothari (2004) anaeleza, Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi. Data hizi za msingi hazijapata kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao ulikusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza.

Kwa kuhitimishia tunaweza kusema, Data za awali ni aina ya data halisi na thabiti ambazo mtafiti huzikusanya kwa mara ya kwanza kutoka katika eneo halisi alilolichagua kwa mujibu wa mada yake ya utafiti. Data za msingi katika utafiti huu zilizokusanywa ni kutoka katika riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

### 3.6.2 Data za Upili (Fuatizi)

Kothari (2004) anafafanua, Data za Upili ni data zote ambazo tayari zimekwishakusanywa na mwenginewe (mtafiti) na ambazo zimepitia katika hatua zote stahiki za ukusanyaji data. Kamuzora na Adam (2008) wanasema, Data za Upili

ni data zote zinazopatikana kutoka vyanzo tangulizi au data zilizokusanywa na watu wengineo kwa malengo maalum.

Katika utafiti huu, mtafiti pia ametumia data za upili kwa lengo maalumu la kukazia, kushadidia, kutilia mkazo taarifa ambazo amezipata kutoka katika data za awali (msingi). Katika kufanikisha dhamira hiyo, mtafiti amesoma kwa umakini kazi tangulizi zikiwemo, tasnifu, vitabu, makala, majarida, magazeti, ripoti na wavuti mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinahusiana na mada ya mtafiti.

### 3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji data ni njia anazochagua mtafiti kuzitumia kukusanya data kwa ajili ya utafiti wake (Kothari, 1990). Kwa udhati kabisa utafiti wowote hauwezi kufanyika bila ya kuwepo mbinu maalum zitakazotumika kukusanya data. Mbinu za utafiti huu ni Mbinu ya usomaji makini kupitia maktaba.

#### 3.7.1 Mbinu ya Usomaji makini kupitia maktabani

Mbinu hii imelenga kutoa fursa ya kupitia na kusoma kwa kina kazi mbalimbali maktaba ambazo zinahusiana na mada ya mtafiti. Katika mbinu hii mtafiti ametumia mbinu ya usomaji makini wa vitabu husika na kazi nyenginezo zinazoendana na mada ya mtafiti akiwa na imani kubwa ya kupata taarifa zenye uhakika katika utafiti huo.

Kothari (2004) anaeleza, Usomaji makini ni mbinu inayolenga kusoma na kuchambua kwa undani (kwa kina) maudhui yanayojitokeza katika kazi husika kama vile vitabu, majarida, magazeti yanayoendana na mada husika. Enon (1998) kwa

upande wake anasema, Mbinu ya usomaji makini ni mbinu inayomtaka mtafiti kukusanya taarifa kwa umakini baada ya kusoma kwa kina kazi husika kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Katika utafiti huu, mtafiti kwa kupitia njia ya maktabani ametumia mbinu ya usomaji makini kupitia kwa undani (kwa kina) na hatua kwa hatua kuanzia mwanzo hadi mwisho riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* na kunukuu sentesi na aya mbalimbali zinazohusiana na dhana nzima ya mwanamke na usawiri wake kwenye daftari (shajara) maalum alilioliandaa na kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti. Kazi hiyo imefanyika kwa lengo la kuchambua data ambazo amezikusanya vyema.

### 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Babbie (1999) kwa upande wake anasema kuwa, Data zinazokusanywa wakati wa utafiti hazina budi kufanyiwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti na malengo ya utafiti yaliyokusudiwa. Kwa hiyo, Uchambuzi wa data ni kitendo kilichorasmi ambacho mtafiti hukitumia mara baada ya kukusanya data za utafiti kutoka katika vyanzo husika kwa lengo la kuzichambua ili kupima uhalali wa taarifa zilizopatikana kwa mujibu wa mada ya utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi wa data ili kufanikisha malengo ya utafiti na kupata matokeo sahihi.

#### 3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa Kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya

utafiti wake (Kothari, 1990). Mtafiti amechagua mbinu hii katika uchambuzi wa data akiamini imekuwa muwafaka hususan katika uchambuzi wa kazi za Fasihi kwa ujumla. Dhana hii haina maana kuwa mbinu ya Kitakwimu haifai katika uchambuzi la hasha, mtafiti ametambua ubora wa mbinu zote (mbinu ya Kitakwimu na mbinu ya Kimaelezo) ila mtafiti ameona ya kuwa mbinu hii imetoa fursa kubwa na imekuwa ni nyepesi kwa mtafiti kuweza kuchambua data kwa uwazi na kwa urahisi zaidi ingawaje mbinu ya Kimahesabu (Kitakwimu) imetumika kwa kiwango kidogo kama ni njia ya kufupisha maelezo na kurahisisha ufahamu.

Vilevile katika uchambuzi wa data, mtafiti amezingatia matumizi ya nadharia husika katika kuhusisha na mada ya utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Nadharia ambazo zimetumika katika uchambuzi wa utafiti huu ni Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika pamoja na Nadharia ya Fasihi Linganishi. Uchambuzi wa data huo wa kimaelezo umezingatia kujibu swali la kwanza na lengo la kwanza la utafiti kwa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Kwa upande mwengine swali la pili na la tatu, sambamba na lengo la pili na la tatu limechambuliwa data zake zikihusishwa na nadharia ya Fasihi Linganishi. Kwa ujumla uchambuzi wote wa data za utafiti umeenda sambamba na mada ya utafiti isemayo: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

### 3.9 Zana / Vifaa vya Utafiti

Mulokozi (1983) anaeleza: Vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivyo huwa ni pamoja na: Kalamu na Karatasi, Shajara, Tepu rekoda (kirimbo) na vifaa vyake, Video (pataninga); na vifaa vyake, Kamera na vifaa vyake,

Ngamizi na vikorokoro vyake, Hojaji, Vifaa vya kupimia na kuhesabia. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia vifaa vifuatavyo:

### 3.9.1 Kalamu na Notibuku / Shajara

Vifaa hivi vimetumika kwa ajili ya kuandikia taarifa mbalimbali kwa lengo la kuweka kumbukumbu za taarifa ambazo zimekusanywa katika mfumo wa maandishi zinazohusiana na mada, malengo na maswali ya utafiti huu.

### 3.9.2 Vitabu, Tasnifu, Makala na Majarida

Vifaa vyote hivi vina umuhimu mkubwa katika utafiti huu.Vifaa hivi vimetumika kama ni sehemu muhimu ya kurejelea wakati mapitio ya kazi tangulizi pamoja na ufafanuzi wa mambo muhimu katika uchambuzi wa data za utafiti ili kuufanya utafiti huu utosheleze mahitajio ya malengo na maswali ya utafiti.

### 3.9.3 Kompyuta na Wavuti / Tovuti

Kompyuta imetumika kwa kiwango kikubwa kuchapa kazi hii ya utafiti kuanzia mwanzo hadi mwisho. Wavuti / Tovuti zimetumika kwa lengo la kutafutia machapisho, maarifa, tasnifu na taarifa nyenginezo muhimu zenye kuhusiana na mada ya utafiti.

## 3.10 Hitimisho

Bilashaka sura hii ni kama sura zilizopita imekuwa na umuhimu mkubwa kwa kuwa imejikita katika mambo muhimu na ya msingi katika utafiti huu. Mambo yaliyojadiliwa katika sura hii yametoa dira au ni kama tochi inayong’ara katika

utekelezaji wa utafiti huu. Vipengele vilivyozingatiwa vinavyohusu Mbinu ya utafiti ni pamoja na: Dhana ya mbinu ya utafiti, Eneo la utafiti, Mbinu ya usampulishaji, Ukusanyaji wa data, Mbinu za Ukusanyaji wa data, Mbinu za uchambuzi wa data na Zana / vifaa vya utafiti. Kwa ujumla kila kipengele kina umuhimu wake katika kukamilisha kazi nzima ya utafiti huu kwa kiwango bora. Sura inayofuata imehusu Uwasilishaji na Uchambuzi wa data za uafiti

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Kwa ujumla Sura hii imezingatia msingi muhimu wa utafiti huu. Vipengele vya msingi vifuatavyo vimejadiliwa kwa kina: Historia / usuli wa mtunzi / mwandishi wa riwaya teule, Muhtasari wa riwaya hizo teule, *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* zikihusishwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Pia Ulinganishaji na Ulinganuzi wa usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ikiwa ni pamoja na Nadharia ya Fasihi Linganishi, Mbinu za usawiri wa mwanamke katika riwaya teule na mwisho ni Hitimisho.

## 4.2 Usuli wa mwandishi: Said Ahmed Mohamed

Profesa Said Ahmed Mohamed alizaliwa Unguja mnamo tarehe 12 /12/ 1947. Alisoma shule ya Msingi Darajani na Sekondari Gulioni, na kuendelea na masomo Chuo Cha Ualimu Nkurumah - Zanzibar mwaka 1966. Mwaka 1976, Prof. Said alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kusomea Shahada ya Kwanza ya Ualimu katika Isimu na Fasihi ya Kiswahili na baada ya miaka mitatu alisomea Shahada ya Uzamili katika Isimu Tekelezi chuoni hapo. Kutokana na umahiri/ uwezo wake mkubwa alipata fursa ya kuelekea Ujerumani kufanya Shahada ya tatu ya Uzamivu (PhD) katika Chuo Kikuu cha Karl Marx – Leipzig mwisho wa mwaka 1981 na kukamilisha mwaka 1985.

Prof. Said amewahi kufundisha Shule ya Sekondari Kizimbani na Utaani baina ya mwaka 1969 na 1974. Shule ya Hamamni kwa miaka mitatu. TAKILUKI kwa miaka

miwili. Mwaka 1987 alikwenda Kenya na kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi mjini Eldoreti na baadae alifundisha Chuo Kikuu cha Nairobi – ndaki ya Kikuyu hadi mwaka 1990. Alipotoka Nairobi alielekea Japan katika Chuo Kikuu cha Osaka – Idara ya Lugha za Kigeni na ndipo alipopata Uprofesa. Alipotoka Japan alikuja Chuo Kikuu cha Bayreuth tangu 1997 hadi kustaafu 2012. Kwa sasa Profesa Said baada ya kustaafu amerudi nyumbani kwake Limbani Wete Pemba kwa mapumziko na kuendeleza kazi yake ya uandishi.

Vile vile akiwa Zanzibar anaendelea kufundisha katika Chuo Kikuu Cha Zanzibar (SUZA) wanafunzi wa somo la Kiswahili hususan Shahada ya Uzamili (Masters) na Shahada ya Uzamivu (PhD) akitumainia mafanikio makubwa kwa chuo na taifa. Kwa upande wa familiya, Profesa ana mke wake mpenzi anayeitwa Rahma na watoto wawili: Mwanamke anaitwa Najma na mwanamme anaitwa Mahir na wote wameshamaliza Shahada ya kwanza.

Katika sanaa ya Uandishi na Ubunifu wa Fasihi, Profesa Said amekuwa mwandishi mashuhuri na gwiji kwasababu ameweza kuandika kwa ustadi mkubwa fani zote: Riwaya, Tamthiliya, Ushairi, Haditi fupi, Kazi za watoto na vitabu vya shule na vyuo. Profesa ameandika vitabu zaidi (50). Riwaya zake ni pamoja na: *Asali Chungu (1977), Utengano (1980), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990), Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Nyuso za Mwanamke (2010), Mhanga nafsi yangu (2012) Mkamandume (2013) na Kamwe si mbali tena (2014).*

### 4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Utengano (1980)

*Utengano* ni miongoni mwa riwaya kongwe iliyotungwa na kuandikwa na Prof. Said Ahmed Mohamed mwaka (1980). Riwaya hii kwa ujumla imechambua mambo kadhaa ya msingi katika nyanja mbalimbali za kimaisha kama vile Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii, mambo ambayo hujitokeza katika maisha yetu ya kilasiku na kwa jamii nyenginezo mbalimbali. Riwaya hii imejikita katika kueleza madhila anayoyapitia mwanamke kwa mfano ukandamizaji, udhalilishaji, uonevu na ukatili anaofanyiwa na mwanamme. Mbali na hayo riwaya imejadili harakati za wanawake katika ukombozi wao Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni ili kufikia hatua ya maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla. Muhusika mkuu katika riwaya hii ni Maimuna. Maimuna ni msichana anayetoka katika familiya ya kitajiri ya Bwana Maksuudi na mama yake Bi Tamima. Baba yake Bwana Maksuudi ni mzee asiyetaka mas-hara - yaani ni mzee mkali mno hususan katika mambo yanayoihusu familiya yake akiwemo mwanawe Maimuna na mkewe Bi Tamima. Maksuudi katika usimamizi wa familiya yake hakumruhusu hata kidogo mwanawe na mkewe kutoka nje ya nyumba au kasri yake bila ya ruhusa kutoka kwake, hali hii ilipelekea familiya kuishi pasi na uhuru ingawa maisha yao yalikuwa mazuri. Familiya iliwekwa utawani.

Kwa upande mwengine Bwana Maksuudi alikuwa ni kiongozi wa kisiasa ambaye katika uchaguzi uliofuata alishindwa vibaya mno na mpinzani wake Bwana Siwa. Miongoni mwa sababu za kushindwa kwake ni tabia yake mbaya katika jamii kama vile rushwa, uasharati, na ukosefu wa uwajibikaji mwema katika jamii. Kwa mfano bwana Maksuudi amepokea rushwa kwa kuuza saini yake kwa ajili ya kiwanja

kutoka kwa mke wa bwana Japu kwa shilingi 200. Pia Makusuudi ni mpenda uasharati na alikuwa na mpenzi wake wa nje ya ndoa aliyeitwa Kazija. Kwa upande wa Maimuna, kwa kuwa aliwekwa utawani, kwa bahati mbaya amepata bahati ya kutoroka maratu baada ya mama yake kujifungua. Baada ya hapo ameingia mitaani na kuwa ni mwenye kujiuza (uasharati) kushiriki ulevi, kupoteza muelekeo, kukosa msaada sahihi na kusababisha kutengana na familiya yake ingawaje mwishowe anaolewa na Kabi na kuishi vyema. Mwisho kabisa Bwana Maksuudi anajuta sana kwa dhambi alizozitenda ikiwa ni pamoja na kusababisha kusambaratisha familiya yake na kuifanya ikose mwelekeo na yeye kufariki ingawa aliomba msamaha kwa familiya na wote aliowakosea na kuamua kubadilika na kuwa mtu mwema. Bi Tamima, Bi Farashuu, Mussa, Maimuna walikubali kusameheana vyema.

Jina la kitabu, *Utengano* linasadifu na yaliyomo (Maudhui) kwasababu kuna Utengano baina ya Maksuudi na wake zake Mwanasururu na Bi Tamima. Utengano baina ya Maksuudi na wanawe Mussa na Maimuna. Utengano baina ya Maksuudi na hawara wake Kazija. Utengano baina ya Mussa na Maimuna na Utengano baina ya mama Jeni na Maimuna. Ingawaje baadhi yao mwishowe walisameheana na kuridhiana, mfano Bwana Maksuudi na familiya yake.

### 4.4 Muhtasari wa Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena

*Kamwe si mbali tena* ni katika riwaya mpya ya mwandishi nguli Profesa Saidi Ahmed Mohamed iliyotungwa mwaka (2014). Kwa muhtasari riwaya imejadili kwa kina masuala nyeti ambayo yameakisi maisha halisi ya jamii zetu katika hali zote za Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii. Riwaya hii imejadili maisha ya muhusika mkuu Bi

Chani ambaye mumewe Bwana Mansouri aliuwawa na watawala katika harakati za mabadiliko na mporomoko.

Bi Chani na Bwana Mansouri walijaaliwa watoto nane na mmoja wa kulea anayeitwa Mwavile. Watoto hao ni: Abuu, Salila, Yasir, Jokha, Sele (Msulupwete kwa jina la utani), Zaharan, Samira na Tambo. Watoto wote hawa walilelewa kwa mapenzi makubwa na mema na wazazi wao. Awali waliishi katika maisha mazuri pamoja na kushirikiana katika hali zote lakini baadae waliamua kuhama nchi yao iliyoitwa Visiwa vya Viungo pale hali ya maisha na familiya yao ilipokuwa mbaya na kuamua kuhama kwao kwenda kutafuta maisha mazuri Ulaya (nchi zilizoendelea) kwa imani tu kuwa huko wataweza kufanikiwa vizuri zaidi kimaisha na kumuachia ulezi Mwavile kumlea mama yao. Bi Chani ambaye alikuwa tayari ni bibi mtu mzima zaidi (kizee) asiyeweza kujimudu na anayehitaji kusaidiwa kwa asilimia zote. Mbali na hilo Bi Chani ambaye huweza kuzungumza wakati fulani na baadae kushindwa alikuwa ni bibi mwenye msimamo madhubuti na mtetezi wa kweli wa haki zake na umma kwa ujumla. Ugonjwa wa Bi Chani mbali ya utuuzima lakini alikuwa anasumbuliwa na tatizo la kupoteza fahamu (kumbukumbu) au “Memory gaps - Alzheimer”. Ni bibi ambaye aliyekuwa anajua vyema maisha ya jamii yake Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii

Watoto wa Bi Chani na Bwana Mansour walifanikiwa kwenda Ulaya lakini kwa bahati ni wachache ambao walifanikiwa kimaisha hususan katika Elimu. Mfano Tambo alikuwa mwanasheria aliyesoma Chuo Kikuu na kuwa miongoni mwa watetezi wa umma. Samira ambaye alikuwa ni Profesa wa somo la “Media na

Information Technology" kutoka Chuo Kikuu kimoja cha Sydney – Australia. Mtoto mwengine ni Zahran ambaye alisoma Uarabuni nchini Abudhabi baadae Iraqi masomo ya Biashara na Uhasibu hadi kumaliza digrii yake na kurudi Abudhabi kufanya kazi katika benki na mwishowe kuwa miongoni mwa viongozi wakuu wa juu wa benki hiyo. Aliporudi kwao alifanya kazi za biashara ya vifaa vya ujenzi na pia alijiunga katika harakati za Vuguvugu la Msimamo. Lakini watoto wengine walirudi kwao maisha yao yakiwa dhaifu na tegemezi. Miongoni mwa hao ni pamoja na Abuu, Yasir na Jokha.

Kwa ujumla dhana ya *"Kamwe si mbali tena"* ambalo ndio jina la riwaya hii ni yenye mawanda mapana ikiwemo kuakisi na kudhihirisha harakati lukuki kwa jamii ya Visiwa vya Viungo na hata jamii nyenginezo dhidi ya utawala wa kidhalimu kama ule ulioshiriki kumuua bwana Mansour na nia ya kumdhulumu Bi Chani na familiya yake kwa shamba lake ambalo mwishowe alisimama imara kulikomboa. Dhana hii pia imelenga katika kutumainia mabadiliko na mafanikio katika jamii Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii jambo ambalo imeonekana mabadiliko hayo kamwe si mbali tena isipokuwa msingi mkubwa ni kushikamana na kuwa pamoja kama walivyokua pamoja Bi Chani na wanawe au kama vile walivyokuwa pamoja Zahran, Tambo na Samira katika Vuguvugu la Msimamo.

### 4.5 Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano

Riwaya ya *Utengano* imesheheni wahusika lukuki, wanawake na wanaume ambao wameshirikishwa vyema na mwandishi katika kufikisha Maudhui aliyoyakusudia kwa jamii. Miongoni mwa wahusika hao kwa upande wa wanaume ni pamoja na:

Bw. Maksuudi, Mussa, Ispekta Fadhili, Bw. Zanga, Bw. Siwa, Bw. Shoka, Rashidi, Kabi na wengineo. Kwa upande wa wahusika wanawake ni: Bi Tamima, Bi Farashuu, Biti Kocho, Maimuna, Kazija, Biti Sururu, Bi Mtumwa, Bi Sada, Mama Jeni, Dora, Sihaba, Kijakazi, Mwanasururu, Mwanamkuu na wengineo.

Mtafiti kwa mujibu wa mada husika hajajishughulisha na uchambuzi wa wahusika wanaume na badala yake amejikita katika kujadili na kuchambua data alizozikusanya kuhusu wahusika wanawake ingawa baadhi ya matendo wahusika wanaume wameshirikishwa. Mtafiti amebaini kuwa usawiri wa mwanamke umejitokeza katika hali / namna mbalimbali zilizo chanya (njema) na hasi (mbaya). Mtafiti akihusisha na nadharia ya Ufeministi amechambua usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* kama alivyoongozwa na swali la msingi la kwanza lifuatalo:

i) Ni kwa vipi usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule ya *Utengano na Kamwe si mbali tena?*

Kwa hakika swali hilo la msingi la kwanza limeenda sambamba na lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lisemalo: Kufafanua usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*. Katika kulijibu swali hilo la msingi, mtafiti amefafanua usawiri mwanamke kama ulivyojitokeza katika riwaya teule mbili kwa kuanzia na riwaya ya *Utengano* kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Mwanamke Kama Mhusika Mshauri Mwema

Suala la kutoa ushauri mwema lina umuhimu mkubwa katika kujenga familia na jamii kwa ujumla. Ushauri ambao utawezesha kurutubisha familia una nafasi kubwa

ya kuthaminiwa na jamii yeyote kwa ukamilifu wake. Katika riwaya hii mtafiti amebaini mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushauri juu ya maendeleo na afya ya familia. Utafiti huu umebaini jinsi Maimuna anavyomshauri mama yake Bi Tamima kuvunja miko ya utawa ya nyumba ya Bwana Maksuudi (mumewe na baba wa Maimuna na Mussa) ili apelekwe hospitali au aitiwe daktari ambaye atamsaidia kujifungua. Mwandishi analisemea hilo kama ifuatavyo:

> "Mama usifanye mchezo vyo. Ikiwa kuogopa kuvunja miko ya nyumba hii, tusiogope. Naivunjwe leo hiyo miko. Hujui utazaa vipi, mama. Tutangojea idhini ya mtu asiyekuwepo, wala tusiyemtarajia kurudi saa hizi? Hatorudi hapa mpaka wiki ishe. Basi yeye baba hatofahamu kuwa ilibidi tukuchukue hospitali au tumwite mkunga hapa?" (Uk. 20)

Vilevile, suala la ushauri mwema limejitokeza tena kupitia kwa muhusika Dora. Mara tu Maimuna alipoamua kuhama Pumziko baada ya kusingiziwa kuwa mwizi na Mama Jeni, Maimuna alikosa mwelekeo na hakujua wapi aelekee ndipo Dora alipomshauri na kumuomba kwenda Bobea kwa Biti Sururu. Ombi na ushauri huo Maimuna aliukubali na Dora alimpa msaada wa shilingi mia mbili akiamini zitamsaidia. Mwandishi anasema:

> "Basi aliruka Dora, nina ombi la mwisho kwako kabla hujenda zako. Ikiwa huna pahala maalumu pa kwenda , naomba wende Bobea kwa Biti Sururu. Yule bibi tuliyekuwa tukimkuta kuta njiani na madukani. Siku zote ananikera nikaishi naye. Ni bibi mtu mzima, lakini ana imani. Sasa badala ya kwenda mimi, nakupeleka wewe kwanza, na mimi nitafuatia. Mimi nina deni langu kwa Mama Jeni, nangoja nilimalize kwanza. 'Dora alitoa barua ndani ya mkoba wa ngozi,'Hii barua, mpe, na anwani yake hiyo hapo juu ya bahasha. Na hizi shilingi mia mbili zitakufaa" (Uk. 85)

Mtafiti kupitia nukuu hizi zimetoa sura kamili ya mwanamke anavyohitajika kuwa katika maendeleo yake na familia au jamii kwa ujumla. Mfano huu wa Maimuna

kumshauri mama yake kuhusu afya yake ni mzuri na unastahiki kuungwa mkono hususan ukizingatia mama wenyewe alikuwa mjamzito. Hili lilifanyika kwa lengo la kuokoa maisha ya mama (Bi Tamima) na mwanawe. Sambamba na hilo kitendo cha Dora kumshauri na kumuomba Maimuna ilikuwa ni sehemu ya kumsaidia kuendeleza vyema maisha yake Maimuna.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, imetilia mkazo zaidi katika kumpa nafasi mwanamke kwa kuzingatia uwezo wake ikiwa ni pamoja na uwezo mkubwa wa kushauri juu ya mambo na mipango ambayo inaweza kuleta mafanikio katika jamii zetu za Kiafrika ikiwemo jamii ya Tanzania. Mtafiti ameona kuwa suala la utoaji wa ushauri mwema lina nafasi yake na ni vyema likaendelezwa na wanawake kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

### 4.5.2 Mwanamke Kama Muhusika Muwajibikaji (Bidii Katika Kazi)

Uwajibikaji au Bidii katika kazi ni jambo muhimu katika kujenga jamii imara na yenye kuhitaji mafanikio. Wanajamii wanapowajibika kupitia kazi mbalimbali husaidia sana kuchangia maendeleo ya taifa. Kupitia utafiti huu, Mtafiti amebaini juhudi za Bi Farashuu za kuwajibika katika biashara ndogondogo mfano kutunga vikuba na asumini, kusukuma mikate hadi usiku au vitumbua na ukunga zilizochangia kuimarisha maisha yake. Mwandishi anafafanua:

> “Jiha ya Farashuu ni salama na upole. Shwari kabisa….. Hakika maisha yake yalikuwa ya wastara hasumbuki, wa mbili havai moja. Aliweza kufanya kazi yoyote mradi iwe haina ujeuri na madamu ataimudu. Naye hakupata kazi ya mtaji hata hivyo zaidi ya biashara ya mikate ya kumimina au vitumbua. Na pengine alitunga vikuba na asumini au unapotokea ukunga huitwa kuutekeleza. Lalamiko lake kubwa ni juu ya kazi. Imani yake ni kwamba, mwanamke angaliweza

> kufanya lolote alifanyalo mwanamme, pindi akipewa fursa…" (Uk. 31)

Mtafiti kwa ujumla amebaini kuwa bado mwanamke ana nafasi kubwa katika kujiletea maendeleo yake binafsi, familia na taifa kwa ujumla. Juhudi za mwanamke zina mchango mkubwa katika mabadiliko ya taifa lolote duniani. Mwanamke ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo.

Vilevile mtafiti anaamini kuwa mashirikiano mazuri baina ya mwanamke na mwanamme ni jambo muhimu katika kumuhamasisha mwanamke na mwanamme huyo kufanya kazi kwa bidii hata kama kazi hiyo ni ya kiwango cha chini kama ambayo aliyokuwa akiifanya Bi Farashuu. Hivyo basi mtafiti anasisitiza zaidi jamii iendelee kumuunga mkono mwanamke na kuthamini juhudi zake zitakazosaidia kuleta maendeleo katika jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mwanamke ana mchango mkubwa katika maendeleo ya mataifa ya Kiafrika na duniani kwa ujumla. Mtafiti amebaini kuwa Uwajibikaji wa mwanamke umempa nafasi ya kuonekana na kutambulika kuwa anaweza kushika nafasi kubwa serekalini na katika taasisi za kimataifa. Mfano nchini Liberia uwajibikaji wa mwanamke umemsaidia kuwa kiongozi mkuu wa serekali (Raisi) na kuweza kuongoza vyema. Aliyekuwa Rais wa Liberia Mheshimiwa Ellen Johnson Sirleaf aliwajibika vyema ndani ya Serekali yake.

Kwa Tanzania tunao viongozi wengi wanawake ambao wameweza kushika nafasi kubwa duniani. Mfano Dr Asha Rose Migiro aliwahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa

Umoja wa Mataifa (UN). Pia amewahi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Pia amewahi kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT). Halkadhalika Mheshimiwa Anna Makinda amewahi kuwa Spika wa Bunge la Tanzania na kwa sasa Makamo wa Raisi wa Tanzania ni mwanamke; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Hivyo basi mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushika nafasi mbalimbali ndani ya nchi na nje ya nchi husika (kimataifa). Hii ni kwa sababu ya uwajibikaji wake mzuri au bidii katika kazi.

### 4.5.3 Mwanamke Kama Muhusika Jasiri Na Mwenye Kujitolea Mhanga

Ujasiri na kujitolea muhanga, kufa au kupona sio jambo jepesi katika maisha yeyote duniani. Mtafiti amebaini kuwa mwanamke ana nafasi kubwa ya kuwa jasiri na mwenye kujitolea mhanga ili kuokoa maisha yake au maisha ya wengine katika misingi ya halali. Jambo hili ni mfano mwema wa kuigwa katika maisha yetu ya kila siku. Utafiti huu umebaini kuwa juhudi za Biti Kocho kuwa jasiri na kujitolea mhanga kuokoa maisha ya Bi Tamima zilikuwa za msingi wakati Bi Tamima alipokuwa anaadhibiwa na Bwana Maksuudi kwa sababu ya kujifungua kwake na kutoroka kwa Maimuna. Mwandishi anaeleza:

> "Biti Kocho aliyeona Tamima atakufa alisogea, 'Bwana Maksuudi, msalie mtume. Tokea hapo Tamima ameshapoteza damu nyingi kwenye uzazi na pigo namna hii utaua. Yeye hakuita mkunga, wala hakwenda hospitali kuzaa. Amini Mungu, nimemzalisha miye…Lakini Biti Kocho alisimama tanda kabisa. Alijua, ili aweze kuokoa nafsi yake na kumwokoa Tamima, alihitaji kuwa jasiri. Lazima asimame kidete na kumkabili mwanamme huyu kidume. Maksuudi alipoona badiliko hili alinywea….." (Uk.49)

> "…..Biti Kocho hakujua vipi, alitimka, akaenda kusimama mbele ya Tamima. Akamficha mgongoni pake ili kumkinga – jicho linamwenda duru, kipaji kimepiga peto, malaika yamemsimama, midomo

> inamtetemeka. Alikuwa simba jike. ‘Sasa kama unataka kumpiga Tamima, tupige sote.’ Hilo lilitosha kumfahamisha Maksuudi, Biti Kocho alikuwa mtu wa namna gani. Ule upole wake wa zamani, ile ridhaa yake kwa tajiri wake kwa sababu ya utumishi, yote yalikuwa siri kubwa iliyoficha umbo la ndani la bibi huyu. Na Maksuudi alipoangalia tambo, kimo na uzima wa bibi huyu alihakikisha tena kuwa Biti Kocho ingawa ni mwanamke hakuwa tani yake…..” (Uk. 52)

Mbali na Biti Kocho, muhusika mwengine aliyedhihirisha ujasiri na kujitolea mhanga kwa lolote ni Kazija. Kazija alisimama imara na kueleza tabia mbaya za Bwana Maksuudi na Bw. Zanga katika mkutano wa kampeni za Ubunge pasi na kujali lolote linaloweza kumtokea. Mfano Kazija anamzungumzia Bwana Maksuudi. Mwandishi anafafanua:

> “Na Maksuudi … huyu aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya, akataka kuifisidi nchi hii kwa kuwadhulumu wananchi, na ambaye baada ya kugundulikana na kusamehewa amekuwa ahasi… Huyu Maksuudi ambaye ameshindwa kuiendesha nyumba yake ataweza kuangalia maslahi yetu? Leo, mwanawe mwanamme hawajaonana mwaka. Mtoto wake mwanamke hamjui alipo, ametoroka, amestahabu kupigwa na ulimwengu. Maksuudi aliyemwacha mkewe kwa kisa cha kumtorosha mwanawe ati. Na huyu huyu Maksuudi aliyekuwa akimwendea kinyume mkewe. Mbali na mali aliyojilimbikia, nyengine ya unyan’ganyi kwa wake zake. Amemnyang’anya mkewe mmoja, Mwanasururu, mali yake na mwisho akamwacha na kusababisha kifo chake, Mengi, mengi……” (Uk. 81)

Hapana shaka yeyote utafiti huu kupitia dondoo hizi umebainisha juhudi, ujasiri wa Biti Kocho kukubali kumuokoa Bi Tamima kutoka katika kipigo cha Bwana Maksuudi jambo ambalo lingeweza kusababisha kifo cha Bi Tamima na hata Biti Kocho mwenyewe.

Pia ujasiri wa Kazija nao umedhihirisha uwezo mkubwa walionao baadhi ya wanawake katika kutetea na kupiga vita maovu katika jamii zetu. Kwa ujumla

wanawake wana wajibu wa kufuata tabia hizi na mfano wa hizi katika maisha yao ya kila siku kwa lengo la kutetea yaliyo ya halali na kupinga batili kwa maendeleo ya taifa.

Kwa kutumia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, imetoa mwamko mkubwa kupitia wanawake na kuonesha mwanamke si mtu lelemama na anaweza kujitolea mhanga katika kutetea na kupinga matendo au matukio yasiyofaa katika jamii zetu. Mtafiti amegundua kuwa hadi leo tunawaona wanawake wengi wa Kiafrika wakijitolea mhanga katika kupinga masuala nyeti ya kijamii kupitia Taasisi zao mbalimbali. Miongoni mwa Taasisi zinazojitolea kupinga matendo maovu kama udhalilishaji kijinsia, utabaka, ukatili na dhana nzima ya rushwa ambazo wasimamizi wakubwa wa taasisi hizo ni wanawake. Kwa mfano Tanzania, Taasisi zinazosimamia utetezi wa kijinsia na maendeleo ya wanawake na watoto ni pamoja na: UMATI (1959) TAMWA (1987), TAWLA (1989), TGNP (1993), WODSTA (1990), WAMA (2006) nk.

### 4.5.4 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Msimamo Thabiti

Msimamo ni hali ya kushikilia, kusimamia, kutetea, kuunga mkono juu ya jambo, tendo au matendo fulani kulingana na sababu husika. Binaadamu anaweza kuwa na msimamo juu ya kitu au jambo fulani kutokana na sababu mbalimbali – yaani sababu zinazotokana na yeye binafsi, familia, jamii au kundi fulani la watu ziwe za ukweli au hata za uongo. Katika maisha ya kila siku mtu anaweza akawa na msimamo wa kutenda au kutotenda jambo kwa kuwa amesingiziwa / kuzuliwa au ameshuhudiwa

na watu wengineo. Matokeo ya msimamo wakati mwengine huweza kuzaa matunda au kuleta athari kwa wahusika

Data zilizokusanywa na mtafiti zimedhihirisha tabia ya baadhi ya wahusika hususan wanawake kuweka msimamo madhubuti baada ya kutuhumiwa au kusingiziwa jambo baya ambalo hawajalitenda na kusababisha kuhama mazingira yao waliyokuwepo ili kuepuka bugdha au idhilali kutoka kwa wanaowasingizia. Kwa kurejelea riwaya ya *Utengano,* mwandishi ameisawiri hali hiyo kupitia muhusika Maimuna, baada ya kusingiziwa kuwa ameiba na kuitwa mwizi aliamua kuweka msimamo wa kuhama Pumziko na kuelekea Bobea kwa Biti Sururu. Mwandishi ameweka wazi hilo:

> "Sirudi Dora, nakwambia sirudi, kwa sababu nimechoka na shengesha za nyumba ile. Huo wivu na uwe ndivyo, lakini kuitwa mwizi, ila hilo! Alijibu Maimuna kwa hasira.' Wewe ndiye unayenijua zaidi, na kama si wewe, ningalikwisha tokomea zamani. Sirudi bibi, na hasa sasa nimeshakuwa debe bovu, sina la kukalia. Sirudi bibi, bora niende. Nisamehe Dora au bora tusameheane." (Uk. 83 - 84)

Katika utafiti huu mtafiti amebaini tabia ya baadhi ya wanaadamu ya kuwazuliwa wenzao matendo maovu kwa sababu tu ya chuki na choyo, bado imezoeleka katika jamii zetu na wakati mwengine husababisha, chuki, ugomvi, visasi na hata mauaji. Hivyo mtafiti anashauri jamii ni vyema tabia hiyo ikaachwa ili kujenga jamii yenye umoja, ushirikiano na mapenzi ya dhati.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetusaidia sana kudhihirisha uhalisia au tabia za wanawake katika maisha yetu ya kila siku na kupitia jamii zetu hususan za

Kiafrika. Wanawake walio wengi wameamua kubadilika na kujijenga kuwa ni wanawake wenye misimamo imara katika mambo ambayo wanaamini yatawaletea faida katika familiya na jamii kwa ujumla. Mtafiti kupitia nadharia husika anawataka wanawake wengi hasa wale wanaojitambua wa Kiafrika wabadilike tena na sasa wasiwe tayari kuburuzwa na kuzushiwa mambo ambayo hawakustahiki au hawakuyatenda hususan maovu kama wizi na unyang'anyi mithili aliyofanyiwa Maimuna. Wanawake walio wengi hususan wa sasa wanajitambua vyema na hii kwa sababu wengi wao wamesoma na wanaendelea kutetea haki zao ipasavyo kutoka kwa waume zao au wale wenye mamlaka juu yao au wengineo.

### 4.5.5 Mwanamke Kama Muhusika Mlezi wa Familiya

Kila binaadamu au kiumbe ana haki zake katika jamii. Kwa misingi hiyo kila mmoja wetu anatakiwa asimamie, aheshimu, athamini na alinde haki za kila binaadamu au kiumbe katika misingi inayostahiki. Kwa mfano mwanamume (mume) ana haki zake kwa mwanamke (mke) na Mwanamke (mke) ana haki zake kwa mwanamume (mume) na kila mmoja anahitajika azitimize kwa kadiri ya uwezo na juhudi zake zote alizojaaliwa.

Suala la ulezi ni kazi nzito, inahitajika juhudi ya makusudi katika kuimarisha familiya ilio bora. Mashirikiano mazuri baina ya mume na mke huimarisha mapenzi na kuachana na utegemezi wa upande mmoja. Kwa hakika mtafiti amebaini kuwa suala la ulezi wa familiya kwa baadhi ya familiya linamwelemea zaidi mwanamke kuliko mwanamume. Baadhi ya wanaume hawajali na hawatoi msaada au mashirikiano kwa wake na familia zao na hivyo basi zigo hilo zito hulibeba

mwanamke au mke peke yake kulea na kusimamia familiya ikiwemo ulezi wa watoto na utafutaji wa chakula na huduma nyengine. Jambo hili lilihitajika na mume ashiriki kikamiifu katika ulezi wa familiya.

Katika kulizingatia hilo, mtafiti amebaini tabia ya baadhi ya wanaume (waume) kutozijali familiya zao. Waume hao katika harakati zao za kimaisha fedha wanazozipata huzitumia kwa kulewa na kushindwa kuwafikiria watoto na wake zao majumbani kwao. Katika kulijadili hilo, mtafiti anathibitisha kupitia malalamiko ya Selume kwa mumewe Shoka. Mwandishi anasema:

> "Kukosa huko kwa kila siku? Selume alijitetea. 'A-a, si kama pesa hupati Shoka, Lakini ulevi na …Mume wangu, ukiingia chicha, ukitoka chicha. Na hadithi zako nazisikia nje. Dunia duara haina siri, ni uwanda wa jangwa huu, ulifanyalo liko nje' …… Mwisho wa habari, wewe mtu una nyumba na watoto, unakwenda kula mkahawani. Unaupiga wali wako uzuri, ukija hapa unajitia njaa ya Majuju wa Majuju. Ee basi inajuzu hivyo? Huna hata imani. Nyooo, mjalaana we! Si mjalaana wewe kwa hakika, vitendo vyako! Nenda huko vilabuni nami niache na ulimwengu wangu. Niache nibebe mizigo nisiyostahili kuibeba….." (Uk.111 - 112)

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa tabia hii ya baadhi ya wanaume au waume ya kukimbia majukumu yao bado inaendelea katika jamii zetu. Hivyo basi ni vyema jamii zikasimama imara kuhakikisha tabia hizi zinakomeshwa na kila mtu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kwa upande wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, imelenga kuwahamasisha wanawake wawe mstari wa mbele kuwakumbusha baadhi ya wanaume au waume ambao hawatimizi vyema majukumu yao. Kwa ujumla mtafiti anakubali kuwa nadharia hii inasisitiza kila mmoja awe imara kusimamia majukumu yake ipasavyo

na isiwe mzigo mzito anabebeshwa mwanamke tu jambo ambalo linalazimika kufanywa na wanaume.

### 4.5.6 Mwanamke Kama Muhusika Tabibu / Daktari wa Kienyeji

Udaktari ni katika fani muhimu katika maisha ya jamii yeyote. Kuwa daktari au tabibu sio jambo la mzaha, inahitajika uwezo mkubwa wa taaluma katika fani husika ili muhusika aweze kutumika kusaidia na kuokoa maisha ya binaadamu na viumbe vyengine. Fani ya udaktari au utabibu wa kienyeji ni ile fani inayotumia utoaji wa msaada wa kitabibu / kiafya pasi na kutumia hospitali. Tabibu wa kienyeji ana mchango mkubwa katika kusaidia kuokoa maisha ya mwanaadamu lakini kwa kutumia matibabu ya kienyeji kama miti shamba, majani, mizizi, hirizi, dua nk. Katika riwaya ya *Utengano* tunamuona Bi Farashuu akiwa tabibu wa kienyeji ambapo kazi yake hasa ni ukunga (kuzalisha wanawake wajawazito) Bi Farashuu alifanikiwa kumsaidia na kumzalisha vyema Bi Tamima akishirikiana na Biti Kocho na watumishi wengine katika jumba la Bwana Maksuudi. Mwandishi anasema:

> Farashuu alimkuta Bi Tamima tayari tayari. Alikuwa kishavunja chupa ya kitoto kingezaliwa dakika yoyote. Farashuu aliingia kazini. Hima alimweka mjamzito katika hali ya kungojea….. 'Haya natumvue nguo ' Farashuu akasaidiana na Kocho wake wakamvua nguo Bi Tamima na kumtupia kanga. Bi Tamima akaumana na maumivu yake. Na kama kawaida, uchungu ulipozidi Tamima alianza kuusia, akadai talaka, akaomboleza. Bi Farashuu aliyekuwa kakaa kwa makini, alikuwa kimya, ila muda hata muda alimpa moyo mzazi…. Wakati ulipofika, Bi Tamima aliuma meno. Haya, haya, kidogo kidogo; hatimaye Farashuu alimpokea mtoto. … Safari hii uzazi haukumfanyia taabu. Alijifungua salama usalimini. Farashuu alipokwisha mpokea mtoto alikamilisha ukunga wake. Akamhudumia mtoto na mzazi. (Uk 34 - 35)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imekuwa ni tegemeo kwa jamii hasa kwa mwanamke. Kwa mfano katika dondoo hii imekuwa na umuhimu kwa mtafiti kwa

sababu imedhihirisha kuwa mwanamke ni mtu muhimu na ni msaada mkubwa katika kunusuru maisha ya wengine. Kazi ya ukunga ni kazi ambayo pamoja na kwamba ni ya kienyeji lakini ina mchango mkubwa katika maisha yetu ya kila siku. Mkunga ni lazima awe na taaluma ya kutosha ili aifanye kazi hiyo vyema. Hivyo ni vyema ikaheshimiwa.

### 4.5.7 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni miongoni mwa raslimali adhimu na iliyotukuka katika kujenga familia na jamii au taifa imara popote duniani. Msingi wa kuwepo kwa mapenzi ya dhati hasa katika ndoa huimarisha masikilizano, mashirikiano, uaminifu, matunzo, heshima, nidhamu, uvumilivu na kuhurumiana, usawa wa haki na uadilifu kwa wahusika. Mapenzi ya dhati katika jamii yeyote huhitajika kwa lengo la kuimarisha familia na jamii husika. Katika utafiti huu, mtafiti amegundua suala la mapenzi ya dhati limechukua nafasi katika riwaya ya *Utengano* na kulipa umuhimu mkubwa. Mwandishi katika kulijadili hilo amemtumia muhusika wake Maimuna na Kabi. Wote walikuwa wanapendana kwa dhati na baadae walifunga ndoa na kuishi pamoja kwa upendo uliotukuka. Mwandishi anasema:

> "…Muda ulipita. Kabi alishangaa akawa anamtazama Maimuna na kusubiri. Mwishowe Kabi alikuwa tayari kuuelezea undani wake, 'Sikiliza Maimuna, mimi niko tayari kukuoa kwa hali yoyote…" (Uk. 162)

> "Kijumba kipya cha Kabi na Maimuna kilijengwa Hitama, kijiji kimoja cha shamba, huko Liwazoni. Kabi na Maimuna wameoana sasa inapata mwaka, na wamehama Futoni. Hii ni kwa pendekezo la bibi mtu, Bi Farashuu. Bi Farashuu aliona wajukuu wake watanufaika zaidi huko Hitama, kijiji chenye rutuba ya nchi kavu na baharini……" (Uk. 171)

Kwa hakika utafiti huu umedhihirisha dhana nzima ya mapenzi ya dhati ambayo ambayo huwafanya wahusika kuhitajiana na kuthaminiana kila mmoja. Kwa mfano mapenzi ya dhati baina ya Kabi na Maimuna yaliwawezesha kuoana na kuishi pamoja bila kujali mapungufu ya kila mmojawao.

Mapenzi ya dhati pia yanalenga dhana nzima ya kusameheana watu / wanaadamu wanapokoseana au wanapotengana hususan wale ambao ni familiya moja. Misukosuko katika maisha huweza kupelekea familia kutengana na huweza kusababisha athari kubwa kwa familiya hiyo na jamii kwa ujumla. Mfano mzuri ni familiya ya Bwana Maksuudi. Kutengana huko baina ya Maksuudi na mkewe Bi Tamima, na watoto wao Mussa na Maimuna. Kwa ujumla pamoja na tofauti hizo mwishowe waliweza kusameheana na kuishi tena kwa upendo (Uk. 172 - 176)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatetea umuhimu wa kuwa na mapenzi ya dhati ili kuweza kujenga jamii iliyo bora na kuepukana na ubaguzi au udhalilishaji. Katika nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika inatilia mkazo mwanamke na mwanamme kuwa na haki na usawa katika masuala mbalimbali katika yale yanayostahiki ikiwemo mapenzi ya dhati baina yao. Mtafiti anaunga mkono kuwa mapenzi ya dhati husaidia kujenga familia bora yenye Umoja na Mashirikiano yaliyo imara ambayo yataleta tija katika jamii zetu. Jamii zetu za Kiafrika ikiwemo jamii ya Watanzania husisitizwa kulizingatia hilo kwa kuwa ni miongoni mwa misingi muhimu ya maisha ya kila siku kwa kila binaadamu.

### 4.5.8 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Tabia ya Ushawishi Na Uchochezi

Tabia ya Ushawishi na Uchochezi ni kitendo cha kufanya mazungumzo au

mawasiliano na mtu au watu kwa lengo la kuridhia au kukubali kufanya matendo ambayo mara nyingi huwa hayana faida kwa muhusika au jamii. Mtafiti amebaini kuwepo kwa tabia hii kwa baadhi ya wanawake ambao ushawishi au uchochezi wao ni kufikia malengo mahsusi binafsi. Mfano mzuri mwandishi amemtumia muhusika Biti Kocho kumshawishi Maimuna ili atoke na aongozane nae kwenda kumtafuta mkunga ambaye atamsaidia mama yake kujifungua. Mwandishi anasema:

> "Liwe hili la leo, la uhai na mauti, aliendelea Biti Kocho, 'hospitali na daktari potelea mbali, hata mkunga wa kikwetu? Ndo zitashuka mbingu akiingia humu huyo mkunga? A-a, makubwa jama. Japo kuwa mtu anakufa? Sana akija babaako sisi tutakufichieni, atajuaje? Na akija kwa meno ya juu, nani kamzalisha Tamima? Mimi nitapiga kifua na kuikabili hiyo na kama atayoiteremsha, si basi?"…"Lakini leo kuna faradhi. Hakuna kubwa lisilokuwa na kubwa mwenzake. Mtu kumwokoa mamaake si jambo dogo. 'Mwana, usifanye mchezo…' kauli ya Biti Kocho ilimgonga tena Maimuna kichwani mwake. Ikamzindua"…"Twende mama, alijibu bila kufikiri zaidi. Mbele ya mastaajabu ya waliokuwepo, na bila ya taarifa ya mamaake, Maimuna alitoa buibui lake, yeye na Biti Kocho wakawa wanateremka ngazi kuelekea Madongoporomoka" (Uk. 22-24)

Utafiti huu kupitia dondoo hizi zimedhihirisha wazi juhudi za Biti Kocho kumshawishi Maimuna aridhie kufuatana nae ili watoke nje ya jumba la Bwana Maksuudi jambo ambalo halikubaliki na ni hatari kwake na familiya hiyo. Hii ni kwa sababu Maksuudi aliiweka familiya yake katika utawa. Mbali na hilo kutoka nje kwa Maimuna ilikuwa ni sababu kubwa ya kumtoa katika utawa  na kumfanya awe huru na ni mpango wa Biti Kocho, Bi Farashuu na wenzake kumtenganisha na baba yake au familiya kwa ujumla.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetusaidia kuweka bayana juu ya tabia ya baadhi ya wanawake kuendeleza suala zima la Ushawishi na Uchochezi. Katika jamii zetu za Kiafrika tabia hii inaendelea kuchukua nafasi ingawa baadhi ya wanawake

wenyewe wanakerwa na kuchukizwa na tabia hizo mbaya. Mtafiti ameona kuwa masuala haya hupelekea kufikia hatua ya unafiki, usaliti, uhasama, uadui na vita baina ya wanawake kwa wanawake au wanawake kwa wanaume au vyenginevyo. Kwa msingi huo tabia za Ushawishi na Uchochezi ni tabia mbaya na kupitia nadharia hii wahusika wenye tabia hii wanaaswa waachane na watende matendo mema ili wawe ni mfano kwa wengine.

### 4.5.9 Mwanamke Kama Muhusika wa Mipango na Hadaa

Mipango na Hadaa ni miongoni mwa matendo ambayo yanaendelea kuchukua nafasi katika maisha yetu ya kila siku. Baadhi ya watu wakiwemo wanawake hubuni mipango ambayo baadae huleta athari kubwa hata katika familiya. Mtafiti amebaini mipango na hadaa hizo huchangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo kisasi kwa matendo aliyotendewa mtu binafsi, familiya au rafiki.

Kwa hakika, mtafiti amegundua juhudi, mipango na hadaa za Kazija, Biti Kocho na Bi Farashuu walizozitumia kuwatenganisha Bwana Maksuudi na familiya yake wakiwemo wanawe Maimuna na Mussa. Mwandishi anaeleza kupitia Biti Kocho kwa Bi Farashuu

> “Bibi we, anokutenda mtende, mche asokutenda. Bwana Maksuudi alivyokutenda wewe je? ‘Mimi nitalipa kisasi Biti Kocho. Bado nalia na kilio changu hakijanyamaza. Lakini sasa saa ngapi? Farashuu alitazama saa yake mezani. ‘Saa saba, kasorobo. Nadhani tutawahi” (Uk. 32).

Mbali na hayo mwandishi anafafanua juhudi za Biti Kocho na Bi Farashuu kumtorosha Maimuna kutoka nyumbani kwao kwa Bwana Maksuudi usiku na ikawa ndio sababu ya kumtenganisha na wazazi wake. Mwandishi anaeleza:

> “Sasa ilikuwa wazi, Maimuna akitoka, itakuwa katoka mwenyewe. Hakutoka na Biti Kocho wala Farashuu. Biti Kocho ndio yumo ndani, na mkunga ametoka peke yake mbele ya macho ya watu wote. Biti Kocho hakujali kwa lolote. Hapana ambaye angedhani kuwa kule kutoka naye Maimuna kwenda kwa mkunga ndio kuwe kumehusika na kukimbia Maimuna sasa. Na hata kufahamike hivyo, nani ambaye angalithubutu kumtaja Biti Kocho nyumba ile ila mwenyewe Bi Tamima, ambaye yeye hakumwona alipotoka naye? Likija suala la kuleta mkunga, hilo tu, Biti Kocho ni kiasi chake. Wala haumpigi mshipa.Baada ya kitambo kifupi, baada ya kutoka Farashuu, Maimuna alivaa buibui lake, akanyatia kwa ustadi na kutoka bila ya kuonekana na mtu yeyote. Baadaye waliungana na Bi Farashuu wakaelekea Madongoporomoka. Walipofika huko ilikuwa saa nane unusu. Watoto wameshasukuma mikate na kulala” (Uk. 40 - 41)

Hapana shaka nukuuu hii imeengeza ladha na kuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu imesadifu namna mipango na hadaa zinaweza kuchukua nafasi katika kutimiza malengo ya wahusika mbalimbali kama ilivyotimia kwa Bi Farashuu na Biti Kocho kumtenganisha Maimuna na familiya yake.

Mtafiti kupitia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika amegundua kuwa nadharia hii imeendelea kutoa msisitizo kwamba matendo maovu sio mtaji. Wanawake wana nafasi kubwa katika kuhamasishana kuhusu maendeleo yao na taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kukemea na kuachana na tabia ya hadaa kwa wenzao au wengineo. Nadharia hii inawataka wanawake wajitambue na wasiwe tayari kujiingiza katika dhambi kama hizi ikiwemo ya kutumia hadaa katika masuala mbalimbali kama katika biashara, elimu na imani za kidini. Jambo hilo limekatazwa na haifai tabia hiyo kuigwa kwa hali yeyote.

### 4.5.10 Mwanamke Kama Muhusika Dhaifu Na Masikini

Dhana ya Udhaifu, kuonewa na kushindwa kujitetea ni miongoni mwa matatizo makubwa yanayoendelea kuwakabili wanawake wingi duniani kwa sababu ya hali

zao kuwa ni masikini. Mtafiti amebaini kuwa matatizo ya aina hii huwafanya wanawake wakati mwengine wakose haki zao za msingi kama matunzo, kuhudumikiwa na mapenzi ya dhati hususan kutoka kwa wanaume. Wakati mwengine matatizo haya huchangiwa kwa kuwa wanawake hao ni masikini na kiafya ni dhaifu na duni ukilinganisha na wanaume katika ndoa zao.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa baadhi ya wanawake ni tegemezi kwa asilimia karibu mia ya mahitajio yao yote kwa waume zao na hulazimika kukubali kukumbwa na visa na mikasa, maonevu na udhalilishaji bila ya kujali kipindi walicho kama cha ugonjwa, ujauzito au mara tu baada ya kujifungua au kuwa kwenye utawa wa mume. Hali hii inapojitokeza hushindwa kuthaminika na kwao kukosa mwelekeo pindi wanapoachwa.

Katika kulifafanua hilo, mwandishi amemtumia Bi Tamima ambaye aliadhibiwa vikali na mumewe Bwana Makusuudi kwa sababu tu ya kujifungua na kutokuwa muwazi kumtaja aliyemzalisha na pia kwa kutokusema Maimuna amekwenda wapi; hali ya kuwa hata Bi Tamima hakujua namna alivyotoroka Maimuna. Maimuna alishindwa kujitetea na kwa sababu hakujua vipi ataendelea kuishi na kwa sababu ni masikini asiye na mwelekeo. Kwa misingi hiyo aliadhibiwa vikali hata kama aliomba msamaha. Mwandishi anasema:

> "Bi Tamima hakujua jengine la maana; na udhaifu wake, alinyanyuka taratibu pale alipokuwa kapinduka akajivuta kusogea kwa mumewe. Alipofika karibu yake, alianguka na kumpigia goti. Alimsogonea mumewe amlaani bilisi. 'Ni… nisameeeeehe bwaaana Mak-maksuudi, si kosa languuuuuu; Maimu…na kakimbiaaaa…' Tamima alilia kwa nguvu.

> Raaap! Ukanda ulitua juu ya mwili wa Tamima. 'Mtumeeee,' alisalia Tamima huku akiangukia meza iliyokuwa na buli na vikombe vya kahawa vya fedha. Hivyo akaenda navyo chini pamoja. Maksuudi aliendelea kumpiga Tamima kanda za mafamba. Tamima hakujua njia ya kujikinga. Maksuudi aliendelea kucharaza. Tamima zilimtoka mtume nyingi. Hakuwa na hila wala rai ya kujiokoa. Pale chini alibaki kusota –malele na huku Maksuudi akimrapua kwa ukanda. Akamwandama ukumbi mzima. Vitu vya mapambo vikaanguka. Maksuudi aliendelea kumrapua Tamima; mara kipembe kile na mara amvute mkono amlete katikati ya ukumbi. Ilikuwa hujma isiyokuwa na mwombezi, na Maksuudi alipiga kama mwendawazimu" (Uk. 48-49)

Mbali na Bi Tamima, hata Mwanasururu ambaye alikuwa mke wa Bwana Maksuudi na mtoto wa Bi Farashuu, sababu ya kifo chake ilitokana na kupigwa na kudhulumiwa mali yake na Bw. Maksuudi na kuachwa masikini. Mwandishi anaeleza kupitia Bi Farashuu:

> "….. Kwenye meza kulikuwa na picha kubwa ya mwanawe, Mwanasururu. Huyu ameshatengana na ulimwengu, amekufa kabla zake. Na Maksuudi, huyu Maksuudi, ndiye aliyekuwa sababu ya kifo chake. Na ile mali ya mwanawe ambayo ilikuwa ikimwendesha yeye Mwanasururu na Farashuu mamaake, yote imefisidiwa na huyu Maksuudi" (Uk.60)

Mtafiti kwa ujumla amebaini usawiri wa mwanamke katika baadhi ya familiya na jamii huwa katika hali ya mateso na idhilali. Wanawake kwa kuwa wao ni binaadamu wanapoomba msamaha huwa hawasilikilizwi na baadhi ya wanaume hujiona wanavyofanya ni sahihi jambo ambalo si sahihi. Tabia hii inahitajika ipigwe vita na kukomeshwa katika jamii zetu ipasavyo.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika iko imara kuamsha hisia hususan za Waafrika ya kwamba wasiwe tayari kuonewa hususan katika kutetea haki zao. Mtafiti amebaini kuwa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni tochi inayoangaza katika kumzindua

mwanamke asiwe dhaifu, na badala yake pamoja na umasikini wake mwanamke asimamie kuhakikisha anaondokana na tabia ile ya kuonewa na kudhalilishwa na wanaume bila ya sababu za msingi. Ingawaje msingi mkubwa wa utetezi wake unatakiwa uzingatie Haki na Sheria za nchi husika kwa usahihi.

### 4.5.11 Mwanamke Kama Mhusika Mtenda Rushwa

"Rushwa ni Adui wa Haki" Ni kauli ambayo hukaririwa katika kila jamii ambayo huchukizwa na tabia hiyo. Pamoja na kelele na mbinu mbalimbali zinazotumiwa na taasisi kadhaa au serekali kupambana na rushwa bado tatizo hili linaendelea kuuchukua nafasi katika maisha yetu. Kwa mfano nchini Tanzania serekali kupitia TAKUKURU imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuzuia na kupambanana lakini bado watoaji na wapokeaji rushwa wamejaa katika jamii zetu. Jambo hili linastahiki kupigwa vita vikali.

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa na mtafiti, utafiti huu umebaini tabia ya baadhi ya wanawake kutoa na kupokea rushwa ya fedha kwa malengo tu wasaidiwe kufanikisha mahitajio yao. Katika kulieleza hilo mwandishi amemtumia muhusika Biti Kocho ambaye aliomba akopeshwe fedha na Bi Farashuu ili akampe rushwa karani anayehusika na viwanja ili na yeye ifanyike mipango ya kupata kiwanja. Mwandishi anafafanua:

> "Mm-u, na mimi niwache kidogo nijinyooshe. Sijalala usiku kucha. Nina mavune makubwa…Ee, nisije nikasahau. Vile vipesa vipi nilivyokwambia unikaridhi' 'Sisahau bibi we, shilingi ngapi vile?' 'Miteni tu' alisema kwa mkato. 'Na tu kweli, ndio maana ukavita vijipesa. Na nyinyi? Shilingi mia mbili ni tu?' 'Ah bibi we, kupeana ni kikoa. Nataka kwenda kumpa Yule karani wa viwanja, chai yake, anifanyie mipango nikipate kile kiwanja' Yakaishia hapo" (Uk.62)

Kwa ujumla mtafiti amegundua kuwa, tabia hii ya kutoa na kupokea rushwa bado inaendelea katika jamii zetu kutoka ngazi za juu hadi za chini. Mbali na hilo kutoka sekta na taasisi binafsi hadi taasisi za serekali, jambo ambalo hurejesha nyuma haki za waliowengi na kufinyaa kwa maendeleo ya jamii husika.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapingana mno na matendo maovu dhidi ya wanawake kwa wanawake au wanawake kwa wanaume. Tabia ya Kutoa au kupokea rushwa ni jambo ambalo linapigwa vita si Afrika pekee bali hata duniani kwa ujumla. Hivyo basi, Mtafiti kupitia nadharia hii anawataka wanawake hasa Waafrika wasijiingize katika janga hilo la kutoa au kupokea rushwa ya aina yeyote na kwa yeyote. Hii itawasaidia  kuishi kwa amani, utulivu na upendo katika jamii husika ikiwemo Tanzania.

### 4.5.12 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe Kwa Mwanamme

Biashara ya danguro na ukahaba ni ile tabia mbaya ya baadhi ya wanawake kujishughulisha katika kuuza miili yao kwa wanaume kwa lengo la wanaume hao kujitosheleza mahitajio yao ya kimwili. Tabia hii bado inaendelea kushika kasi katika jamii mbalimbali  ikiwemo jamii ya watanzania. Sambamba na hilo baadhi ya wanawake wamekuwa wakitumika kama chombo cha starehe kwa wanaume. Jambo hili huweza kusababisha kuendelea kwa maradhi hatari yakiwemo yale ya UKIMWI. Mwandishi katika kulifafanua hilo amemtumia mama Jeni ambaye alikuwa mmiliki wa danguro huko Pumziko. Biashara ya kuuza miili kwa wanaume iliendeshwa na mama Jeni kupitia Maimuna na Dora ingawaje Maimuna hakuwa tayari kuuza mwili wake kwa James. Mwandishi anafafanua:

> " ….Sitaki' Maimuna alijikwapua na kuepa mikono ya James kwa hamaki. Alimgeukia Maimuna, akatanua mikono yake. Tayari kumwinda tena mwanamke huyu. Moyo unamtuta, macho kayatoa, anahema. Kadhamiria moja tu…Sasa James alikuwa anakuja kwa matao ya mtu aliyekuwa na uhakika ya ushindi, …. Na pale alipofika karibu na Maimuna alichupa kama kirongwe, lakini Maimuna aliepa na James akapinduka chini ya ukuta. Dakika hiyo hiyo Maimuna alitimka mbio…" (Uk. 56 - 57)

Mtafiti kupitia dondoo hii inadhihirisha wazi juhudi za baadhi ya wanawake kutokuwa tayari kutumika kama bidhaa au chombo cha kumstareheshea mwanamme. Hali hii inastahiki kuungwa mkono na jamii nzima ya kwamba tabia ya wanawake kutumika kama chombo cha starehe haistahiki kuwepo katika jamii zetu. Kwa upande mwengine mwanamke ametumika kama chombo cha starehe kwa mwanaume kwa lengo la kujipatia fedha na tamaa. Mfano mzuri ni kupitia kwa muhusika Dora katika danguro la mama Jeni. Mwandishi anathibitisha hayo:

> "Kutoka ukumbini alichomoza mwanamke mmoja aliyekuwa akimwongoza mwanamme. Mwanamke huyu mwembamba alikuwa kavaa shati na blauzi manjano iliyoandikwa Toyota. Shingoni mkufu wa shaba ulimning'inia. Walipopishana huyu mwanamke alichekacheka, akamwamkia Mama Jeni. Shikamoo…. Hatimaye Yule mwanamke alijichoma chumbani na bwanaake akafuatia huku akiufunga mlango kwa nguvu….." (Uk. 64 - 65)

Mbali na mwanamke kutumika kama chombo cha starehe katika mapenzi, mwanamke pia ametumia kama chombo cha starehe katika kutoa burudani ya kuimba ikiwa ni sehemu katika kazi zake. Mfano mzuri ni kupitia Maimuna alipokuwa muimbaji kule Rumbalola Hotel. Mwandishi anaeleza:

> "Muziki ulianzwa kugongwa kwa mahadhi ya rumba. Maimuna katikati ya shangwe aliteremka vidaraja kuelekea pale penye zulia katikati ya ukumbi. Njiani alipokea kikuza sauti kutoka kwa yule mtangazaji. Akaanza kuyumbayumba kwa madaha. Alibembea na mdundo huku mwili wake kaulegeza na macho yanasinzia. Muziki ulipofika pahala fulani, alianza kuimba,

“Nina kovu, nina kovu, Wanitonesha kwa inda,
Ukikatazwa maovu, Warudi wenda yatenda?
Wanitia roho mbovu, Kwa sababu nakupenda?
Nakupenda, nakupenda, Kwa sababu nakupenda
…….. ……...” (Uk. 124 - 125)

Mtafiti kwa hakika kabisa amegundua bado tabia ya kumtumia au kujitumikisha mwanamke kama chombo cha starehe ipo katika jamii zetu na hakuna shaka yeyote tabia hiyo si njema si kwa mwanamke tu hata kwa mawanamme na jamii kwa ujumla. Ni vyema tukaachana na tabia hiyo na kumuona mwanamke au mwanamke mwenyewe kutambua thamani yake na kutokuwa tayari kutumika kama bidhaa kwa wanaume nk.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika katika utetezi wake wa wanawake inawakumbusha kuwa wao sio bidhaa au chombo tu cha kumfurahisha / kumstarehesha mwanamme. Wanawake ni binaadamu na wana haki inayostahiki kwa kuzingatia hali zao. Mtafiti anawataka wanawake waachane na tabia kutumika kama ni chombo au bidhaa ya kumstarehesha mwanmme pasipo stahiki. Waachane na tabia ya kujidhalilisha kwa matashi binafsi isipokuwa haki ya kustarehe kihalali iko kwa waume zao kwa umoja wao.

### 4.5.13 Mwanamke Kama Muhusika Mlevi

Ulevi bado ni miongoni mwa tabia mbaya ambayo baadhi ya watu huiendeleza. Ulevi katika jamii yeyote una athari kubwa na huchangia kurejesha nyuma maendeleo ya taifa. Hii ni kwa sababu wale wanaoendekeza ulevi hushindwa kutimiza majukumu yao ya kikazi ipasavyo. Pia ufanisi katika kazi hukosekana kwa

sababu watendaji ni walevi. Akili zao huwa haziko timamu. Utafiti huu umebaini baadhi ya wahusika wakiwemo wanawake wamekuwa wakiendesha biashara ya ulevi na baadhi ya wanywaji pia ni wanawake. Miongoni mwa wanawake wanaojishughulisha na ulevi ni pamoja na Biti Sururu, Kijakazi na Maimuna. Mfano mwandishi anamweleza Maimuna ambaye alilewa:

> "Maimuna alipiga moyo konde, akagugubia. Lo, ulikuwa mrututu. Mrututu uliochanganyika na kakasi, uchachu, uchungu, na ubabuaji. 'Ni asidi, ni asidi, ulevi wa gongo,' Maimuna alikumbuka maneno ya Dora aliyokuwa akimwambia kila siku. Maimuna alilitua kopo. Akachichimkwa tena na mwili. Ndani aliyasikia machango yake yalivyokuwa yakipaparika na kujitetea. Aliisikiliza vyema pombe na hatimaye ilipoa pahala fulani. Hapo tena ndipo nadhari yake iliporudi. Akaishika" (Uk. 91)

Mtafiti kupitia nukuu hii inasawiri na uhalisia wa tabia za aina hii za baadhi ya wanawake wanaoendekeza ulevi na hatma yao afya zao kuwa dhaifu zaidi. Mfano zaidi na uhalisia wa afya ya Maimuna baada ya kuendekeza ulevi . Mwandishi anaeleza:

> "…. Biti Sururu aligundua kuwa ngozi ya Maimuna ilikuwa ikifichua mikunjo midogo midogo ya siri ambayo bado ilikuwa inastahi kudhihiri kwa uwazi. Uti wake wa mgongo ulikuwa ukitoa tindi kama gurunzi la mua, ulionekana waziwazi, toka shingoni mpaka ulipoishia. Nundu la fupa la bega, la kushoto na kulia lilichomoza kwenye uchache wa nyama. Ngozi ya tumbo ilikuwa na mapeto ya siri. Mvundumuko bado upo, lakini hakujaza, ulikuwa umeyayuka mafuta. Huyo ndiye Maimuna aliyebaki baada ya kufyonzwa na ulimwengu" (Uk. 135)

Mtafiti kupitia dondoo hizi zimetoa picha halisi ya wale wenye tabia za ulevi na afya zao huwa mbaya hukabiliwa na ugumu wa maisha. Hivyo basi tabia ya ulevi haifai kuigwa. Nadharia ya Ufeministi bado inaliangazia suala la ulevi kuwa miongoni mwa matendo maovu ambayo baadhi ya wanawake hususan wa Kiafrika wanaendelea kulitekeleza. Mtafiti anaona kuwa ulevi sio suluhisho au biashara

muwafaka katika jamii zetu. Mtafiti anasisitiza kuwa ulevi hupoteza nguvu kazi ya vijana na kuzorotesha maendeleo ya taifa. Kwa minajili hiyo, mtafiti anaitaka jamii kupitia wanawake wabadilike, waache tabia ya ulevi na wajitolee kufanya kazi za halali kwa juhudi kubwa ipasavyo.

### 4.5.14 Mwanamke Kama Muhusika Mgomvi (Mshari)

Tabia ya ugomvi au ushari bado imezoeleka kwa baadhi ya wanawake katika jamii zetu. Baadhi ya wanawake huwa na tabia hii mbaya na hatma yake huweza kuleta athari kubwa kwa jamii ikiwemo kuvunja uhusiano (urafiki), kuendeleza kuwepo kwa visasi, matusi, uhasama na mfano wa hayo. Utafiti huu, umebaini tabia hii mbaya kupitia Kijakazi na Maimuna ambao baadae walipigana na kuumiza vibaya. Mwandishi anaeleza:

> "Lo! Yasin, mwanamke gani naye wa kukustua wewe Shoka. Si basi tu huna kazi' Kijakazi alimtazama Maimuna kwa jicho lililomtambulisha Maimuna kuwa maneno hayo ni yake. 'Shoti anavyoringa, utafikiri si bao la mkahawani. Nani naye anayeshtua watu, akitupiwa mbwa hamtaki.' Kijakazi aliendelea kutia mchanga wa moto…(Uk. 139)

> "Nataka unambie kwanza…nambie lile ulilolisema. Kama huwezi, unyamaze maisha… Na basi bibi usishindane na Kari, Kari mja wa Mungu. Kupata na kukosa kwangu kusikushughulishe wewe. Ukome kama ulivyolikoma la mamayo, mwana…' Hapo hapo Maimuna alimzaba kibao Kijakazi na kabla ya vile vimulimuli alivyokuwa akiviona Kijakazi havijapotea, alishtukia kavamiwa na Maimuna. Hao, walipinduka pamoja. Shoka karuka kule kipembeni. Meza, viti na makopo – vyote chini. Wakabingirishana. Mara Maimuna juu, mara Kijakazi juu. Makofi, minyukuo, magumi, meno, pumzi juu juu. Ukwenzi ulizuka na halafu ukajibiwa na mwengine….. " (Uk. 143)

Kwa kurejelea data hii imesawiri kwa uwazi tabia mbaya ya ugomvi na ushari kwa baadhi ya wanawake. Ingawa baadhi ya wanaume wanayo tabia hii ambayo ni vyema kuachwa.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaona kuwa Ugomvi au Ushari si miongoni mwa sifa nzuri kwa wanawake. Kwa ujumla wanawake ni watu wa kuheshimiwa na kuthaminiwa, kuenziwa na kuhudumikiwa ipasavyo na sio kujiingiza katika tabia hii mbaya. Mtafiti amegundua kuwa bado katika jamii zetu za Kiafrika tunao wanawake wenye tabia hii mbaya ya ushari au ugomvi, jambo ambalo halina faida yeyote kwao na hata wengineo. Kwa kuzingatia hilo, mtafiti kupitia nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika anawataka wanawake wajikite katika shughuli za kimaendeleo mfano vikundi vya ujasiriamali ambavyo vitawasaidia kujisogeza katika maisha yenye afadhali na hatimaye mafanikio yakiyotukuka kwa jamii zetu ikiwemo jamii ya Watanzania.

**Jadwali 4.1: Muhtasari wa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano**

| Na. | **Usawiri Wa Mwanamke Katika Riwaya Ya Utengano** |
|---|---|
| 01 | Mwanamke kama muhusika Mshauri mwema |
| 02 | Mwanamke kama muhusika Muwajibikaji (mwenye bidii katika Kazi) |
| 03 | Mwanamke kama muhusika Jasiri na mwenye Kujitoa mhanga |
| 04 | Mwanamke kama muhusika mwenye Msimamo thabiti |
| 05 | Mwanamke kama muhusika Mlezi wa familiya |
| 06 | Mwanamke kama muhusika Tabibu/ daktari wa kienyeji |
| 07 | Mwanamke kama muhusika mwenye Mapenzi ya dhati |
| 08 | Mwanamke kama muhusika mwenye tabia ya Ushawishi na Uchochezi |
| 09 | Mwanamke kama muhusika mwenye Mipango na Hadaa |
| 10 | Mwanamke kama muhusika Dhaifu na Masikini |
| 11 | Mwanamke kama muhusika mtenda Rushwa |
| 12 | Mwanamke kama muhusika Chombo cha starehe kwa mwanamme |
| 13 | Mwanamke kama muhusika Mlevi |
| 14 | Mwanamke kama muhusika Mgomvi (mshari) |

Chanzo: Data kutoka riwaya ya Utengano, 2016

Kwa ujumla mtafiti kupitia data alizozikusaanya na uchambuzi wake katika riwaya ya *Utengano* amefanikiwa kufafanua na kuthibitisha kwa uwazi usawiri wa

mwanamke kwa kuhusisha na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hivyo basi kwa kurejelea riwaya hiyo mtafiti anaiomba jamii iwe tayari kubadilika kwa kufuata yaliyo mema na kuwacha yalio maovu kama ambavyo imehusishwa na swali la msingi la kwanza pamoja na lengo mahsusi la kwanza la tafiti huu.

### 4.6 Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena

Riwaya ya *Kamwe si mbali tena*, kama ilivyo riwaya ya *Utengano* nayo imesheheni wahusika kadhaa wakiwemo wanawake na wanaume ambao mwandishi amewatumia kwa namna mbalimbali ili kufanikisha malengo na maswali ya utafiti huu. Kwa upande wa wahusika wanaume riiwaya imejumuisha baadhi ya wahusika wafuatao: Bwana Mansour (bwana Toba), Bwana Hassan, Bwana Haji, Bwana Kitwana, Bwana Mwandoa, Mzima, Mabruki, Abuu, Yasir, Selemani (Sele Msurupwete), Zahran na Tambo.

Kwa upande wa wahusika wanawake, riwaya hii imehusisha wahusika wanawake wafuatao; Bi Chani (Mwanamkisi/ Waridi/ Warida), Bi Halima, Bi Badria, Bi Alwiya, Bi Ruqaiya, Bi Fat-hiya, Bi Tabiba, Mwanamvua, Mwanaleo, Mwanakujua, Mwanahili, Salila, Jokha, Janet, Samira na Mwavile.

Kwa ujumla utafiti huu umejikita kuzingatia zaidi, kufafanua usawiri wa wahusika wanawake na hii ni kwa mnasaba wa mada husika. Wahusika wanaume wanaweza kujitokeza katika ushirikishwaji kwa baadhi ya matendo. Hivyo basi mtafiti kwa mujibu wa data alizozikusanya amechambua usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena.* Wahusika hao wanawake usawiri wao umejitokeza katika upande wa chanya (matendo mema) na upande wa hasi (matendo maovu). Katika

kuzingatia hayo mtafiti amechambua pande zote (chanya na hasi) kwa kuhusisha na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika huku akiendelea kujibu swali la kwanza la utafiti lisemalo:

ii) Ni kwa vipi usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?*

Katika kujibu vyema swali hilo, mtafiti amezingatia lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lisemao: Kufafanua usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*. Sambamba na hilo uchambuzi kuhusu usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya pili ya *Kamwe si mbali tena* umehusishwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Kwa mujibu wa data zilizokusaanywa na mtafiti usawiri huo wa mwanamke umejitokeza kama ifutavyo

### 4.6.1 Mwanamke Kama Muhusika Muwajibikaji (Bidii Katika Kazi)

Wajibu wa kuwahudumia wazazi au walezi ni jambo la lazima na la msingi. Ulazima wake au wajibu huu unajitokeza kwa kuwa wazazi au walezi hao walifanya kazi na juhudi kubwa kukulea wewe mtoto tangu ukiwa mdogo (mchanga) hadi sasa umekuwa mtumzima. Dini zote zinasisitiza kuwaenzi, kuwahudumia na kuwathamini wazazi/ walezi na hasa wanapokuwa watu wazima / wazee. Kufanya hivyo ni kujikurubisha kwao na kutafuta radhi zao na radhi za Mwenyezi Mungu mtukufu na malipo yao huwa ni Pepo. Uwajibikaji au kufanya kazi kwa bidii ya kuwahudumia wazazi/walezi husaidia sana kuwapa faraja na matumaini mema wazazi/walezi hao kwa watoto. Watoto wanapotekeleza vyema kazi hii huimarisha mapenzi kwa wazazi/ walezi hao hao na mapenzi inayoambatana na radhi kwa M/Mungu.

Katika riwaya hii, mwandishi amemtumia muhusika Mwavile ambaye alifanya juhudi kubwa ya kumlea, kumuhudumia, kumthamini na kumuenzi mama yake wa kulea Bi Chani kwa juhudi na kwa mapenzi makubwa huku watoto wake wa kuwazaa wakiwa wako Ulaya kutafuta maisha mazuri kama wasemavyo. Katika kulidhihirisha hilo mwandishi anasema:

> "Pamoja na yote hayo, yeye mwenyewe, mamake, Bi Chani, na Mwavile dadake wa kulea wasingeshindwa kupeleka mkono kinywani. Mwisho wa yote aliwambia ndugu zake waende tu. Wangeonana mwakani. Sababu kubwa ya kutotaka kuondoka nchini ni nia yake ya kutaka kutekeleza jukumu alilojipa mwenyewe. Jukumu la kumlea na kumtunza mamake. Na mamake ni mama yao. Alikuwa tayari kujazwa , moyoni mwake, fikra za kumtunza mamake. Hata kama atambeba mamake kwa namna ya kitikiti cha Mfaume"…… "Mwavile, aliyekuwa amesawijika na kuhuzunika pia, alimwambia Tambo kwa sauti iliyojaa hisia…"Nenda, Tambo. Nenda. Nenda pamoja na kaka na dada zako. Mimi nitabaki hapa kumlea na kumtunza mama yetu. Nitamtunza kwa viganja viwili. Inshalla nitamfikisha kwenye mwisho mwema kwa uwezo wa M/Mungu" (Uk.4-6)

Katika utafiti huu, mtafiti amebaini kwamba watoto wana wajibu wa kuwalea, kuwaenzi, kuwaheshimu na kuwatunza wazazi na walezi katika maisha yao yote pasi na kutoa sababu zisizo za msingi au vyenginevyo ili waweze kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni muongozo mmoja wapo muhimu katika kutambua thamani, heshima, uwezo na uhalisia wa hali za wanawake na utetezi wake. Mtafiti amebaini kuwa data alizozikusanya na kwa kupitia msaada wa nadharia hii, wanawake wanastahiki kutambulika ipasavyo katika jamii zetu hususan jamii za Kiafrika kwa kuwa uwezo wao mkubwa katika kusimamia mambo kadhaa ya kimaendeleo. Wanawake pia wana uwezo mkubwa wa kutimiza majukumu yao

ipasavyo tena kwa bidii kubwa ikiwa pamoja na kuwalea wazazi au walezi wao vyema.

### 4.6.2 Mwanamke Kama Muhusika Mtambuzi na Mwanahistoria

Kutambua historia kuna umuhimu wake katika jamii yeyote. Historia ni darasa tosha kwa vizazi vya leo na vile vya kesho. Jamii yeyote huweza kujifunza matukio mbalimbali yanayotokea duniani kwa yale yaliyo mema na yale yaliyo maovu na mwishowe huwa ni mafunzo makubwa kwa jamii husika.

Katika utafiti huu data zilizokusanywa zinadhihirisha kuwa mwanamke ana mchango mkubwa katika utambuzi wa historia ya jamii yake na jamii nyenginezo. Jambo ambalo huwa ni msingi wa kuwafunza wengineo. Utafiti huu umekuwa muhimu kwa sababu kupitia muhusika Bi Chani, mwandishi anamweleza juu ya uwezo wake wa kusimulia matukio ya zamani mno kwa usahihi na kuwa ndio somo kwa watoto wake na wengineo. Mwandishi anaeleza:

> "Mnajua kwamba hapa visiwani tangi la kupokea mafuta ya petrol lilijengwa pale gati – ndogo ya Mtakuja mwezi wa Agosti mwaka 1901? Lilijengwa na Messrs, Smith Mackenzie and Co. Tokea wakati huo sikuona kupotea mafuta ya petrol wala mafuta ya taa.' Alisita hapo kama kungojea ukweli uzame akilini mwa wasikilizaji wake. Kisha aliendelea kusema kwa usahihi kama vile kaseti inayozunguka kwenye chombo cha kutolea sauti"……" Mnajua kwamba mwezi wa Septemba mwaka 1905, mtambo wa kutoa umeme ulianzishwa visiwani hapa na Bwana J.A. Jones wa New York. Baada ya hapo mji wa Visiwa vya Viungo uling'ara mapema zaidi kuliko baadhi ya barabara za London ambazo zilikuwa zikitumia taa za gesi. Leo tuna umeme usiokuwa na hakika. mara upo mara haupo. Mara waaa, mara ziii! " Bi Chani alipoteza baadhi ya fahamu ndiyo, lakini hakupoteza usahihi wa matokeo makuu ya fahari yaliyoanzishwa visiwani ….." Paketi ya majani ya chai ya biashara ilianzishwa Dunga, Januari 1901, 'aliendelea kuorodhesha Bi Chani…." (Uk 89 - 90)

Hakuna shaka yeyote utafiti huu umekuwa na tija kwa kuwa umedhihirisha juhudi za baadhi ya wanawake kama Bi Chani kuwa na uwezo mkubwa wa kusimulia matukio ya zamani kwa usahihi ikiwa ni darasa tosha kwa wengine kutambua neema zilizokuwemo ndani ya jamii zetu, mfano katika visiwa vya Viungo. Wazazi kama hawa wanastahiki kuenziwa kwa kuwa ni walimu maridhawa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetusaidia sana kuelezea na kuhamasisha juu ya umuhimu wa kuwataka wanawake wakomboke ili wawe watambuzi wazuri wa historia ya jamii yao na jamii nyenginezo. Kwa upande wa mtafiti, amebaini kuwa wako baadhi ya wanawake ni wasomi na watambuzi wa historia vizuri. Kwa mfano katika jamii ya watanzania mke wa aliyekuwa rais wa kwanza wa Tanzania, Bi Maria Nyerere na mke wa aliyekuwa rais wa kwanza wa Zanzibar, Bi Fatma Karume, ni miongoni mwa wanawake wenye uwezo mkubwa wa kueleza historia na matukio mbalimbali Tanzania.

### 4.6.3 Mwanamke Kama Muhusika Mpenda Dini

Dini ni muongozo katika maisha yetu ya kilasiku. Kila binaadamu anatakiwa awe mtekelezaji mzuri wa dini katika misingi yake stahiki ili aweze kuishi vyema na kumuomba Mwenyezi Mungu atakapokufa amsamehe makosa yake na amjaalie awe ni miongoni mwa waja wa Peponi. Katika riwaya hii utafiti umedhihirisha usawiri wa kuwa mwanamke ni muhusika mpenda Dini kupitia Bi Chani ambaye mwanzo alikuwa akiitwa Waridi / Warida au Mwanamkisi. Mwandishi anafafanua:

> "Jambo la pili alilolitekeleza Warida kama ibada ni kwenda chuoni kwa mafunzo ya dini. Mwalimu wake Bwana Mwandoa, Alikuwa mshabiki wa Tariki ya Dandarawiya. Aina fulani ya ibada ya Sufism au Mysticism. Mafunzo ya mwalimu Mwandoa hayakuwa tu ya Kitabu Kitakatifu cha Mungu, bali pia mafunzo ya kujipeleka katika ukuruba wa mapenzi ya Mungu na Mtume wake kupitia njia ya Tawasuf, hasa kwa nyenzo za maulidi ya homu, maulidi ya barazanji, dhikr na nyuradi za matamko ya tasbihi zinazorudiarudia majina ya Mungu ili hatimaye kufikia ukamilifu wa kuwa chini ya Muumba wao."……"Warida alipenda kujitambulisha na Mungu na dini yake pia kwa njia ya vitendo kuliko maneno matupu yasiyo na mashiko katika maisha ya mwanadamu. Alijifundisha Kitabu cha Mungu kwa ilidili. Akahifadhi juzuu thelathini za Kitabu hicho na tafsiri yake kwa muda usiokuwa mrefu. Kisha akaingia katika hadithi za Mtume…. Jambo hili la ibada liliwafurahisha sana wazazi wake wote wawili walikuwa na fahari kubwa kwa vitendo alivyovifanya binti yao" (Uk. 108 - 109)

Data zilizokusanywa zimethibitisha usawiri wa mwanamke katika juhudi zake kubwa katika dini. Jambo hili linastahiki kuigwa ili kujenga jamii ambayo imejikita katika misingi ya kidini nakumtambua Mungu kwa kujiepusha na maovu na kutenda mema.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, inazingatia juu ya umuhimu na thamani ya mwanamke kwa mujibu wa imani ya kidini. Mtafiti ameona kuwa dini ina nafasi kuwa katika kumjenga mwanamke katika tabia njema na zinazostahiki kufuatwa na kuacha maovu. Wanawake hususan wa Kiafrika bado wana wajibu mkubwa wa kuwafunza wanawake wenzao wa Afrika na duniani kwa ujumla juu ya tabia njema. Kwa sasa juhudi hizo bado zinaendelezwa kupitia dini mbalimbali kama Dini ya Kiislam na Dini ya Ukiristo. Hapana shaka mtafiti anaona ni vyema wanawake hao kuendelea na juhudi hizo ipasavyo ili kujenga jamii za kiafrika zenye nidhamu na maadili mema.

### 4.6.4 Mwanamke Kama Muhusika Tabibu/ Daktari wa Kienyeji

Kuwa tabibu au daktari si jambo la mzaha au jepesi. Ni jambo linalohitaji kuwa na maarifa ya kutosha ili muhusika aweze kutoa huduma kwa wagonjwa ipasavyo na kwa uhakika zaidi. Utibabu au Udaktari wa kutumia mitishamba nao unahitaji maarifa ya kutosha kuweza kujua dawa ipi (mizizi, majani au matunda nk) gani yanaweza kuwa muafaka kutibu maradhi fulani kwa mgonjwa.

Katika kuzungumzia dhana ya utabibu au udaktari kwa kutumia Mitishamba, Dua, Makobe na Hirizi. Utafiti huu umegundua uwezo mkubwa alionao Bi Chani (Warida) katika kutibu wanaadamu ipasavyo. Hii ni kwa sababu elimu ya utabibu wa kutumia Mitishamba, Dua, Makobe na Hirizi alifunzwa na wazazi wake (babake na mamake) kwa mapenzi makubwa na yeye (Bi Chani) kufanya juhudi kuweza kuipata elimu hiyo. Mwandishi anafafanua zaidi:

> "Jambo la tatu ambalo ni la kidunia zaidi ni lile la yeye Warida kushiriki katika kazi ya babake na mamake kutibu watu kwa dawa za mitishamba, dua, makobe na hirizi. Kwani (kwa maneno madhubuti aliowasikia watu wakisema) Mungu kasema: Niombeni nikupeni!"……"Tokea mdogo wa miaka sita, Warida aliingizwa katika kazi hiyo. Akakua nayo hadi leo uzeeni. Hata kufikia umri huu alionao, watu huja nyumbani kwake kuja kutibiwa hiki na kile mara tu wakisikia fahamu za Bi Chani zimeamka angalau kwa muda mfupi' Hii ni amali tunayokuachia mwanetu, babake Bi Chani , Bwana Hassani, alikuwa akisema hivyo kila siku mpaka mdomo wake ulipofumba milele" (Uk. 110)

Mbali ya Bi Chani hata Mwavile aliweza kupata elimu ya utabibu kutoka kwa mamake wa kulea Bi Chani na aliweza kutoa matibabu hayo vyema kwa wagonjwa akiwemo kaka yake Abuu kama anavyosema mwandishi.

> " Kwa ufundi wa uganga aliourithi Mwavile kwa mamake wa kulea, Bi Chani, Abuu alianza kupewa madawa ya mitishamba na mchanganyiko wa vyakula vyenye rutuba …." (Uk. 138)

Kwa mtafiti kupitia data hizo zimeweka bayana uwezo na mapenzi makubwa ya wazazi kwa watoto wao. Mfano mzuri ni kutoka kwa wazazi wa Bi Chani kumpatia elimu ya utabibu wa mitishamba mtoto wao na yeye (Bi Chani) kumfunza mwanawe wa kumlea Mwavile kwa moyo wao wote. Bila shaka ni amali ya kuzingatiwa na wanajamii.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni miongoni mwa nyenzo muhimu katika kumkomboa mwanamke ikiwa ni pamoja na kuzingatia afya yake na mtoto au familia kwa ujumla. Sambamba na hilo, mtafiti amebaini kuwa umuhimu wa kuwa na afya njema kunasaidia sana katika utendaji wa kazi ulio imara. Mtafiti ameshauri kuwa katika jamii zetu za Kiafrika wanawake wanahitajika waendelee kufanya juhudi ya kusoma fani ya utabibu (udaktari) ili waweze kupunguza tatizo sugu la madaktari wanawake. Wakiweza kufanikiwa hilo kwa kiwango cha juu zaidi wataweza kunusuru maisha ya kina mama na watoto walio wengi katika jamii zetu na wataachana na tabia ya utegemezi kwa wanaume jambo ambalo linaendelea kusumbua hadi sasa kwa kiwango fulani.

### 4.6.5 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Huruma na Imani Thabiti

Kuwa na Huruma na Imani Thabiti ni jambo linalohitajika na kila binaadamu na kwa kila kiumbe. Kuachana na tabia ya unafiki, chuki, choyo. Tamaa na mfano wa hayo si katika tabia njema na ni vikwazo vya ujenzi wa jamii imara na yenye mafanikio. Katika kulijadili hilo, mtafiti amebaini usawiri wa mwanamke katika suala zima la kumuhusisha mwanamke na tabia njema ya Huruma na Imani thabiti

kwa wanaadamu wenzake na viumbe vyenginevyo. Mtafiti kupitia data alizozikusanya amebaini tabia njema ya kuwa na Huruma na Imani thabiti kupitia kwa Mwavile ambaye aliwaombea kheri ndugu zake wende zao salama na wawe wenye kufanikiwa katika safari yao ya kutafuta maisha yenye mafanikio huko Ulaya. Mwandishi anasema:

> "Mwavile alitamka huku sauti imejaa kilio kisicho na machozi, 'mimi nakutakieni kila la heri Tambo. Sina kinyongo na nyinyi ndugu zangu. Mwende kwa furaha mrudi kwa furaha. Siku moja tutakutana tu. Inshalla mtabarikiwa katika madhumuni yenu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Nitaomba dua kila siku mbarikiwe na mfanikiwe huko mwendako. Mambo yakizidi hapa petu nyinyi ndio mtakaotunyooshea mikono kutuopoa. Nina hakika kwamba huko mnakokwenda mtavuna mengi kuja kutugawia sisi hapa. Sisi na nchi yetu. Hakuna mwanzo lisilokuwa na mwisho. Nenda Tambo kwa radhi zangu na radhi za mamako….." (Uk. 7)

Bilashaka, mtafiti ameweka wazi usawiri wa imani na huruma thabiti ya Mwavile kwa Tambo na kuwaombea mafanikio mazuri ndugu zake ili waweze kufanikiwa katika maisha yao kwa kuwa kufanikiwa kwao ndio kufanikiwa kwake na nchi kwa ujumla.

Kwa upande wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mtafiti amekuwa akisisitiza na kuunga mkono imani kubwa aliyonayo mwanamke katika familia. Huruma na imani thabiti ya mwanamke ina nafasi kubwa ya kujenga Mapenzi, Umoja na Mashirikiano. Kama hiyo haitoshi mwanamke kuwa na huruma na imani thabiti kunamfanya mwanamke huyo awe nguzo muhimu katika kubadili na kuigwa na wale ambao hasira, chuki, hamaki, ugomvi na ushari umechukua nafasi katika maisha yao.

### 4.6.6 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Msimamo Thabiti

Kuwa na msimamo thabiti katika kutetea au kusimamia jambo la msingi na lenye

faida ni suala linaloungwa mkono na umma wowote unaohitaji kusonga mbele kimaendeleo. Msimamo thabiti ni hazina inayosaidia kuondokana na udhalilishaji, unyanyasaji, ubaguzi na mfano wa matendo hayo ambao hutumiwa na baadhi ya watu kwa watu wengine. Katika hali hiyo, mtafiti amedhihirisha usawiri wa mwanamke kupitia dhamira hiyo. Usawiri huo umejitokeza kupitia kwa mwanamke ambaye ni Bi Chani aliyesimama kidete pamoja na uzee wake pasi na kutetereka kutetea haki yake ya shamba ambalo alitakiwa kudhulumiwa na wale wenye nguvu (waheshimiwa na serekali) kule mahakamani. Mwandishi anasema:

> "… Miaka kumi na tatu nilikuwa nikipanda na kushuka kizimbani, mahakamani kuhami shamba letu lililochukuliwa na mheshimiwa… Kesi ilirefushwa kila siku… Mara leo mara kesho… Mara mwezi ujao mara mwezi unaofuatia ujao…… Baada ya ule ukwenzi ulioleta ukimya wa ajabu pale penye ukumbi wa mahakama, alionekana kwa ukaidi na maumivu makubwa akiinuka pale kwenye kiti cha ulemavu alipokuwa kaketi. Huyo, polepole alisimama. Hatimaye akasimama wima ingawa mgongo wake umepinda Akainua kichwa chake na kumtazama hakimu kwa muda, hakimu ambaye alikuwa kamtolea macho yeye kwa mshangao mkubwa ……''Ho, kwanza Bwana Hakimu, nataka kusema maneno machache kabla ya uamuzi wako… Lazima iruhusiwe leo, Hakimu, wakati wa ruhusa umeshafika … Ninachotaka kusema ni kwamba hakuna tena kuomba ruhusa … Hakuna tena kuogopa … Hakuna tena kusita …' alipasuka na kufululiza Bi Chani. Ukumbi wote uliokuwa umenyamaza alilipuka…. " Wacha tuseme kama mnavyosema nyinyi… Sheria za ukoloni mnazoziendeleza zibadilisheni. Sheria za ruhusa zisiwepo tena tunapodai haki zetu……Kabla Tambo hajajua kilichokuwa kikiendelea, alihisi uzito wa mamake Bi Chani aliyekuwa akiporomoka na kuelekea kuanguka. Imara alimshika mamake kabla hajaanguka chini. Hapohapo ilitamkwa kwamba Bi Chani amefariki. Siku hiyohiyo mahakama iliamua kwamba mashamba na ardhi zote zilizochukuliwa na waheshimiwa na serekali yarejeshwe kwa wananchi wanaomiliki ardhi hizo. Siku zilizofuatia matokeo haya, kulikuwa na furaha nchi nzima. Watu walijua kwamba huo ulikuwa tu mwanzo wa ushindi wa vita vyao vya kupigania haki kwa wote" (Uk. 208 - 213)

Kwa muhtasari, data zilizokusanywa na mtafiti zimetoa sura kamili ya juhudi walizonazo baadhi ya wanawake katika kutetea haki zao na kudhihirisha misimamo

yao ya dhati katika kutetea maslahi binafsi na ya jamii kwa ujumla kutoka katika dhulma, unyanyasaji, udhalilishaji, utabaka na baadhi ya maovu mengineyo mfano wa hayo. Mifano mengineyo kuhusu usawiri wa mwanamke kuwa muhusika mwenye msimamo ni: (uk. 144, 157 na 167 – 169)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inaendelea kutetea kikamilifu juu ya mwanamke kuwa na msimamo thabiti katika kusimamia haki zake na wale ambao wanawajibika juu yake. Mtafiti kupitia data zilizokusanywa anaona kuwa thamani mojawapo kubwa ya mwanamke ni kujitambua na kuweza kuwa na msimamo sahihi juu ya haki zake na familia yake au nafasi ya uongozi aliyonayo. Hii itamjenga kufikia hatua kubwa ya maendeleo kwa jamii zetu za kiafrika na duniani kwa ujumla.

### 4.6.7 Mwanamke kama muhusika Mwanamabadiliko / Mageuzi.

Mabadiliko / Mageuzi / Mapinduzi ni jambo la msingi katika jamii ilioza kwa hali isiyo njema (hali ya upotofu) kuelekea hali iliyo muruwa (hali njema). Kwa minajili hiyo, data zilizokusanywa na mtafiti zinaweka wazi usawiri wa mwanamke kama ni muhusika Mwanamabadiliko/ Mageuzi. Mfano mzuri ni kupitia kwa muhusika Bi Chani ambaye alikuwa na mwamko mkubwa wa kuleta mageuzi katika jamii yake. Mwandishi anasema:

> "… Kila siku Bi Chani alipoona yale mabaki ya mwili wa meli yaliyopwelewa, aliuliza swali lile lile zuri analouliza siku zote: Kwa nini watu hulazimishwa kupigana vita visivyowahusu hata kidogo? Kwa nini wanakubali kumwaga damu na kupoteza roho zao kwa faida ya watu wengine? Kwa nini wanakubali kupiganishwa? Kwa nini wakishapiganishwa hawapati chochote ila kubakishiwa mabaki ya uchafu na sumu inayowapa jaka moyo?" (uk 65)

Data zilizokusanywa na mtafiti zimedhihirisha kuwa, maswali ya msingi anayouliza Bi Chani yamelenga kuleta mwamko wa mabadiliko / mageuzi / mapinduzi / ukombozi kwa jamii ambayo imejaa ukandamizaji, udhalilishaji, ukatili na mauaji. Bi Chani anahuzunishwa na kupinga vikali tabia hii ya maonevu kwa watu wa tabaka la chini na kuitaka jamii iamke na kusimamia upatikanaji wa haki sawa kwa wote.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa upande mwengine inawataka wanawake kuungana katika kufanya mabadiliko / mageuzi katika mambo ambayo hayakubaliki katika jamii zetu za Kiafrika. Mtafiti anaona kuwa pamoja na kwamba nchi zote za Kiafrika zimekuwa huru na waafrika wenyewe ndio watawala lakini bado mfumo na maendeleo ya nchi hizo ni dhaifu. Kwa misingi hiyo mtafiti anaona kuwa wanawake wakishirikiana na wanaume wana nafasi kubwa ya kuleta mapinduzi kwa wale viongozi wasio watendaji wazuri serekalini na kwenye mashirika au taasisi nyenginezo.

### 4.6.8 Mwanamke Kama Muhusika Mlezi wa Familiya

Uzazi na baadae ulezi ni katika mambo magumu kwa mwanamke au kwa mzazi na mlezi yeyote. Ulezi unahitaji matunzo na usimamizi mzuri, mapenzi na maadili mazuri kwa mtoto au watoto. Mwanamke ana nafasi kubwa na ni nambari moja katika malezi ya watoto na familiya ingawaje hata mwanamme ni msimamizi muhimu katika familiya hiyo husika. Utafiti huu umebaini juhudi kubwa za Bi Chani katika ulezi wa familiya yake ya watoto wake wa kuwazaa nane na mmoja (Mwavile) wa kulea kwa mapenzi huruma na matunzo. Mwandishi anafafanua:

> “Kabla wengine hawajaondoka, kulikuwa na Abuu, Salila, Yasir, Jokha, Sele (Msurupwete kwa jina jingine la utani), Zahran, Samira na

> Tambo. Hawa wote walikuwa watoto wa Bi Chani na Bwana Mansour. Watoto wanane. Bi Chani alikuwa na mbegu nzuri tumboni. Si haba! Na Mwavile bila ya shaka , mtoto wao wa tisa, lakini ni mtoto wa Bi Chani wa kulea. Mbali na Mwavile, wote wengine walikuwa hawapo, isipokuwa Tambo ambaye karudi nyumbani muda mrefu uliopita…… ” (Uk. 134)

Kwa upande wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inamuona Mwanamke kuwa bado ni mtu muhimu mno katika malezi ya watoto na familiya. Usimamizi, malezi na matunzo mazuri ya familiya yatasaidia sana kuleta tija kwa Jamii husika. Hivyo basi ni vyema Jamii ikaendelea kuwapa heshima yao wazazi kwa malezi bora ya familiya zetu.

### 4.6.9 Mwanamke Kama Muhusika Yatima Anayehitaji Msaada

Kuwa yatima ni jambo linalotia huzuni na simanzi kwa yeyote. Kuwa yatima ni kuondokewa au kufariki kwa wazazi wa mtoto huyo. Mwanadamu yeyote wazazi wake wanapokufa mwanadamu huyo hukosa muelekeo wa hali ya juu na hubaki katika majonzi makubwa. Wazazi ndio msaada mkubwa kwa mtoto katika kumjenga mtoto huyo katika misingi mema na yenye tija kimalezi. Katika utafiti huu, mtafiti ameweza kugundua uyatima wa mwanamke ambaye ni Mwavile. Mwavile alikuwa mwanamke ambaye wazazi wake walifariki wakati yeye akiwa ni mdogo na baadaye kuchukuliwa na mjomba wake na baadaye kupelekwa kwa Bwana Mansour na mkewe Bi Chani kwa lengo la kulelewa na kusaidia kazi za nyumba. Mwandishi anasema:

> “Mwavile alikuwa mtoto mdogo ambaye hakuwahi kumwona babake na mamake. Tokea kuzaliwa kwake alihamishiwa kwa mjomba wake alikochukuliwa kulelewa baada ya kufa wazazi wake wakati nyumba yao ilipopigwa na radi, na yeye akanusurika kufa kwa miujiza ya Mungu. Kwa sababu ya tamaa ya pesa Mwavile alipelekwa kwa

> Bwana Mansouri na Bi Chani kulelewa na kusaidia kazi za nyumba. Mpaka leo amebakia humo nyumbani mwao? Aende wapi naye kaganda na kugonga ukuta? Ndiyo majaaliwa yake" (Uk. 152)

Kwa hakika data hizi zinaweka wazi juhudi kubwa ya Bwana Mansour na Bi Chani kwa kumlea Mwavile kwa uwezo na juhudi zao zote na kumfanya kama mtoto wao wa kumzaa sawa na watoto wao nane ambao ni: Abuu, Salila, Yasir, Jokha, Sele Msulupwete, Zahran, Samira na Tambo.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni mwalimu mkubwa katika kuelezea uhalisia wa wanawake katika jamii zetu za Kiafrika. Baadhi ya familia au jamii, wanawake wameachwa pasipo na msaada wa makusudi. Kwa mfano wengine wameachwa na kuwa wajane kwa sababu zisizo za msingi. Mtafiti anaona kuwa wanawake wamekuwa na ulezi mkuwa wao binafsi na watoto pasi na msaada kutoka kwa wanaume. Kama hiyo haitoshi, wanawake walio wengi ni mayatima kwa kuwa wazazi wao wamewatelekeza kwa sababu tofauti ikiwemo ukewenza au matunzo, ugumu wa maisha, vifo na kutengana kwa sababu ya siasa au dini. Kwa msingi huo mtafiti anaitaka jamii ibadilike na iwaone wanawake ni watu muhimu na wanaohitaji msaada wa kila hali kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla.

### 4.6.10 Mwanamke Kama Muhusika Msamehevu

Kwa hakika kusamehe au kusameheana ni jambo kubwa kwa binaadamu yeyote. Kusameheana kunajenga upendo, masikilizano, ushirikiano na kusaidiana. Kusameheana kunamwepusha mwanaadamu na chuki, husda, choyo, ubinafsi, tamaa, kiburi nk. Suala la kusamehe au kusameheana lina nafasi kubwa katika kujenga jamii

yenye umoja na mashirikiano ambayo ni mojawapo wa silaha madhubuti ya kuleta maendeleo.

Katika kulijadili hilo, mtafiti kupitia usawiri wa mwanamke, amemtumia muhusika Bi Chani ambaye alimsamehe mwanawe Jokha aliyepingana naye na kumdharau mama yake Bi Chani baada ya Bi Chani kumkataza asiolewe na Bwana Mzima. Baadaye Jokha alimtukana na kumdharau mama yake na kuolewa na Mzima. Mwisho wake Jokha alikuwa akipigwa, akidhalilishwa, na kuonewa na mumewe Mzima. Baada ya kutokea hayo, Jokha aliamuwa kwenda kwa mama yake kumuomba amsamehe na mama huyo akakubali kumsamehe kwa ukamilifu. Mwandishi anasema:

> "Mama, nakushika miguu, alianza kuangua lio jengine. Nisamehe mamangu. Ulinambia nikakukana. Ulinambia asiyesikia la mkuu huvunja guu, na sasa kweli nimevunjika guu. Nimevunjwa guu na adui yetu ambaye alikuwa mpenzi wangu. Aaa – a ama kweli: Mchamago hanyele huja akawia papo… Majuto mjukuu kweli huja mwishoni! Nisamehe mama. Nimesafiri mamia ya kilomita kuja kukuomba radhi. Najua kwamba pepo ya mwana imo miguuni mwa mama. Hayo ni maneno ya kitabu cha Mwenyezi Mungu. Mwanzoni sikujua, lakini sasa nimetambua…….Ghafla, Bi Chani akafurukutafurukuta. Akageuza uso wake kumtazama yule aliyekuwa akisema ndani ya kilio. Midomo yake ya kibogoyo ikaonesha tabasamu nyepesi. Akasema, Nani? Nani wewe? Jokha? Umekuja? Nenda kanipikie uji. Mama mwadilifu hamtupi mwanawe" (Uk. 186 - 187)

Kwa ujumla data hizi zimedhihirisha jinsi mwanadamu anapotambua makosa yake analazimika afanye haraka kuomba radhi (kuomba msamaha). Dhana hii humjenga mwanaadamu kuweza kubadilika na kutokurejea tena makosa hayo.

Tukirejelea Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mtafiti ameona kuwa jamii za Kiafirika bado zina nafasi kubwa ya kusameheana kwa matendo ambayo wanaadamu

huyafanya hususan watenda makosa hayo wanapokubali kuwa wametenda makosa na baadae kuomba msamaha na kuahidi kutorejea tena makosa hayo. Mtafiti anaona kuwa wanawake nao ni binaadamu na kila binaadamu ana udhaifu wake na hutenda makosa ama yawe ya kukusudia au yasiyo ya kukusudia. Mtafiti anawashauri wanawake na wanadamu wote waishi kwa kusameheana ili kujenga mapenzi zaidi baina yao.

### 4.6.11 Mwanamke Kama Muhusika Msomi (Mwenye Elimu)

Elimu ni mabadiliko ya tabia yanayotokana na ujuzi. “Elimu ni ufunguo wa maisha”, “Elimu ni hazina”. Elimu ni msingi nambari moja katika kujenga jamii yenye wataalamu na mafanikio makubwa kwa jamii au taifa lolote duniani. Maendeleo ya taifa lolote hutegemea juhudi za wataalamu ambao ndio wasomi katika fani husika. Elimu humuongoza mwanadamu kuwa mwema kwa kutenda yanayostahiki na kuacha yasiyostahiki kwa mujibu wa elimu na dini husika. Dini zote humtaka mwanaadamu asome ili aweze kutenda ibada zake kisomi (kielimu).

Katika utafiti huu, data zilizokusanywa zimeweka wazi usawiri wa mwanamke kuwa ni msomi baada ya yeye kufanya juhudi katika masomo na kuweza kuitumia elimu yake vyema. Kwa kuzingatia hilo mtafiti amebaini wahusika mbalimbali ambao walifanya juhudi ya kutafuta elimu wakiwemo wahusika wanawake. Miongoni mwa wahusika hao ni pamoja na Bi Chani, Mwavile na Samira. Mwandishi ametutolea mfano mmoja wapo kupitia Samira.

> “Samira alibakia Australia wakati kaka na ndugu zake walipomueleza kuwa wanarudi nyumbani. Huko Samira alishika uprofesa wa somo la Media na Information Technology katika Chuo Kikuu kimoja cha

> Sydney. Lakini vuguvugu la mabadiliko lilipopamba moto katika Visiwa vya Viungo, Zahran na Tambo walimwomba arudi kuja kuwasaidia katika shughuli za itikadi na uenezi." (uk 200)

Kwa upande mwengine hata Bi Chani alikuwa na elimu aliyoweza kuitumia vyema kwa kuusia, kutetea na kuelekeza na kuwafunza wanawe katika mfumo mzima wa maisha sahihi. Bi Chani alifanya juhudi katika masomo tangu akiwa mdogo na kupata mafanikio makubwa. Mwandishi anafafanua:

> "Tambo alikuwa mtupu katika fikra hizi za kila siku, fikra mbichi zinazotoja damu. Kila siku Tambo alishangaa kwamba bibi huyu mkongwe aliyejisomesha mwenyewe ndani ya miaka mingi amefikia kiwango hiki cha ujuzi. Na yeye? Yeye anajaribu, lakini hajafikia hata robo ya upeo huo. Ingawa alizimeza taarifa na fikra zote hizo anazozitoa mamake, mpaka sasa kashindwa kuzifikisha maanani. Maana kila siku ina utata…" (Uk. 54)

Kwa hakika mtafiti amegundua kuwa suala la elimu lina nafasi kubwa katika jamii, si kwa wanawake tu bali hata wanaume au jamii kwa ujumla. Hii ni kwa sababu Elimu ni nuru na ni ufunguo wa maisha yaliyotukuka.

Kwa msaada wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mtafiti amegundua wanawake walio wengi wanaendelea kuamka na kutoa msukumo mkubwa katika kutafuta elimu. Elimu tangu zamani hadi sasa imeonekana ni silaha yakinifu yakumuokoa mwanamke dhidi ya ujinga, uzembe, utegemezi mkubwa kwa mwanamme nk. Wanawake waliowengi wamebadilika na sasa wamekuwa wasomi wakubwa na wenye uwezo mkubwa katika fani mbalimbali kama Ualimu, Udaktari, Biashara, Uhasibu, Uongozi nk. Hii imewafanya waweze kujiamini na kuwa viongozi bora katika mataifa mbalimbali.

### 4.6.12 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni miongoni mwa hazina muhimu katika kujenga familia bora, jamii au taifa kwa ujumla. Katika jamii yeyote endapo raia wake watakuwa wanaishi pasi na kuwa na mapenzi ya dhati basi kwa hakika amani, utulivu , maelewano , umoja na mashirikiano yatakuwa ni yenye kukosekana na jamii hiyo itakumbwa na ukame wa hali ya juu kimaendeleo. Katika kulifafanua hilo. Utafiti huu umebaini usawiri wa mwanamke katika mapenzi ya dhati katika familiya na hata katika ndoa. Mfano mmojawapo ni mapenzi ya dhati baina ya Mwavile na Tambo tangu kabla hawajaoana, hadi mwisho wakaoana. Katika ndoa yao mwandishi anasema:

> "Mapenzi na shauku ya Mwavile na Tambo ilibidi yafunuke. Kila mmoja alikuwa akimtazama mwenzake kwa mbali na woga. Kila mmoja alimpenda mwenzake kuliko kitu chochote. Kila mmoja alikuwa amejaa shauku kubwa ya kuwa na mwenzake kwa daima na milele. Lakini haikuwa rahisi kutamka nia zao katika miaka yote waliyokuwa wanatafutana katika mapenzi ya udugu. Nani angeanza na nani angemaliza? Baada ya kupita mwaka unusu wa ushindi wa marehemu Bi Chani, Tambo ndiye aliyeamua kuanza'Mwavile, mimi nataka uwe wangu wa milele,' alitamka Tambo huku akimtazama Mwavile machoni mwake moja kwa moja" ….. "Ghafla Mwavile alinyoosha mkono kuukamata mkono wa Tambo. Kisha aliunyanyua mkono wa Tambo akauweka kifuani pake pale penye moyo wake, uliokuwa ukidunda mbiombio. Kisha akasema 'Nani mwengine ambaye ningemtaka kama si wewe? Nani kuliko wewe?'"…."Arusi ya Mwavile na Tambo ilifanywa miezi mitatu iliyopita . Kwa ajabu ya kila arusi hii ilichanganyika na arusi ya Janet na Sele Msulupwete… Arusi mbili hizo zilihudhuriwa na ndugu na marafiki ili kuwahongera maarusi hao" (uk.214 - 215)

Uchambuzi wa dondoo hii unaweka wazi utafiti huu, juu ya usawiri wa mwanamke katika mapenzi ya dhati ambayo ndio raslimali muhimu katika jamii zetu.

Mtafiti kupitia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, anaamini kuwa, nadharia hii inafaa sana katika kuchambua mchango mkubwa wa wanawake katika kudumisha

mapenzi ya dhati. Mtafiti ameiona nadharia kuwa mwanamke mwema huwa mwema hata katika mapenzi yake iwe kwa mumewe, watoto, familia na jamii kwa ujumla. Nadharia inawataka wanawake wadumishe mapenzi ya dhati kwa wale wanaostahiki kwao na sio vyenginevyo ili kuweza kujenga jamii ilio imara na yenye maelewano muruwa.

### 4.6.13 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe Kwa Mwanamme

Chombo cha starehe ni hali ya kutumika kwa binaadamu kama bidhaa au kutoa huduma ya kuwaridhisha wanaadamu wengineo. Baadhi ya wanawake hutumika kama bidhaa au chombo cha kustarehewa na wanaume. Baadhi ya wanaume wamekuwa wakiwaona wanawake wanaweza kumaliza kiu yao hasa katika masuala ya mapenzi. Kwa maana hiyo ni wanaume hususan wale wenye uwezo huweza kudhibiti wanawake walio wengi ili waweze kutimiza kiu yao. Kwa upande wa utafiti huu mtafiti amegundua kuwa usawiri wa mwanamke kama chombo cha starehe umejitokeza kupitia kwa Bwana Toba kuwatumia wake zake pamoja na masuria wake. Mwandishi anafafanua:

> “Mamake yeye Mansour aliyeitwa Badria, alikuwa miongoni mwa wake zake wane wa Kiarabu. Bi Badria alikuwa na wivu mkali kwa mume wake Bwana Toba kwa vile alikuwa mke wa mwanzo wa bwana huyo. Seuze Masuria waliokuja kurukia ndoa za mabanati wa peponi kama walivyoitwa na watu wengine. Majina ya wake wengine wa Bwana Toba yalikuwa Alwiya, Ruqaiya na Fat-hiya. Masuria wao kwa pamoja walibandikwa jina la vijakazi …..“Majina ya hao Masuria watatu yalikuwa Mwanamvua, Mwanaleo na Mwanakujua. Majina ambayo yalileta tofauti na dharau kubwa ya utambulisho kati ya mwanamke katika misingi ya taasisi ya ndoa ya kugawana mume. Tofauti na dharau kati ya mabibiye na wahudumu walioletwa kushiriki mwili wa bwana Toba na kufanya kazi chafu za nyumba. Lakini wake wa Bwana Toba kazi yao kubwa ilikuwa kumfurahisha mume wao kwa kupakwa hina mikononi na miguuni, kurembwa wanja kopeni, kuvishwa nguo za hariri na kujipamba vyombo vya

> dhahabu. Hasa pete, herini na bangili za dhahabu walizovaa kochokocho" (uk.112 - 113)

Mtafiti kupitia nukuu hiyo imeweka wazi tabia ya baadhi ya wanaume au waume kuoa wake wengi na baadae kuwatumia kama chombo cha kustarehe. Sambamba na hilo wale waume wenye uwezo kimali hutafuta pia Masuria na kuwatumikisha kwa maslahi binafsi kama tunavyomuona Bwana Toba. Tabia hii haipendezi na si vyema ikaungwa mkono. Mwanamke naye ni binaadamu ana haki zake na anatakiwa aheshimiwe, athaminike na atunzwe. Vilevile kwa upande wa wanawake wenyewe wanalazimika kujua nafasi yao na thamani yao ili waweze kusimama imara kutetea nafasi hizo.

Kwa upande wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, inapinga vikali mwanamke kutumika kama bidhaa hususan kwa mwanamme. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa bado kuna baadhi ya wanawake hususan katika jamii za Kiafrika hutumika kama bidhaa kwa wanaume. Wanawake wengine hutumika kama bidhaa au chombo cha starehe kwa sababu mbalimbali ikiwemo tama au hali duni ya kimaisha. Mtafiti ameona kuwa hali hii haistahiki kwa wanawake na ni vyema wanawake hao wakajitambua thamani yao na wakaachana nayo na kujiona wao ni watu ambao wana nafasi kubwa kwa maendeleo ya jamii husika na Afrika kwa ujumla.

### 4.6.14 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi

Tamaa, Jeuri na Kiburi ni katika tabia mbaya mno kwa binaadamu na binaadamu mwenye tabia hizo anahitajika kuachana na kuishi kuwa na tabia njema. Msingi mzuri wa maisha sehemu yeyote ni kuwa na tabia nzuri / njema ambazo zitaleta faida

katika familiya na jamii kwa ujumla. Tabia hizi mbaya (Tamaa, Jeuri na Kiburi) huweza kumponza mwanaadamu na kumweka katika hasara au majanga makubwa. Hivyo basi ni vyema kwa kila mwanajamii kuziepuka.

Katika utafiti huu, data zilizokusanywa na mtafiti zimebaini kuwa baadhi ya wanawake wana tabia hizo mbaya na hivyo mwisho wa majuto ni mjukuu. Mtafiti kupitia mwanadishi anaweka wazi hilo kupitia Jokha na Salila. Kwa mfano mwandishi anasema kupitia Salila kama ifuatavyo:

> "Kweli unayoyasema Mwavile. Mimi niligombana na wazazi wangu kwa kutaka kuolewa na mwanamume ambaye ana cheo kikubwa na utajiri usiokuwa na mipaka kwa viwango vya huku kwetu. Lakini ndoa yetu imefikia wapi? Mimi sina furaha na sidhani kama yeye mume wangu ana furaha…" (Uk.165)

Kwa upande mwengine majadiliano ya Mwavile na Salila yamedhihirisha chuki, kiburi na tamaa ya Salila kuhusu kuuzwa kwa shamba la Bi Chani kwa rafiki muengereza wa mume wa Salila ambaye ni Mabruki. Mwandishi anasema:

> "Lakini Salila, si unajua kwamba bibiye alipigana mwisho wa kupigana shamba hili lilipochukuliwa na bwana mkubwa mmoja mwenye nguvu?
>
> Najua
>
> Kwa nini basi unataka shamba lichukuliwe tena leo baada ya Bi Chani kulitia mikononi hatimaye?
> Sio lichukuliwe. Nasema linunuliwe. Liuzwe kila mtu apate haki yake na kila mtu apumzike
>
> Liuzwe bila idhini ya mwenye shamba, ambaye yu hai hajafa. Tutamrithije mtu ambaye hajafa?
> Hajafa kama kesha kufa. Hivyo alivyo ana uhai gani?
>
> Ni kweli amepoteza fahamu, lakini hajapoteza akili. Fahamu zake zinapanda na kushuka
> Aaaa, mimi sitakuwa radhi na wala sitaingia katika uovu huo" (Uk. 168)

Kwa hakika data na dondoo hizo zimeweka bayana dhana nzima ya Tamaa, Jeuri na Kiburi cha Salila kufikia kulazimisha kuuzwa hata shamba la mama yao kwa maslahi ya wachache na kwa kumridhisha mumewe. Jambo hili halikustahiki kufanywa na Salila na wale wenye tabia kama za Salila.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inaendelea kuwataka wanawake watambue kuwa, matendo maovu kama Tamaa, Jeuri na Kiburi hayana nafasi kwao na hata kwa wanaume. Mtafiti anawatahadharisha wanawake hususan wa Kiafrika kuwa tamaa, jeuri na kiburi sio mtaji kwao na wala sio mtaji kwa maendeleo ya taifa lolote Afrika au kwengineko. Kwa misingi hiyo ni vyema kwa wanawake hao kuepuka tabia hizo za Jeuri, Kiburi na Tamaa na kubaki katika tabia njema.

Kwa hakika maelezo ya uwasilishaji na uchambuzi yaliyotangulia kuhusu riwaya ya *Kamwe si mbali tena* yamedhihirisha kikamilifu kiu ya kujibu suala la msingi la kwanza ambalo ni: *Ni kwa vipi usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule ya Utengano na Kamwe si mbali tena?* Sambamba na swali hilo imeenda pamoja na lango mahsusi la kwanza la utafiti huu lisemalo: Kufafanua usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Hivyo basi mtafiti kupitia data alizokusanya ameona kuwa mwanamke amejidhihirisha kuwa na tabia za aina mbili ambazo ni: Tabia njema (chanya) na tabia mbaya (hasi). Kwa misingi hiyo wanawake sawa na wanaume wana lazima au wajibu wa kujitahidi katika tabia njema na kuachana na tabia mbaya. Hii ni pamoja na kwa kuhusisha na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

**Jadwali 4.2: Muhtasari wa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Kamwe Si Mbali Tena**

| Na. | **Usawiri wa Mwanamke katika Kamwe si mbali tena** |
|---|---|
| 01 | Mwanamke kama muhusika Muwajibikaji (Mwenye bidii katika kazi) |
| 02 | Mwanamke kama muhusika Mtambuzi na Mwanahistoria |
| 03 | Mwanamke kama muhusika Mpenda Dini |
| 04 | Mwanamke kama muhusika Tabibu/daktari wa kienyeji |
| 05 | Mwanamke kama muhusika mwenye Huruma na Imani thabiti |
| 06 | Mwanamke kama muhusika mwenye Msimamo thabiti |
| 07 | Mwanamke kama muhusika Mwanamabadiliko / Mageuzi |
| 08 | Mwanamke kama muhusika Mlezi wa familiya |
| 09 | Mwanamke kama muhusika Yatima anayehitaji msaada |
| 10 | Mwanamke kama muhusika Msamehevu |
| 11 | Mwanamke kama muhusika Msomi (mwenye elimu) |
| 12 | Mwanamke kama muhusika mwenye Mapenzi ya dhati |
| 13 | Mwanamke kama muhusika Chombo cha starehe kwa mwanamme |
| 14 | Mwanamke kama muhusika mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi |

Chanzo: Data kutoka riwaya ya Kamwe si mbali tena, 2016

## 4.7 Kufanana Kwa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya Teule ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena

Kwa haki zaidi baada ya kusoma, kuchunguza kwa kina, kutathmini na kuchambua riwaya hizi mbili za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena,* mtafiti amebaini kuwa pamoja na kwamba riwaya hizi zimetungwa na kupishana kwa tofauti ya miaka thelathini na nne (34) yaani riwaya ya *Utengano* imetungwa mwaka (1980) ikiwa ni miongoni mwa riwaya za mwanzo za mwandishi baada ile ya *Asali Chungu (1977) na Dunia Mti mkavu (1980)* na kwa upande mwengine riwaya ya *Kamwe si mbali tena* imetungwa mwaka (2014) ikiwa ni miongoni mwa riwaya mpya baada ile ya *Mhanga nafsi yangu (2012) na Mkamandume (2013).*

Mtafiti amebaini kuwa riwaya hizi mbili zina baadhi ya mambo ambayo yanafanana ingawa kwa kiasi kidogo (wastani wa asilimia thelathini). Kwa kuwa mtafiti

ametathmini kuhusu mwanamke, utafiti huu umekusudia kuchambua kulingana (kufanana) kwa usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Uchambuzi huu umeongozwa na swali la msingi la pili lifuatalo.

iii) Ni kwa namna gani usawiri wa mwanamke umefanana katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

Kwa hakika swali hilo la msingi la pili limekwenda sambamba na lengo mahsusi la pili la utafiti huu lisemalo: Kufananisha usawiri wa mwanamke katika riwaya teule ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Hivyo basi uchambuzi huu utadhihirisha mfanano huo wa usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* kwa kuhusisha na Nadharia ya Fasihi Linganishi. Nadharia ya Fasihi Linganishi imetumika ikiwa ni msaada muhimu wa kushadidia mfanano uliopo baina ya riwaya hizo teule kama ifuatavyo:

### 4.7.1 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati kama ambavyo mtafiti alivyokwishaieleza imethibitisha kuwa ni jambo muhimu katika kujenga familia bora. Kwa misingi hiyo usawiri wa mwanamke kama muhusika mwenye mapenzi ya dhati umeonekana kufanana vyema na kujitokeza katika riwaya zote mbili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano* tumeona mapenzi ya dhati baina Maimuna na Kabi ambao mwishowe walioana bila ya kujali mapungufu ya kila mmoja na kuishi kwa raha huko Hitama (uk. 162 na 171) wa riwaya ya *Utengano* na baadae kujishughulisha na kilimo.

Sambamba na hilo, mapenzi ya dhati yamejitokeza katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* kupitia wapendanao wawili ambao ni Tambo na Mwavile. Mwavile alimpenda

sana Tambo na kuhitaji amuoe ili wawe mke na mume ingawaje aliyeanza kumtamkia mwenzake mwanzo ni Tambo na mwishowe walioana na kuishi vyema (uk 214 - 215).

Kwa msaada wa Nadharia ya Fasihi Linganishi, imetuelekeza kutambua kuwa dhana ya mapenzi ya dhati bado ni dhana inayoendelea kuchukua nafasi katika maisha yetu ya kila siku. Mapenzi hayakuanza miaka thelathini na nne iliyopita (1980) ya uandishi wa riwaya ya *Utengano* na wala (2014) katika uandishi wa *Kamwe Si Mbali Tena* au sasa (2016) sio ukomo wa mapenzi. Kwa mnasaba huo mtafiti kupitia mwandishi amelinganisha mapenzi ya awali na mapenzi ya sasa bado yana nafasi kubwa na yanastahiki kuenziwa kwa wapendanao kwa uhalali kwa lengo la kudumisha upendo, masikilizano, huruma, usamehevu, uvumilivu na ujenzi wa familiya bora hususan katika ndoa.

### 4.7.2 Mwanamke ni Muhusika Mwenye Msimamo Thabiti

Kwa hakika kuwa na msimamo thabiti ni jambo la maana na la umuhimu katika kusimamia haki na kupinga batili. Msimamo unahitajika kwa wote si kwa wanawake pekee bali hata wanaume. Katika utafiti huu mtafiti amebaini mfanano wa dhana ya mwanamke kuwa ni muhusika mwenye msimamo thabiti katika riwaya zote mbili teule kama alivyokwisha elezwa hapo juu. Kwa mfano katika riwaya ya *Utengano*, mtafiti amebainisha msimamo thabiti kupitia kwa muhusika Maimuna, baada ya kusingiziwa kuwa ameiba na kuitwa mwizi aliamua kuweka msimamo wa kuhama Pumziko na kuelekea Bobea kwa Biti Sururu ambapo aliamini kutakuwa ni salama kwake kama alivyoshauriwa na kuombwa na rafiki yake Dora. Mwandishi anaweka

wazi hilo (Uk 83 - 84). Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe si mbali tena,* usawiri wa mwanamke kuwa ni muhusika mwenye msimamo thabiti umejidhihirisha wazi kupitia kwa Bi Chani aliyesimama kidete pamoja na uzee wake pasi na kutetereka kutetea haki yake ya shamba ambalo alitakiwa kudhulumiwa na wale wenye nguvu (waheshimiwa na serekali) kule mahakamani (uk. 208 - 213)

Nadharia ya Fasihi Linganishi imeweka wazi kuchambua kufanana kwa dhana hii ya mwanamke kuwa na msimamo thabiti ikionesha juhudi zinazoendelezwa na baadhi ya wanawake katika kutetea haki zao na kupinga kudhulumiwa na kudhalilishwa. Wanawake kupitia riwaya hizi mbili teule wamekuwa wakipigania haki zao tangu kabla ya miaka themanini (1980) yaani kabla ya uhuru kwa nchi ya Tanzania (1964) au kabla ya karne ya ishirini (20) na hata sasa (2016) ambapo ni karne ya ishirini na moja (21). Kwa ujumla riwaya zote mbili teule zimesadifu juu ya dhana ya msimamo thabiti kwa mwanamke. Ni vyema tabia hii ikaendelezwa kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

### 4.7.3 Mwanamke Kama Muhusika Muwajibikaji (Bidii Katika Kazi)

Uwajibikaji ni dira ya mafanikio. Katika jamii yeyote wananchi wanalazimika kufanya kazi kwa bidii kwa lengo la kuleta mapinduzi yenye tija katika jamii husika. Maendeleo hayapatikani kama kutakuwa na watu wavivu na wasojituma ipasavyo. Dhana ya uwajibikaji imeonekana kufanana na kujitokeza katika riwaya zote mbili teule. Kwa mfano katika riwaya ya *Utengano,* mtafiti amebaini juhudi za Bi Farashuu katika biashara ndogondogo ikiwemo kusukuma mikate hadi usiku au vitumbua na ukunga (uk 31).

Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena,* dhana nzima ya uwajibikaji imejitokeza kikamilifu. Baadhi ya wanawake wameonekana sio wavivu na wako mstari wa mbele katika kutimiza majukumu yao vyema ikiwemo kuwahudumia wazazi au walezi wao ipasavyo. Katika riwaya hii, mwandishi amemtumia muhusika Mwavile ambaye alikuwa ni mtoto wa kulea tu kwa Bi Chani. Mwavile aliwajibika vyema na kufanya kazi kwa bidii kubwa ya kumlea, kumuhudumia, kumthamini na kumuenzi mama yake wa kulea Bi Chani kwa mapenzi yake yote huku watoto wake nane wa kuwazaa wa Bi Chani wakiwa wako Ulaya kutafuta maisha mazuri kama wasemavyo. Bila shaka huu ndio wajibu mkubwa wa watoto kwa wazazi au walezi wao ili kupata radhi za M/Mungu (Uk 4 - 6).

Nadharia ya Fasihi Linganishi imetupa fursa adhimu kutathmini mfanano wa riwaya hizi mbili na kuona jinsi zinazofanana kupitia usawiri huu wa mwanamke kuwa ni muwajibikaji (mwenye bidii katika kazi). Pamoja na kwamba riwaya hizi zimetafautiana kwa miaka thelathini na nne, bado zimeonekana zinafanana katika kumsawiri mwanamke katika utimizaji wa majukumu yake vyema kupitia ulezi, matunzo, usimamizi, heshima na thamani kwa wazazi / walezi. Hii ina maana suala hili halina ukomo katika utekelezaji wake. Ni wajibu wa watoto kuendelea katekeleza matunzo bora kwa wazazi/walezi.

### 4.7.4 Mwanamke Kama Muhusika Mlezi wa Familiya

Ulezi mwema wa familiya ni msingi wa familiya bora na kinyume chake ni matatizo makubwa. Ulezi mwema wa familiya unahusisha matunzo, nidhamu na uvumilivu, busara na hekima, heshima na adabu, bidii na uadilifu pamoja na mashirikiano baina

ya pande mbili; mke na mume. Kwa ujumla usawiri huu wa mwanamke umetokea kulingana katika riwaya zote mbili teule. Msingi mkubwa ni kwamba dhana ya malezi kwa familiya imeanzia tangu enzi za mababu na mabibi (enzi za kale). Hivyo basi hadi sasa malezi ya familiya ni kuendeleza jukumu hilo pevu kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto ipasavyo kwa pamoja na sio kwa kumuona na kumtupia mzigo mzito wa ulezi mwanamke peke yake kuwa ndiye mwenye jukumu la kufanya hivyo.

Dhana hii imetokea kulingana katika riwaya zote mbili katika hali tofauti kwa mfano: Kwa upande wa riwaya ya *Utengano* tumeona ulezi wa familiya umemwelemea zaidi mwanamke kuliko mwanamme na kuonekana ndio dhamana wa familiya.

Katika riwaya ya *Utengano,* mtafiti amebaini tabia ya baadhi ya wanaume (waume) kutozijali familiya zao na hawashiriki vyema katika malezi na familiya na hatima yake humuachia mwanamke peke yake. Waume hao katika harakati zao za kimaisha fedha wanazozipata huzitumia kwa kulewa na kushindwa kuwafikiria watoto na wake zao majumbani kwao. Ushahidi ni malalamiko ya Selume kwa mumewe Shoka (uk 112).

Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena,* tumeona kuwa malezi na familiya yamejitokeza kwa mashirikiano na inapotokea mmoja kama mume kufariki jukumu hilo huendelezwa vyema na mwanamke. Mfano mzuri ni kupitia kwa Bi Chani na mumewe Bwana Mansour ambapo walijaaliwa watoto nane na mmoja wa kulea. Utafiti huu umebaini juhudi kubwa za  Bi Chani katika ulezi wa familiya yake ya

watoto wake wa kuwazaa nane na mmoja (Mwavile) wa kulea kwa mapenzi huruma na matunzo (uk 134).

Nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia misingi yake imetusaidia katika kutathmini mfanano wa riwaya hizi mbili kupitia usawiri huu wa mwanamke kuwa ni mlezi wa familiya. Mfanano huu kuhusu ulezi wa familiya unahitajika kwa ukamilifu kupitia pande zote mbili na sio vyenginevyo ili kuimarisha famliya bora na yenye maadili. Kwa ujumla mwanamke ameonekana ndiye mtendaji mkubwa katika malezi ya familiya tangu mtoto huyo hajazaliwa hadi anapozaliwa na kuendelea kulelewa. Hivyo basi mwanamke naye anahitajika kuthaminiwa na kuheshimiwa, kutunzwa na kuenziwa na kupewa msaada wa kila namna ili ajihisi vyema. Tabia hii ya kumjali mwanamke ni vyema ikaendelezwa.

### 4.7.5 Mwanamke Kama Muhusika Tabibu/ Daktari wa Kienyeji

Fani ya Udaktari au utabibu ni muhimu katika maisha ya jamii yeyote. Kuwa daktari au tabibu sio jambo la mzaha, inahitajika uwezo mkubwa wa taaluma katika fani husika ili muhusika aweze kutumika kusaidia na kuokoa maisha ya mwanaadamu na viumbe vyengine. Fani ya udaktari au utabibu wa kienyeji ni ile inayotumia utoaji wa msaada pasi na kutumia hospitali kama kituo cha huduma kilicho rasmi. Tabibu wa kienyeji ana mchango mkubwa katika kusaidia kuokoa maisha ya mwanaadamu lakini kwa kutumia matibabu ya kienyeji kama miti shamba, majani, mizizi, hirizi, dua nk. Mtafiti amebaini kuwa udaktari / utabibu wa kienyeji umefanana na kujitokeza katika riwaya zote mbili. Katika riwaya ya *Utengano* tunamuona Bi Farashuu akiwa tabibu wa kienyeji na kazi yake hasa ni ukunga (kuzalisha

wajawazito) Bi Farashuu alifanikiwa kumsaidia na kumzalisha vyema Bi Tamima akishirikiana na Biti Kocho na watumishi wengine katika jumba la Bwana Maksuudi (uk 34 - 35).

Sambamba na hilo, katika kuzungumzia dhana ya utabibu au udaktari kwa kutumia mitishamba, dua, makobe na hirizi. Kwa kugeukia riwaya ya *Kamwe si mbali tena* utafiti huu umegundua uwezo mkubwa alionao Bi Chani (Warida) katika kutibu wanaadamu ipasavyo. Hii ni kwa sababu elimu ya utabibu wa kutumia mitishamba, dua, makombe na hirizi ambao alifunzwa na wazazi wake (babake na mamake) kwa mapenzi makubwa na yeye (Bi Chani) kufanya juhudi kuweza kuipata elimu hiyo (uk 110)

Kama hiyo haitoshi, hata Mwavile aliweza kupata elimu ya utabibu kutoka kwa mamake wa kulea Bi Chani na aliweza kutoa matibabu hayo vyema kwa wagonjwa akiwemo kaka yake Abuu kama anavyosema mwandishi. (uk 138)

Kwa haki zaidi, Nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia utafiti huu imeweka wazi kuwa dhana ya utabibu wa kienyeji bado unaendelea katika zama hata hizi ingawaje kwa kiasi fulani umepungua na idadi kubwa ya watu au wagonjwa hupelekwa hospitali kwa ajili ya kupata matibabu ya kisasa yanayoshirikisha vipimo vya uhakikia kwa kiwango kikubwa. Nadharia ya Fasihi Linganishi ni msingi mmoja wapo unaoonesha pamoja na kwamba jamii hubadilika lakini kuna baadhi ya mambo hubadilika taratibu na mengineyo kwa haraka kimaendeleo iiwa ni pamoja na mabadiliko ya utoaji wa huduma za afya.

### 4.7.6 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe Kwa Mwanamme

Kwa hakikia katika jamii zetu wako baadhi ya wanawake wanaoendesha biashara ya danguro na ukahaba. Biashara hii ni ile tabia ya baadhi ya wanawake kujishughulisha katika kuuza miili yao kwa wanaume kwa lengo la wanaume hao kujitosheleza mahitajio yao ya kimwili (kimapenzi). Tabia hii bado inaendelea kushika kasi katika jamii mbalimbali ikiwemo jamii ya watanzania. Pamoja na hilo baadhi ya wanawake wamekuwa wakitumika kama chombo cha starehe kwa wanaume. Tabia hiii huweza kusababisha kuendelea kwa maradhi hatari yakiwemo yale ya UKIMWI na mengineyo. Mwanamke kutumika kama chombo cha starehe kwa mwanamme ni tabia ambayo imejitokeza na kufanana katika riwaya zoe mbili teule. Kwa mfano, kupitia riwaya ya *Utengano,* mtafiti amebaini kuwa baadhi ya wasimamizi na wamiliki wa hayo madanguro ni wanawake. Mwandishi katika kulifafanua hilo amemtumia mama Jeni ambaye alikuwa mmiliki wa danguro huko Pumziko. Biashara ya kuuza miili kwa wanaume iliendeshwa na mama Jeni kupitia Maimuna na Dora ingawaje Maimuna hakuwa tayari kuuza mwili wake kwa James (uk 56 - 57).

Utafiti huu umebaini kuwa baadhi ya wanawake hawako tayari kutumika kama bidhaa au chombo cha kumstareheshea mwanamme kingono. Hali hii inastahiki kuungwa mkono na jamii nzima. Kwa upande mwengine mwanamke ametumika kama chombo cha starehe kwa mwanaume kwa lengo la kujipatia fedha na tamaa. Mfano mzuri ni kupitia kwa muhusika Dora katika danguro la mama Jeni (uk 64 - 65). Mbali na hayo mapenzi, mwanamke ametumika kama chombo cha starehe katika kutoa burudani ya kuimba ikiwa ni sehemu ya kazi zake. Mfano mzuri ni

Maimuna alipokuwa muimbaji kule Rumbalola Hotel (uk 124 -125). Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena*, utafiti huu mtafiti amegundua kuwa usawiri wa mwanamke kama chombo cha starehe umejitokeza kupitia Bwana Toba kwa kuwatumia wake zake pamoja na Masuria wake (uk 112 - 113).

Nadharia ya Fasihi Linganishi inatoa picha kamili kuakisi na kufanana kwa usawiri wa muhusika mwanamke kutumika kama chombo cha starehe kwa mwanamme kuanzia hapo zamani hata kabla ya miaka ya 1980 ukilinganisha na sasa miaka 2014/2016. Hii imedhihirisha tabia ya kutumika mwanamke kama chombo cha starehe bado inaendelea katika jamii zetu. Mtafiti anawataka wanawake na jamii kwa ujumla wasiwe tayari kutumiwa kama bidhaa ya kumstarehesha mwanamme kwa maslahi binafsi isipokuwa kwa wale wanaostahiki kwao (mume wa ndoa)

Kwa hakika kabisa riwaya ya *Utengano* ya mwaka (1980) na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ya mwaka (2014) ni riwaya za mwandishi mmoja ambaye pamoja na kuandikwa kwa vipindi tofauti (miaka thelathini na nne) zimepishana bado zimedhihirisha kuwepo kwa usawiri wa mwanamke hususan katika baadhi ya maeneo. Maeneo ambayo mwanamke amesawiriwa na kufanana kwa riwaya hizo mbili teule ni pamoja na: Mwanamke kama muhusika mwenye Mapenzi ya dhati, Msimamo thabiti, Muwajibikaji, Mlezi wa familiya, Daktari/tabibu wa kienyeji na Chombo cha starehe kwa mwanamme.

Kwa misingi hiyo mtafiti kwa kutumia Nadharia ya Fasihi Linganishi ameona kuwa matendo hayo bado yameendelea kuchukuwa nafasi katika maisha ya kila siku ya

jamii husika ikiwa ni pamoja na jamii ya Watanzania. Hivyo basi mtafiti anasisitiza mema yaendelezwe na maovu ni yaachwe kwa maslahi ya wanawake wenyewe na umma.

**Jadwali 4.3: Muhtasari wa Kufanana Kwa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena**

| Na. | **Utengano** | **Kamwe Si Mbali Tena** |
|---|---|---|
| 01 | Mapenzi ya dhati | Mapenzi ya dhati |
| 02 | Msimamo thabiti | Msimamo thabiti |
| 03 | Muwajibikaji (bidii katika kazi) | Muwajibikaji (bidii katika kazi) |
| 04 | Mlezi wa familiya | Mlezi wa familiya |
| 05 | Tabibu/daktari wa kienyeji | Tabibu/daktari wa kienyeji |
| 06 | Chombo cha starehe | Chombo cha starehe |

Chanzo: Data kutoka riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena, 2016

## 4.8 Kutofautiana Kwa Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena

Kwa hakika riwaya ya *Utengano* (1980) na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* (2014) ni riwaya adhimu katika kumsawiri mwanamke katika hali zote za hasi na chanya. Pamoja na kwamba riwaya hizi zimemsawiri mwanamke katika hali zote mbili (hasi na chanya) mtafiti katika tathmini yake ya utafiti huu amebaini kuwa riwaya hizi teule zimetafautiana kwa wastani wa asilimia sabiini (70%) katika kumsawiri mwanamke. Kwa misingi hiyo mtafiti amebaini kuwa kutofautiana kwa riwaya hizi katika kumsawiri mwanamke kumetokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kimazingira, kiwakati, kidini, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kihistoria. Mtafiti ameona kuwa tofauti hizi zinaweza kuendelea kukua au kupungua kulingana na mabadiliko ya jamii kwa ujumla wakiwemo na wanawake wenyewe.

Kwa kuzingatia kutofautiana kwa usawiri wa mwanamke katika riwaya teule, mtafiti amerejelea swali la msingi la tatu la utafiti huu lisemalo: Ni kwa tofauti gani za usawiri wa mwanamke zinazojitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?* Swali hili limekwenda sambamba na lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lisemalo: Kutofautisha usawiri wa mwanamke kaika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*. Kwa ujumla uchambuzi wa swali la tatu la utafiti na lengo mahsusi la tatu la utafiti huu umeambatana na muendelezo wa Nadharia ya Fasihi Linganishi kwa kuzingatia kutofautiana kwa riwaya hizo teule kama ifuatavyo:

### 4.8.1 Mwanamke Kama Muhusika Mshauri Mwema

Ushauri mwema ni hatua muhimu kubwa katika kujenga familia na jamii kwa ujumla. Ushauri mwema ni ule utakaowezesha kurutubisha familia au jamii yeyote kwa ukamilifu wake. Katika riwaya ya *Utengano* mtafiti amebaini mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushauri juu ya maendeleo na afya ya familia. Utafiti huu umebaini jinsi Maimuna anavyomshauri mama yake Bi Tamima kuvunja miko ya utawa wa nyumba ya Bwana Maksuudi (mumewe na baba wa Maimuna na Mussa) ili apelekwe hospitali au aitiwe daktari ambaye atamsaidia kujifungua (uk 20).

Kwa upande mwengine, suala la ushauri mwema limejitokeza tena kupitia kwa muhusika Dora. Mara tu Maimuna alipoamua kuhama Pumziko baada ya kusingiziwa kuwa mwizi na Mama Jeni, Maimuna alikosa mwelekeo na hakujua wapi aelekee ndipo Dora alipomshauri na kumuomba kwenda Bobea kwa Biti Sururu. Ombi na ushauri huo Maimuna aliukubali na Dora alimpa shilingi mia mbili akiamini zitamsaidia (uk. 85)

Kwa kutumia Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amebaini kuwa ni kwa kiasi kikubwa dhana ya mwanamke kutumika kama muhusika mshauri mwema imejitokeza katika riwaya ya *Utengano* kuliko riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena.* Data ambazo mtafiti amekusanya ameona kuwa katika riwaya ya *Utengano* pamoja na kuwa ni ya zamani (1980) lakini imempa fursa mwanamke na kumuona ana uwezo mkubwa wa kushauri kwa maendeleo ya familia na jamii kwa ujumla ukilinganisha riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ambapo katika usawiri huu mwanamke hakuonekana na kutofautika kwa kiwango kikubwa akiwa kama mshauri mwema. Hivyo basi mtafiti ameona kuwa bado mwanamke ni mtu muhimu katika kushauri mambo muhimu ya kimaendeleo ya jamii zetu.

### 4.8.2 Mwanamke Kama Muhusika Jasiri na Mwenye Kujitolea Mhanga

Ni fakhari na utakaso kwa binaadamu kuwa na Ujasiri na kuweza Kujitolea muhanga, kufa au kupona katika jambo ambalo litaleta tija au kuokoa uhai wa mtu ingawaje hata huyo anayejitolea mhanga huhatarisha uhai wake. Mtafiti kupitia riwaya ya *Utengano* amegundua kuwa mwanamke ana nafasi kubwa ya kuwa jasiri na mwenye kujitolea mhanga ili kuokoa maisha yake au maisha ya wengine katika misingi ya halali. Jambo hili ni mfano mwema wa kuigwa katika maisha yetu ya kila siku. Utafiti huu umegundua kuwa juhudi za Biti Kocho kuwa jasiri na kujitolea mhanga kuokoa maisha ya Bi Tamima zilikuwa za msingi wakati Bi Tamima alipokuwa anaadhibiwa na Bwana Maksuudi kwa sababu ya kujifungua kwake na kutoroka kwa Maimuna (uk 49 - 52). Mfano mwengine ni Kazija alikuwa jasiri na alijitolea mhanga kueleza tabia mbaya za Bw. Maksuudi na Bw. Zanga katika mkutano wa kampeni za Ubunge pasi na kujali lolote linaloweza kumtokea. Mfano

Kazija alisimulia maovu ya Bw. Maksuudi ili jamii ione hafai kuwa kiongozi wa umma wakati alipokuwa anagombania ubunge (uk 81).

Kwa kutumia Fasihi Linganishi imetoa mwamko mkubwa kupitia wanawake na kuonesha mwanamke si mtu lelemama na anaweza kujitolea mhanga katika kutetea na kupinga matendo au matukio yasiyofaa katika jamii zetu. Mtafiti amegundua kuwa hadi leo tunawaona wanawake wengi wa Kiafrika wakijitolea mhanga katika kupinga masuala nyeti ya kijamii kupitia Taasisi zao mbalimbali. Tathmini ya mtafiti imeelekezwa zaidi katika kumuona mwanamke yuko mstari wa mbele kuokoa maisha ya mwanamke mwenzake, mtoto na jamii, hali hii ikiwa tofauti ukiilinganisha na riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena* ambayo pamoja nayo imemsawiri mwanamke lakini ni katika kiwango cha chini kisichoifikia riwaya ya *Utengano*.

### 4.8.3 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Tabia ya Ushawishi na Uchochezi

Kwa hakika, tabia ya Ushawishi na Uchochezi ni katika matendo maovu yanayotendwa na baadhi ya watu wakiwemo wanawake na hayana faida kwa muhusika au jamii. Mtafiti amebaini kuwepo kwa tabia hii kwa baadhi ya wanawake ambao ushawishi au uchochezi wao ni kufikia malengo mahsusi binafsi. Kwa mujibu wa riwaya ya *Utengano,* mwandishi amemtumia Biti Kocho kumshawishi Maimuna ili atoke na aongozane nae kwenda kumtafuta mkunga ambaye atamsaidia mama yake kujifungua (uk 22 - 24).

Ushawishi na uchochezi huu ulifanyika kwa sababu Maksuudi aliiweka familiya yake katika utawa. Mbali na hilo ilikuwa ni mpango wa Biti Kocho, Bi Farashuu na

Kazija kumtenganisha Maimuna na wazazi wake au familiya kwa ujumla. Pia haya yalitendeka kwa lengo la kulipiza kisasi cha kumdhulumu na kusabaisha kifo cha mwanawe Bi Farashuu ambaye ni Mwanasururu aliyekuwa mke wa Bwana Makusuudi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Fasihi Linganishi, usawiri huu wa mwanamke kama mwenye tabia ya ushawishi na uchochezi umekuwa wa tofauti ukilinganisha na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ambayo mtafiti hakuona ikitiliwa mkazo. Hii ina maana kuwa katika kipindi cha sasa tabia hizi za ushawishi na uchochezi zimeonekana kupungua katika jamii zetu ukilinganisha na hapo awali. Wanawake wanaonekana wameanza kustaarabika na kujitambua kwa kiasi kikubwa kwa kuachana na tabia hizo potofu.

### 4.8.4 Mwanamke Kama Muhusika wa Mipango na Hadaa

Mipango na Hadaa ni miongoni mwa matendo ambayo yanaendelea kuchukua nafasi katika maisha yetu ya kila siku na athari zake huweza kuwa kubwa. Kwa hakika, katika utafiti huu, kwa mujibu wa riwaya ya *Utengano*, mtafiti amegundua juhudi, mipango na hadaa ya Kazija, Biti Kocho, Bi Farashuu walizozitumia ili kuwatenganisha Bwana Maksuudi na familiya yake wakiwemo wanawe Maimuna na Mussa (uk 32). Mbali na hayo mwandishi amefafanua juhudi, mipango na hadaa za Biti Kocho na Bi Farashuu kumtorosha Maimuna kutoka nyumbani kwao kwa Bwana Maksuudi usiku na ikawa ndio sababu ya kumtenganisha na wazazi wake (uk 40 – 41).

Hapana shaka utafiti huu umekuwa muhimu kwa kuwa umesadifu namna mipango

na hadaa zinaweza kuchukua nafasi katika kutimiza malengo ya wahusika mbalimbali kama ilivyotimia kwa Bi Farashuu na Biti Kocho kumtenganisha Maimuna na familiya yake.

Mtafiti kupitia Nadharia ya Fasihi Linganishi, amebaini kuwa kuna tofauti ya usawiri wa mwanamke katika riwaya *Utengano* ukilinganisha na *Kamwe si mbali tena.* Mtafiti kupitia data zilizokusaywa amegundua kuwa wanawake wana nafasi kubwa katika kuhamasishana kuhusu maendeleo yao na taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kukemea na kuachana na tabia ya hadaa kwa wenzao au wengineo. Nadharia ya Fasihi Linganishi katika muktadha wa mtafiti kupitia riwaya hizi mbili imeonesha kuwepo kwa tofauti ya matendo ya wanawake kutoka katika tabia za hadaa na mipango kama ilivyo katika *Utengano* (1980) kwenda tabia za mwelekeo mzuri katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* (2014) hadi sasa (2016) Hii ina maana wanawake wameanza kpango ya kubadilika na kuhangaikia mipango ya kimaendeleo.

### 4.8.5 Mwanamke Kama Muhusika Dhaifu na Masikini

Dhana ya Udhaifu, kuonewa na kushindwa kujitetea ni miongoni mwa matatizo makubwa yanayoendelea kuwakabili wanawake duniani kwa sababu ya hali zao kuwa ni masikini. Mtafiti amebaini kuwa matatizo ya aina hii huwafanya wanawake wakati mwengine wakose haki zao za msingi kama matunzo, kuhudumikiwa na mapenzi ya dhati hususan kutoka kwa waume zao. Wakati mwengine matatizo haya huchangiwa kwa kuwa wanawake hao ni masikini na kiafya ni dhaifu kuliko wanaume katika ndoa. Utafiti huu  umedhihirisha kuwa baadhi ya wanawake ni

tegemezi kwa asilimia karibu mia ya mahitajio yao yote kwa waume zao na hulazimika kukubali kukumbwa na visa na mikasa, maonevu na udhalilishaji bila ya kujali kipindi walicho kama cha ugonjwa, ujauzito au mara tu baada ya kujifungua au kuwa kwenye utawa wa mume. Hali hii inapojitokeza hushindwa kuthaminika na kwao kukosa mwelekeo pindi wanapoachwa.

Katika kulifafanua hilo, kwa mujibu wa riwaya ya *Utengano,* mwandishi amemtumia Bi Tamima ambaye aliadhibiwa vikali na mumewe Bwana Makusuudi kwa sababu tu ya kujifungua na kutokuwa muwazi kumtaja aliyemzalisha na pia kwa kutokusema Maimuna amekwenda wapi; hali ya kuwa hata Bi Tamima hakujua namna alivyotoroka Maimuna. Bi Tamima alishindwa kujitetea na kwa sababu hakujua vipi ataendelea kuishi na kwa sababu ni masikini asiye na mwelekeo. Kwa misingi hiyo aliadhibiwa vikali pamoja na kwamba aliomba msamaha (uk.48 - 49) Mbali na Bi Tamima, hata Mwanasururu ambaye alikuwa mke wa Bwana Maksuudi na mtoto wa Bi Farashuu, sababu ya kifo chake ilitokana na kupigwa na kudhulumiwa mali yake na Bwana Maksuudi na kuachwa masikini (uk 60)

Kwa mujibu wa Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amebaini kuwa katika riwaya ya *Utengano,* wanawake walikuwa ni tegemezi zaidi kwa wanaume tofauti na riwaya ya *Kamwe si mbali tena* ambako sasa wameamka na wamekuwa na msaada mkubwa katika kufanya kazi na kuepuka utegemezi ikiwa ni pamoja na kazi za ujasiriamali au biashara ndogondogo za kuwafanya wasiweze kuonewa hususan katika kutetea haki zao na kudhalilishwa na wanaume bila ya sababu za msingi. Ingawaje msingi

mkubwa wa utetezi wao umetakiwa uzingatie Haki na Sheria za nchi husika kwa usahihi.

### 4.8.6 Mwanamke Kama Mhusika Mtenda Rushwa

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa na mtafiti, kupitia riwaya ya *Utengano*, utafiti huu umebaini tabia ya baadhi ya wanawake kutoa rushwa ya fedha kwa malengo tu wasaidiwe kufanikisha mahitajio yao. Kwa mfano serekali ya Tanzania kupitia TAKUKURU imeendelea kupambana na wale wanaotoa na kupokea rushwa. Katika kulieleza hilo, katika riwaya ya *Utengano*, mwandishi amemtumia muhusika Biti Kocho ambaye aliomba akopeshwe fedha na Bi Farashuu ili akampe rushwa karani anayehusika na viwanja ili na yeye ifanyike mipango ya kupata kiwanja (uk 62).

Kwa ujumla, kwa mujibu wa Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amegundua kuwa, tabia hii ya kutoa na kupokea rushwa bado inaendelea katika jamii zetu kutoka ngazi za juu hadi za chini. Mbali na hilo kutoka sekta na taasisi binafsi hadi taasisi za serekali, jambo ambalo hurejesha nyuma haki za walio wengi na kufinyaa kwa maendeleo ya jamii husika. Pamoja na hayo dhana ya Mwanamke kama muhusika mtenda rushwa kwa mujibu wa mtafiti haikuonekana kwenye riwaya ya *Kamwe si mbali tena*. lakini imejitokeza katika riwaya ya *Utengano.*

Hii inamaanisha jamii ya sasa nayo imeanza kutambua athari za rushwa na wanawake kwa umoja wao wanaungana na serekali na taasisi binafsi kupiga vita uozo huo, ingawa bado wako wachache wanaendeleza.

### 4.8.7 Mwanamke Kama Muhusika Mlevi

Tatizo la ulevi bado ni miongoni mwa tabia mbaya ambayo baadhi ya watu huendeleza. Ulevi katika jamii yeyote una athari kubwa na huchangia kurejesha nyuma maendeleo ya taifa. Hii ni kwa sababu wale wanaoendekeza ulevi hushindwa kutimiza majukumu yao ya kikazi ipasavyo. Pia ufanisi katika kazi hukosekana kwa sababu watendaji ni walevi. Akili zao huwa haziko timamu. Katika riwaya ya *Utengano,* mtafiti amebaini baadhi ya wahusika wakiwemo wanawake wamekuwa wakiendesha biashara ya ulevi na baadhi ya wanywaji pia ni wanawake. Miongoni mwa wahusika wanawake wanaojishughulisha na ulevi ni pamoja na Biti Sururu, Kijakazi na Maimuna (uk 91). Mfano zaidi na uhalisia wa afya ya Maimuna baada ya kuendekeza ulevi (uk 135).

Kwa mnasaba wa misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti ameona kwamba suala la ulevi limetamalaki mno katika riwaya *Utengano* na bado halijajitokeza katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena*. Makusudio ya mtafiti kupitia data zilizokusanywa na tathmini yake ni kwamba jamii ya sasa pamoja na kwamba wako baadhi ya wanawake ni walevi lakini kundi kubwa limeamua kuachana na tabia hiyo mbaya na kujishirikisha katika mipango ya kimaendeleo. Mtafiti ameona kuwa Mabadiliko haya yanasawiri kikamilifu na maisha yanayohitajika kwa wanawake wa sasa na jamii kwa ujumla.

### 4.8.8 Mwanamke kama muhusika Mgomvi (mshari)

Hakuna shaka kuwa tabia ya ugomvi au ushari bado imezoeleka kwa baadhi ya wanawake katika jamii zetu. Baadhi ya wanawake huwa na tabia hii mbaya na hatma

yake huweza kuleta athari kubwa kwa jamii ikiwa ni pamoja kuvunjika kwa uhusiano (urafiki), kuendelea kuwepo kwa visasi, matusi, uhasama nk. Katika utafiti huu, kwa mujibu wa riwaya ya *Utengano,* mtafiti amebaini kuwa tabia hii mbaya kupitia wahusika wake Kijakazi na Maimuna ambao baadae walipigana na kuumiza vibaya (uk 139 na 143).

Kwa kuhusisha na Nadharia ya Fasihi Linganishi, tumeona kuwa suala la ushari na ugomvi limepewa nafasi kubwa katika riwaya ya *Utengano* lakini halijajitokeza na ni tofauti katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena*. Kwa misingi hiyo mtafiti kupitia data zilizokusanywa na mtafiti ameona kwamba katika maisha ya sasa ugomvi na ushari hauna nafasi ya kuendelea kuwepo na ni vyema ukaachwa si kwa wanawake tu lakini hata wanaume. Mtafiti ameona kuwa ugomvi na ushari si miongoni mwa mtaji na sifa au utukufu kwa mwanamke bali ni aibu na fedheha kwa mwanamke anayetabua thamani na heshima yake vyema. Kwa ujumla wanawake ni watu wa kuheshimiwa na kuthaminiwa, kuenziwa na kuhudumikiwa na sio kujiingiza katika tabia hii mbaya.

### 4.8.9 Mwanamke Kama Muhusika Mtambuzi Na Mwanahistoria

Katika jamii yeyote suala la kutambua historia lina umuhimu wake. Historia ni somo lenye thamani tosha kwa vizazi vya leo na vile vya kesho. Jamii yeyote huweza kujifunza matukio mbalimbali yanayotokea duniani kwa yaliyo mema na yaliyo maovu na mwishowe huwa ni mafunzo makubwa kwa jamii husika.

Kwa kurejelea riwaya ya *Kamwe si mbali tena (2014),* utafiti huu umedhihirisha kuwa mwanamke anamchango mkubwa katika utambuzi wa historia ya jamii yake na

jamii nyenginezo. Jambo ambalo huwa ni msingi wa kuwafunza wengineo. Data zilizokusanywa zimethibitisha kuwa Bi Chani, ana uwezo mkubwa wa kusimulia matukio ya zamani mno kwa usahihi na kuwa ndio somo kwa watoto wake na wengineo ingawaje alikuwa tayari ni bibi kikongwe anayehitaji kuhudumiwa kila wakati (uk 89 - 90).

Kwa kurejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amebaini kuwa suala la kumfanya mwanamke kuwa na uwezo mzuri wa kutambua na kusimulia historia ya mambo na matukio yaliyopita halikuonekana katika riwaya ya *Utengano (1980).* Hali hii imetufanya tuamini kuwa wanawake wa miaka (1980) sio wale wa miaka (2014) au sasa (2016). Wanawake wa sasa wamekuwa na juhudi ya kutambua Jamii yao zaidi kwa lengo la kuitetea na kuandaa mipango ya kimaendeleo kama ilivyokuwa dhamira ya Bi Chani kwa jamii yake ya Visiwa vya Viungo.

### 4.8.10 Mwanamke Kama Muhusika Mpenda Dini

Tofauti ya usawiri wa mwanamke yamejitokeza pia katika dhana ya Dini. Dini ni muongozo katika maisha yetu ya kila siku. Mwanaadamu yeyote anawajibu wakuwa muumini wa kweli kwa mujibu wa dini yake. Mwanadamu huyo ana wajibu wa kuipenda dini hiyo na kutenda kama ambavyo Mwenyezi Mungu ametaka ili atakapokufa Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake na amjaalie awe ni miongoni mwa waja wa Peponi. Data ambazo mtafiti amezikusanya katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* zimedhihirisha usawiri wa mwanamke kuwa ni muhusika mpenda dini kupitia Bi Chani ambaye mwanzo alikuwa akiitwa Waridi / Warida au Mwanamkisi. Waridi (Bi Chani) alijifundisha kitabu cha Mungu kwa ilidili na kuhifadhi juzuu

thelathini za kitabu hicho na tafsiri yake kwa muda mfupi, baadae akahifadhi hadithi za Mtume (uk 108 - 109).

Nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia dhana hii ya Dini imeonekana kujitokeza zaidi katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* na kukosekana (kuwa tofauti) katika riwaya ya *Utengano*. Mtafiti ameona kuwa kupitia dini, wanawake wa jamii ya sasa wamebadilika sana na kwa kiasi kikubwa wamejielekeza katika ibada ingawaje wako wachache bado bidii yao ni ndogo katika dini. Hivyo ni ushauri wa mtafiti kwa jamii kuipenda dini na kuwa tayari kutenda mema na kuacha maovu ili iwe ni sababu ya kufaulu baada ya mauti.

### 4.8.11 Mwanamke Kama Muhusika Mwenye Huruma na Imani Thabiti

Kwa hakika kuwa na Huruma na Imani thabiti ni jambo linalohitajika na kila binaadamu  na kwa kila kiumbe. Kuachana na tabia ya unafiki, chuki, choyo, tamaa na mfano wa hayo si katika tabia njema na ni vikwazo vya ujenzi wa jamii imara na yenye mafanikio. Kwa mujibu wa data za utafiti huu imebainika kuwa  usawiri wa mwanamke katika suala zima la kumuhusisha na tabia njema ya Huruma na Imani thabiti kwa wanaadamu wenzake na viumbe vyenginevyo ni jambo la msingi na la kuzingatiwa. Katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* mtafiti kupitia data alizozikusanya amebaini tabia njema ya kuwa na Huruma na Imani thabiti kupitia kwa Mwavile ambaye aliwaombea kheri ndugu zake wende zao salama na wawe wenye kufanikiwa katika safari yao ya kutafuta maisha yenye mafanikio huko Ulaya. Mwandishi anasema (uk. 7)

Kwa kurejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amekuwa akisisitiza na kuunga

mkono umuhimu wa kuwa na huruma na imani kubwa katika familia na jamii kwa ujumla Huruma na imani thabiti ya mwanamke ina nafasi kubwa ya kujenga mapenzi, umoja na mashirikiano. Kama hiyo haitoshi mwanamke kuwa na huruma na imani thabiti kunamfanya mwanamke huyo awe nguzo muhimu katika kubadili na kuigwa na wale ambao hasira, chuki, hamaki, ugomvi na ushari umechukua nafasi katika maisha yao. Kwa hakika kwa mujibu wa data za mtafiti dhana ya huruma na imani thabiti imejitokeza zaidi katika riwaya ya *Kamwe si mbali tena* na kutoonekana (kuwa tofauti) katika riwaya ya *Utengano*. Hivyo basi imani na huruma kwa jamii ya leo imeonekana kuwa na thamani zaidi ukilinganisha na hapo zamani. Na hii imechangia wanawake wa sasa kubadilika na kuweza kuishi kwa kuthaminiana, kuhitajiana na kusaidiana.

### 4.8.12 Mwanamke kama Muhusika Mwanamabadiliko / Mageuzi.

Kwa hakika mabadiliko / mageuzi / mapinduzi katika jamii yeyote ni jambo la msingi na linastahili kupiganiwa katika jamii iliyojaa upotofu. Mapinduzi / mabadiliko hufanyika kwa lengo la kuimarisha maslahi ya umma. Kwa minajili hiyo, data zilizokusanywa na mtafiti kwa kurejelea riwaya ya *Kamwe si mbali tena* zimeweka wazi usawiri wa mwanamke kama ni muhusika mwana mabadiliko/ mageuzi. Mfano mzuri ni Bi Chani ambaye alikuwa na mwamko mkubwa wa kuleta mageuzi katika jamii yake (uk 65).

Bilashaka data zilizokusanywa zimedhihirisha kuwa, maswali ya msingi anayouliza Bi Chani yamelenga kuleta mwamko wa mabadiliko / mageuzi / mapinduzi / ukombozi kwa jamii ambayo imejaa ukandamizaji, udhalilishaji, ukatili na mauaji.

Bi Chani amehuzunishwa na kupinga vikali tabia hii ya maonevu kwa watu wa tabaka la chini na kuitaka jamii iamke na kusimamia upatikanaji wa haki sawa kwa wote.

Mtafiti kupitia Nadharia ya Fasihi Linganishi amebaini kuwa kuna tofauti kubwa baina ya riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena* na riwaya ya *Utengano*. Mtafiti ameona kuwa riwaya ya *Kamwe si mbali tena* imejitahidi kudhihirisha ushupavu wa Mwanamke ambaye amedhamiria kuleta mabadiliko katika jamii na ni muhusika ambaye si lelemama. Hali hii imeonekana ni tofauti na katika riwaya ya *Utengano* ambayo juhudi ya mwanamke bado ni ndogo kwa kuwa amekabiliwa na vikwazo vingi ikiwemo kuwekwa utawani kutoka kwa mume.

### 4.8.13 Mwanamke Kama Muhusika Yatima Anayehitaji Msaada

Binaadamu yeyote anayejitambua huwa na furaha ikiwa wazazi wake bado wako hai. Vilevile wazazi hao wakiwa wanajiweza, wana afya njema na wana mapenzi makubwa kwa mtoto au watoto wao. Kuwa yatima ni jambo linalotia huzuni na simanzi kwa yeyote. Kuwa yatima ni kuondokewa au kufariki kwa wazazi wa mtoto huyo. Mwanadamu yeyote wazazi wake wanapokufa hukosa muelekeo wa hali ya juu na hubaki katika majonzi makubwa. Wazazi ndio msaada mkubwa kwa mtoto katika kumjenga mtoto huyo katika misingi mema na yenye tija kimalezi. Katika utafiti huu, mtafiti ameweza kugundua uyatima wa mwanamke ambaye ni Mwavile. Mwavile alikuwa mwanamke ambaye wazazi wake walifariki wakati nyumba yao ilipopigwa na radi na yeye kuokoka kwa rehma za Mwenyezi Mungu. Wakati akiwa ni mdogo alikuchukuliwa na mjomba wake na baadaye kupelekwa kwa Bwana

Mansour na mkewe Bi Chani kwa lengo la kulelewa na kusaidia kazi za nyumba (uk 152).

Kwa hakika data hizi zimeweka wazi juhudi kubwa ya Bwana Mansour na Bi Chani kwa kumlea Mwavile kwa uwezo na juhudi zao zote na kumfanya kama mtoto wao wa kumzaa sawa na watoto wao nane ambao ni: Abuu, Salila, Yasir, Jokha, Sele Msulupwete, Zahran, Samira na Tambo.

Nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia riwaya ya *Kamwe si mbali tena* imetusaidia sana kuelezea umuhimu wa kuwalea vyema na kuwasaidia kwa kuwapatia huduma zote zinazostahiki kwa ukamilifu watoto yatima kama alivyofanya Bi Chani akishirikiana na marehemu mumewe Bwana Mansour kwa Mwavile. Dhana ya ulezi kwa watoto yatima imekuwa haikuonekana na ni tofauti kwenye riwaya ya *Utengano.* Kwa maana hii, mtafiti ameona kuwa hapo zamani katika jamii zetu na ukilinganisha na Jamii zetu za sasa kuna ongezeko la watoto yatima ambao walipoteza wazazi wao kwa sababu mbalimbali ikiwemo maradhi kama ya UKIMWI, kutelekezwa kwa sababu ya umasikini, ajali nk. Kwa ujumla watoto hao wanahitaji msaada wa hali ya juu tofauti na zamani ambapo kidogo tatizo hilo lilikuwa dogo au halikujitokeza hasa.

### 4.8.14 Mwanamke Kama Muhusika Msamehevu

Kila binaadamu ni mtenda makosa lakini mbora wa wote ni yule anayetambua makosa yake na akafanya haraka kuomba msamaha na asirejee tena kosa au makosa hayo. Tabia ya kusamehe au kusameheana ni jambo kubwa kwa binaadamu yeyote.

Kusameheana kunajenga upendo. Masikilizano, ushirikiano na kusaidiana. Kusameheana kunamwepusha mwanaadamu na chuki, husda, choyo, ubinafsi, tamaa, kiburi nk. Suala la kusamehe au kusameheana lina nafasi kubwa katika kujenga jamii yenye umoja na mashirikiano ambayo ni mojawapo wa silaha madhubuti ya kuleta maendeleo.

Kwa kurejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi, kupitia riwaya ya *Kamwe si mbali tena*, mtafiti kupitia data alizokusanya amebaini kuwa suala la kusameheana limejitokeza zaidi katika riwaya hiyo ukilinganisha na riwaya ya *Utengano*. Katika kulijadili hilo, mtafiti kupitia usawiri wa mwanamke, amemtumia muhusika Bi Chani ambaye alimsamehe mwanawe Jokha aliyepingana naye na kumdharau mama yake Bi Chani baada ya Bi Chani kumkataza asiolewe na Bwana Mzima. Baadaye Jokha alimtukana na kumdharau mama yake na kuolewa na Mzima. Mwisho wake Jokha alikuwa akipigwa, akidhalilishwa, na kuonewa na mumewe Mzima. Baada ya kutokea hayo, Jokha alitambua kosa lake na aliamuwa kwenda kwa mama yake kumuomba amsamehe na mama huyo akakubali kumsamehe kwa ukamilifu (uk 186 - 187). Hali hii imedhihirisha kuwa hakuna binaadamu mkamilifu na hakuna mzazi anayemchukia mwanawe. Mbali na hilo mzazi hususan wa kike (mama) ana moyo wa huruma na mapenzi zaidi kwa motto / watoto wake kuliko mzazi wa kiume (baba)

### 4.8.15 Mwanamke Kama Muhusika Msomi (Mwenye Elimu)

Maendeleo ya jamii au taifa lolote duniani linategemea raia wake na raia hao wawe wasomi (wenye elimu). Elimu ni msingi nambari moja katika kujenga jamii yenye

wataalamu na mafanikio makubwa kwa jamii au taifa lolote duniani. Maendeleo ya taifa lolote hutegemea juhudi za wataalamu ambao ndio wasomi katika fani husika. Elimu humuongoza mwanadamu kuwa mwema kwa kutenda yanayostahiki na kuacha yasiyostahiki kwa mujibu wa elimu na dini husika. Dini zote humtaka mwanaadmu asome ili aweze kutenda ibada na kazi zake kwa ufanisi na kisomi (kielimu).

Kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi, na kwa kurejelea riwaya ya *Kamwe si mbali tena* kupitia utafiti huu, data zilizokusanywa zinaweka wazi usawiri wa mwanamke kuwa ni msomi baada ya yeye kufanya juhudi katika masomo na kuweza kuitumia elimu yake vyema. Miongoni mwa wahusika wasomi (wenye elimu) na waliweza kuitumia vyema elimu yao ni pamoja na Bi Chani, Mwavile na Samira. Mwandishi ametutolea mfano mmoja wapo kupitia Samira (uk 200) Kwa upande mwengine Bi Chani alikuwa na elimu aliyoitumia vyema kwa kuusia, kutetea na kuelekeza na kuwafunza wanawe katika mfumo mzima wa maisha sahihi. Bi Chani alifanya juhudi katika masomo tangu mdogo na kupata mafanikio makubwa (uk 54).

Kwa hakika mtafiti amegundua kuwa suala la elimu limejitokeza sana katika riwaya *Kamwe si mbali tena* kwa kiasi kikubwa na halikuonekana au halikupewa nafasi hasa kwa wahusika wanawake katika riwaya ya *Utengano.* Makusudio ya tafsiri hiyo ni kwamba zama za sasa wanawake walio wengi wanaendelea kufanya juhudi katika kutafuta elimu ili waweze kujiajiri au kuajiriwa. Pia waweze kuwa msaada na watetezi wakubwa kwa familiya na Jamii zinazowazunguka. Wanawake waliowengi

wamebadilika na sasa wamekuwa wasomi wakubwa na wenye uwezo mkubwa katika fani mbalimbali kama Ualimu, Udaktari, Biashara, Uhasibu, Uongozi nk. Hii imewafanya waweze kujiamini na kuwa viongozi bora katika mataifa mbalimbali. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa kwa wanawake hao.

### 4.8.16 Mwanamke kama Muhusika Mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi

Baadhi ta wanawake wana tabia mbaya kama za Tamaa, Jeuri na Kiburi na huziendeleza katika maisha yao kwa tadi na inda au sifa bila ya kujali athari yake mbeleni. Msingi mzuri wa maisha sehemu yeyote ni kuwa na tabia nzuri / njema ambazo zitaleta faida katika familiya na jamii kwa ujumla. Tabia hizi mbaya (tamaa, jeuri na kiburi) huweza kumponza mwanaadamu na kumweka katika hasara au majanga makubwa. Hivyo basi ni vyema kwa kila mwanajamii kuziepuka.

Nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia riwaya ya *Kamwe si mbali tena* imesawiri kikamilifu hali hii kupitia wahusika mbalimbali alikwemo Jokha na Salila (uk 165). Kwa upande mwengine majadiliano ya Mwavile na Salila yanadhirisha chuki, kiburi na tamaa ya Salila kuhusu kuuzwa kwa shamba la Bi Chani kwa rafiki muengereza wa mume wa Salila ambaye ni Mabruki (uk 168). Kwa hakika data na dondoo hizo zinaweka bayana dhana nzima ya tamaa, jeuri na kiburi cha Salila kufikia kulazimisha kuuzwa hata shamba la mama yao kwa maslahi ya wachache na kwa kumridhisha mumewe. Jambo hili halikustahiki kufanywa na Salila na wale wenye tabia kama za Salila. Kwa upande mwengine dhana hizi za Mwanamke kama Muhusika Mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi hazikuonekana katika riwaya ya *Utengano.*

Mtafiti kupitia maelezo yaliyotangulia yamedhihirisha tathmini ya tofauti ya usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Kama yalivyoelekeza katika swali la msingi la tatu lisemalo:

iv) Ni kwa tofauti gani usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?*

Katika swali hili la msingi la tatu la utafiti huu, limekwenda sambamba na lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lisemalo: Kutofautisha usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*, mtafiti amebaini kuwepo kwa tofauti baina ya riwaya hizi mbili teule. Hivyo basi mtafiti amegundua kuwa pamoja na kuwepo kwa mfanano wa baadhi ya nafasi za mwanamke kwa (wastani wa asilimia thelethini) katika jamii lakini tofauti ni kubwa kwa (wastani wa asilimia sabiini) na hii imechangiwa na mambo mingi ikiwemo mabadiliko ya wakati, mazingira, dini, utamaduni, siasa, uchumi, nk yanayowakumba wahusika wenyewe na hata jamii kwa ujumla.

**Jadwali 4.4: Muhtasari wa Tofauti Ya Usawiri wa Mwanamke Katika Riwaya ya Utengano Na Kamwe Si Mbali Tena**

| Na. | **Utengano** | **Kamwe Si Mbali Tena** |
|---|---|---|
| 01 | Mshauri Mwema | Mtambuzi na Mwanahistoria |
| 02 | Jasiri na mwenye Kujitoa mhanga | Mpenda Dini |
| 03 | Ushawishi na Uchochezi | Mwenye Huruma na Imani thabiti |
| 04 | Mipango na Hadaa | Mwanamabadiliko/ mageuzi |
| 05 | Dhaifu na Masikini | Yatima anayehitaji msaada |
| 06 | Mtenda Rushwa | Msamehevu |
| 07 | Mlevi | Msomi (mwenye elimu) |
| 08 | Mgomvi (mshari) | Mwenye Tamaa, Jeuri na Kiburi |

Chanzo: Data kutoka riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena, 2016

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho yenye mada: Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni: Sehemu ya kwanza ni Muhtasari, sehemu ya pili imehusu Hitimisho na sehemu ya tatu ni Mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu mada ya utafiti isemayo: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena*. Huu ni Utafiti Linganishi. Utafiti huu uligawanywa katika sura tano zifuatazo: Sura ya kwanza ilihusu Utangulizi wa jumla. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na; Utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti (Lengo kuu na malengo mahsusi), Maswali ya utafiti, Umuhimu wa utafiti, Vikwazo vya Utafiti na utatuzi wake, Mipaka ya utafiti, Muundo wa tasnifu na Hitimisho.

Katika Utafiti, huu mtafiti aliongozwa na malengo ya aina mbili; Lengo kuu na malengo mahsusi. Lengo kuu lilikuwa ni: Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano na Kamwe si mbali tena.* Malengo Mahsusi yalikuwa matatu: (i) Kufafanua usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* (ii) Kufananisha usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* (iii) Kutofautisha usawiri wa

mwanamke katika riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Sambamba na hilo utafiti huu uliambatana na maswali matatu ya msingi: (i) Ni kwa vipi usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?* (ii) Ni kwa namna gani usawiri wa mwanamke umefanana katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena* (iii) Ni kwa tofauti gani usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?*

Sura ya pili ilihusu Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia. Kwa upande wa sura hii ilijumuisha mada ndogo ndogo zifuatazo; Utangulizi, Ufafanuzi wa Istilahi muhimu (mfano, Dhana ya Wahusika), Mapitio ya kazi tangulizi, Nadharia zilizotumika ni Ufeministi wa Kiafrika na Nadharia ya Fasihi Linganishi. Mwisho ni Hitimisho.

Sura ya tatu ilihusu Mbinu za utafiti. Katika sura hii vipengele vifuatavyo vilijadiliwa: Utangulizi, Maana ya mbinu za utafiti, Eneo la utafiti, na sababu za uteuzi wa eneo la Utafiti, Mbinu ya usampulishaji, Ukusanyaji wa data na Mbinu za ukusanyaji wa data, Mbinu za uchambuzi wa data zilitumika ambayo ni mkabala wa Kimaelezo, Zana / vifaa vya utafiti na mwisho ni Hitimisho.

Sura ya nne ilihusu Uwasilishaji, Uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa: Utangulizi, Usuli wa mwandishi – Said A. Mohamed, muhtasari wa riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*, Uchambuzi wa usawiri wa mwanamke katika riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

Sura ya Tano ni Muhtasari wa Utafiti, Hitimisho na Mapendekezo.

Kwa ujumla kulingana na mada husika ambayo ni: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si mbali tena: Utafiti Linganishi.* Mtafiti kwa kurejelea data zilizokusanywa na uchambuzi wake, riwaya hizi zimefanana kidogo (wastani wa asilimia thelathini) ukilinganisha na kutofautiana kwake (wastani wa asilimia sabiini) katika usawiri wa mwanamke. Hali hii imechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo za kimazingira, kiwakati, hisoria, dini, siasa, uchumi na utamaduni. Sambamba na hilo uchambuzi wa utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi ya utafiti. Kwa muhtasari ufafanuzi wa malengo mahsusi hayo ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu ilikuwa ni: Kufafanua usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Lengo hili liliongozwa na swali la msingi la kwanza lisemalo: Ni kwa vipi usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?*

Katika Utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa riwaya mbili hizi teule zimemsawiri mwanamke katika hali mbili (chanya na hasi). Kwa mfano katika riwaya ya *Utengano;* Mwanamke amesawiriwa kama muhusika Mshauri mwema, Jasiri na mwenye kujitoa mhanga, Mwenye msimamo thabiti, Mlezi wa familiya, Mapenzi ya dhati, Muwajibikaji, Tabibu na daktari wa kienyeji, Ushawishi na Uchochezi, Mipango na Hadaa, Mlevi na Mgomvi / Mshari, Dhaifu na Masikini, Chombo cha starehe na Mtenda rushwa.

Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe si mbali tena,* mtafiti aligundua mwanamke amesawiriwa katika hali / tabia zile zile mbili (chanya na hasi). Kwa mfano, Mwanamke amesawiriwa kama muhusika Muwajibikaji, Mtambuzi na Mwanahistoria, Mpenda dini, Huruma na mwenye Imani thabiti, Mwanamabadiliko, Msamehevu, Tabibu / daktari wa kienyeji, Mlezi wa familiya, Chombo cha starehe, Yatima na anayehitaji msaada, Jeuri, Kiburi na mwenye tama. Ni vyema mema yakafuwatwa na maovu yakaachwa.

### 5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu ilikuwa ni: Kufananisha usawiri wa mwanamke katika riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Lengo hili lilikitwa katika swali la msingi lisemalo: Ni kwa namna gani usawiri wa mwanamke umefanana katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.*

Utafiti huu ulibaini kuwa, riwaya hizi teule katika kufanana kwa usawiri wa mwanamke umejitokeza kama ifuatavyo: Mwanamke amesawiriwa kama muhusika mwenye Mapenzi ya dhati, Msimamo thabiti, Muwajibikaji, Mlezi wa familiya, Tabibu / daktari wa kienyeji na Chombo cha starehe kwa mwanamume. Kwa makusudio hayo riwaya hizi pamoja na kwamba zimetofautiana kwa miaka (34) lakini bado kuna baadhi ya tabia chache zimeonekana kufanana kwa wastani wa asilimia thelathini (30%).

### 5.2.3 Lengo Mahsusi la Tatu

Katika utafiti huu, lengo mahsusi la tatu lilikuwa ni: Kutofautisha usawiri wa mwanamke katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena.* Lengo mahsusi

hili liliongozwa na swali la msingi la tatu lisemalo: Ni kwa tofauti gani usawiri wa mwanamke umejitokeza katika riwaya teule za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena?*

Kwa ujumla riwaya hizi zimetofautiana kwa wastani wa asilimia sabiini (70%) kaika kumsawiri mwanamke. Kwa mfano katika *Utengano* mwanamke amesawiriwa kama muhusika mshauri mwema, jasiri na mwenye kujitolea mhanga, ushawishi na uchochezi, mipango na hadaa, dhaifu na masikini, mtenda rushwa, mlevi, na mgomvi (mshari). Kwa upande wa riwaya ya *Kamwe si mbali tena* mwanamke amesawiriwa kama muhusika mtambuzi na mwanahistoria, mpenda dini, mwenye huruma na imani thabiti, mwanamabadiliko / mageuzi, yatima anayehitaji msaada, msamehevu, msomi (mwenye elimu), mwenye tama, jeuri na kiburi.

### 5.3 Hitimisho

Kwa kuhitimishia, tunaweza kusisitiza kuwa mwanamke ni muhusika binaadamu kama walivyo wanaadamu wengineo. Ni muhusika mwenye uwezo mkubwa wa kutenda matendo mbalimbali ambayo hugawanywa katika sehemu mbili kuu. Matendo mema (chanya) na matendo maovu (hasi). Mtafiti amegundua kuwa kuna tofauti baina ya usawiri wa mwanamke katika maisha ya zamani (riwaya ya *Utengano* ya mwaka 1980) na usawiri wa mwanamke katika maisha ya sasa (riwaya ya *Kamwe si mbali tena,* ya mwaka 2014) hadi sasa (2016). Kwa udhati kabisa tathmini ya tofauti ya usawiri huo katika riwaya hizi mbili yanaakisi na maisha ya sasa kwa kuhusisha na matendo ya jamii ya leo na kumfanya mwanamke aonekane amebadilika zaidi tofauti na zamani. Hii inamaanisha kuwa mwanamke ni muhusika anayekwenda sambamba na mabadiliko ya wakati, historia, imani na ushiriki au

ushirikishwaji wake, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hali hii humfanya aendelee kuonekana ni mwenye thamani na kuhitajika.

## 5.4 Mapendekezo

Kwa udhati kabisa, kazi za utafiti wa aina yeyote duniani si kazi nyepesi. Ni kazi zinazohitaji utulivu, uvumilivu, muda wa kutosha na hata uwezo na taaluma ya kufanya utafiti wenyewe na hata gharama ya fedha. Utafiti huu umehusu: Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za *Utengano* na *Kamwe si mbali tena*: Utafiti Linganishi. Kwa hakika ni imani kubwa ya mtafiti ametimiza shauku aliyokusudia kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti kama ilivyoyangulia. Licha ya hayo, mtafiti ameona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutoa mapendekezo katika maeneo muhimu yafuatayo:

### 5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma

Wanataaluma kama vile wahadhiri, walimu, watunga mitaala, wasomi wengineo na wanafunzi hasa wa somo la Fasihi wana nafasi kubwa ya kukuza taaluma zao kwa kuzingatia maeneo muhimu ambayo bado hayajatafitiwa kwa mujibu wa utafiti huu. Kwa mfano mtafiti ametathmini kuhusu usawiri wa mwanamke baina ya riwaya ya zamani (*Utengano)* na riwaya mpya *(Kamwe si mbali tena)* pamoja na kufananisha na kutofautisha kwa riwaya hizo.Hii ina maana kuwa bado nafasi ya kuchunguza riwaya nyenginezo za mwandishi huyu na riwaya hii mpya (Kamwe Si Mbali Tena) inapatikana au kulinganisha na riwaya nyenginezo kutoka kwa mwandishi huyu (Said A. Mohamed) wa visiwani Zanzibar na waandishi wengineo wa Tanzania bara au kwengineko, Sambamba na kuzingatia matumizi ya Nadharia ya Fasihi

Linganishi. Mbali na hayo fursa nyenginezo zipo kwa upande wa vipengele vya Fani na Maudhui. Sambamba na hilo mada kama Ufasihi Simulizi, na matumizi ya Nadharia kama Fasihi Linganishi yana umuhimu wake kufanyiwa Utafiti katika maeneo mengine muwafaka.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Serekali

Kwa upande wa serekali ina wajibu wa kuhamasisha umuhimu wa kufanya tafiti za kitaaluma ikiwemo eneo maalumu la Fasihi ili kuweza kuimarisha taaluma hiyo katika maendeleo ya elimu nchini Tanzania na kwengineko duniani. Juhudi hizo za makusudi zitasaidia kuamsha ari ya wanajamii kujifunza na kuweza kuisaidia serekali katika maendeleo ya taifa kwa kuongeza idadi ya wasoni (wataalamu) waliobobea katika fani husika ikiwemo Fani ya Fasihi. Kwa mnasaba wa hilo, kwa kuwa utafiti ni gharama ni vyema serekali ikaandaa bajeti maalum kwa wanataaluma na wasomi chipukizi wa Fasihi kwa lengo la kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za Fasihi katika utanzu wa riwaya na tanzu nyenginezo za mwandishi huyu Said A. Mohamed au waandishi wengine wa Fasihi na kujenga ushindani wa kitaaluma na ikitumainiwa kuwa tasnifu hii ikiwa ni mojawapo wa marejeleo muhimu kwa wapenzi na wanataaluma wa Fasihi.

Kama hiyo haitoshi kupitia vyuo vikuu fani ya Fasihi ni vyema ikaendelea kutiliwa mkazo ikiwa ni pamoja na utunzi wa vitabu, tasnifu na makala nyengine za kitaaluma katika kiwango cha kuanzia Shahada ya kwanza, shahada ya Uzamili hadi shahada ya Uzamivu nk.au hata chini ya ngazi hiyo.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii ina dhima kubwa ya kujifunza taaluma mbalimbali ikiwemo taaluma ya Fasihi. Mtafiti anapendekeza kuwa wanajamii wawe na utamaduni wa kusoma vitabu kwa bidii ya kusudi. Utamaduni huu wa kusoma vitabu utasaidia sana kuongeza maarifa na kuwafanya wanajamii hao waweze kutenda yaliyo mema na kuacha yaliyo maovu. Sambamba na hilo tabia ya usomaji wa vitabu ikiwa ni pamoja na vitabu vya Fasihi kama Riwaya, Tamthiliya na Ushairi, Tasnifu na makala mengineyo ya kitaaluma ikiwemo tasnifu hii ni nyenzo muhimu katika kuinua upeo wa maarifa na akili kwa maendeleo binafsi hadi taifa kwa ujumla.

### 5.4.4 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Kwa hakika Utafiti huu ulichunguza vitabu viwili kati ya vitabu zaidi ya arubaini vya muandishi huyu (Saidi Ahmed Mohamed) vikiwemo vya Riwaya, Tamthiliya, Ushairi, na Hadithi Fupi nk. Baadhi ya vitabu hivyo ni kama vifuatavyo:

(i) **Ushairi**: *Sikata Tamaa (1980), Kina Cha Maisha (1984), Jicho la Ndani (2002).*

(ii) **Tamthiliya**: *Pungwa (1988), Kivuli Kinaishi (1990), Amezidi (1995), Kitumbua* **Kimeingia** *Mchanga (2000) pamoja na Profesa Kitula King'ei wameandika Posa za Bi Kisiwa (2007).*

(iii) **Riwaya**: *Asali Chungu (1977) , Utengano (1980), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza Katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990), Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Nyuso za Mwanamke (2010), Mhanga Nafsi Yangu (2012) Mkamandume (2013) na Kamwe Si Mbali Tena (2014).*

Kwa misingi hiyo mtafiti amependekeza kuwa ni fursa adhimu kuendelea kufanya utafiti kwa watafiti wengine katika maeneo mengine tofauti kwa kuzingatia Fani na Maudhui, pamoja na matumizi ya Nadharia hasa nadharia ya Fasihi Linganishi ambayo bado ni tunu katika Fasihi ya Kiswahii ili kuona ni vipi mwandishi anavyobadilika na kukuwa katika maeneo mbalimbali ya kazi zake za Fasihi.

## MAREJELEO

Adam, J. & Kamuzora, F (2008). *Research Methods for Business and Social Studies,* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Africa Gender Equality Index, (2015). Empowering African Women: An Agenda for Action – African Development Bank Group: African Development Bank.

Aiello, F. (1999). Mabadiliko ni maumbile: The Thematic and Stylistic Dynamism in S. A. Mohamed's Novel Utengano. *AAP,* 60, 59-65.

Ann, S. S. (2013). Usasa na Usasa wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya Said A.Mohamed. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Kiswahili; Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha,* Nairobi: Oxford University Press.

Bassnett, S. (1993) *Comparative Literature: A Critical Introduction.* Oxford: Blackwell.

Boldor, A. (2003). Perspective on Comparative Literature. A Thesis of Master of Arts in The Interdepartmental Program in Comparative Literature, Louisiana State University, USA.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods,* New York: Oxford University Press.

Buliba, S. (2014). *Misingi ya Nadharia na Utafiti,* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Limited.

De Beavoir, S. (1949). *The Second Sex*. London: Pan Book Publishers.

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learner's Dictionary,* (7th ed.), Oxford: Oxford University Press.

Eagleton, M. (1991). *Feminist Literary Criticism-Women in Literature*. London: Longman Publisher.

Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Forster, E. M. (1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, (2000). *Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia –Wizara* ya *Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto,* Dar es Salaam: Government Printer.

Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi, Dar es Salaam: Daud Publishing Company

Juma, K. B. (2008). *Utamaduni wa Mzanzibar.* Zanzibar: BAKIZA.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Madumullah, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Nairobi: Mture Educational Publishers Limited.

Massamba, D. (2009). *Kamusi ya Isimu na Lugha, Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, S. A. (1980). *Utengano.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed, S. A. (2014). *Kamwe si mbali tena*. Nairobi: Oxford University Press.

Mhando, P. & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho.*Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mwamzandi, I. (2013). Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi. *Swahili Forum*, 20 (2013), 48 – 66.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: EAEP Ltd.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1983). *Utafiti wa Fasihi Simulizi*. Katika, *Makala za Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two*: *Misingi ya Nadharia ya Fasihi Ya Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Nkwera, F. M. V. (1978). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TPH.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za Fasihi*, Augustana: Rock Island.

Osore, M. (2013). Magical Transformaions and the Subjugation of Nature in Said Ahmed Mohamed's Babu Alipofufuka. *International Journal of Humanities and Social Science,* 3(10), 132-136.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Dodoma: Karljamer Print Technology.

Remark, H. H. (1971). *Comparative Literature: Its definition and Functions.* Corbondale: Southern Illinois.

Ruto, M. C. (2015). Matatizo ya Mwanamke katia Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Kiswahili; Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Sengo, S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: AERA Kiswahili Researched Products.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Steady, F. C. (ed) (1981). *The Black Africa Cross – Cultulary:* Cambridge: Schenkman Publishing Company.

Traore, F. A. (2008) *Family and Society in Said Ahmed's Novels.* Swahili Forum 15.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

UN, (2014). *Gender Equality and Sustainable Development.* The Data Section of UN Women, United States: AGS Custom Graphics, RR Donnelly Company.

UN, (1995). *Beijing Declaration and Platform for Action: Beijing+5 Political Declaration and* Outcome. UN Women 2014.

Wanjiru, M. J. (2013). Uhalisia na Uhalisiajabu katika riwaya mpya: Babu Alipofufuka (Said Ahmed Mohamed) na Watu wa Gehenna (Tom Olali), Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Kiswahili; Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Walibora, K.W. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17 (2010): 143-157.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix Publishers, Nairobi, Kenya.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Wellek, R. & Warren, A. (1949). *Theory of Literature*, New York: Harcourt, Brace and Company.

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Women*. Harmondworths: Black Well Publishers.

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) Thousands Oaks California: SAGE Publishers.

Zepetnek, S. (1998). *Comparative Literature: Theory, Method, Application*: Amsterdam: Atlanta Rodopi.